

u DHANA NA MATNIZO YA TAFSIRI:
TATHMINI YA RISASI ZIANZAPO KUCHANUA. 4

OMONDI, F. OSANO

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza
baadhi ya mahitaji ya shahada ya M.A. katika
Chuo Kikuu cha Nairobi



1997

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa na mtu mwingine kutosheleza mahitaji ya shahada ya M.A. katika Chuo kingine chochote.



.....
Omondi, F. Osano
(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kwa mtihani chini ya usimamizi wetu, sisi tulioteuliwa kuisimamia.



.....
Dkt. Kineene Wa Mutiso
(Msimamizi)

.....
Mw. Rose Shake
(Msimamizi)

YALIYOMO

UKURASA

TABARUKU	i
SHUKRANI	ii
MUHTASARI	iv

SURA YA KWANZA

1.0: MWONGOZO WA TASNIFU	1
1.1: UTANGULIZI	1
1.2: TATIZO LA UTAFITI	3
1.3: MADHUMUNI YA TASNIFU	5
1.4: UPEO WA TASNIFU	7
1.5: SABABU ZA KUCHAGUA SOMO	8
1.6: HAIPOTHESIA	11
1.7: YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI	13
1.8: MISINGI YA KINADHARIA	18
1.9: NJIA ZA UTAFITI	28
1.10: HITIMISHO	29
1.11: TANBIHI	29

SURA YA PILI

2.0: DHANA MBALIMBALI ZA TAFSIRI	32
2.1: UTANGULIZI	32
2.2: DHANA YA TAFSIRI	33
2.2.1: AINA ZA TAFSIRI	43
2.2.2: TAFRISI ZA MOJA KWA MOJA	45
2.2.3: TAFSIRI MAANA	47

2.2.4:	TAFSIRI HURU	49
2.2.5	TAFSIRI MAWASILIANO	51
2.2.6:	TAFSIRI KIKAZI/KIHUDUMA.	53
2.2.7:	TAFSIRI WAZI - KINATHARI/KITUTUMBI	54
2.2.8:	TAFSIRI UJUMBE/HABARI	54
2.2.9:	TAFSIRI KIUTAMBUZI	55
2.2.10:	TAFSIRI KIAKADEMIKI	56
2.3:	MAWASILIANO KATIKA TAFSIRI.	57
2.4:	MUKTADHA KATIKA TAFSIRI	68
2.4.1:	MATATIZO YANAYOHUSIANA NA MUKTADHA	76
2.5:	DHANA YA MAANA KATIKA TAFSIRI	78
2.6:	TANBIHI	96

SURA YA TATU

3.0:	MATATIZO YALIYOSABABISHWA NA PUNGUFU UPANDE WA MTAFSIRI.	101
3.1:	UTANGULIZI.	101
3.2.0:	MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA GRAFOLOJIA.	102
3.2.1:	KUONGEZWA KWA ALAMA ZA GRAFOLOJIA KATIKA MP.	102
3.2.2:	KUFUTILIWA MBALI KWA ALAMA ZA GRAFOLOJIA KATIKA MP	104
3.3.0:	MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA FONOLOJIA	107
3.3.1:	KUONGEZWA KWA SAUTI KATIKA MP	107
3.3.2:	KUFUTILIWA MBALI KWA SAUTI KATIKA MP.	108
3.4.0:	MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA MOFOLOJIA	109
3.5.0:	MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA SINTAKSIA.	111
3.5.1:	KUGAWANYA MISHORORO YA MA.	111
3.5.2:	KUTAFSIRI MISHORORO YA MA. MOJA KWA MOJA KATIKA MP.	113

3.5.3:	KUFUTILIWA MBALI KWA BAADHI YA VIPENGELE KATIKA MP.	114
3.5.4:	KUFUTILIWA MBALI KWA MAFUNGU YA KISINTAKSIA KATIKA MP.	116
3.5.5:	KUONGEZWA KWA MAFUNGU ZAIDI KATIKA MP.	118
3.6.0:	MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA LEKSIA NA SEMANTIKI.	122
3.6.1:	MATATIZO YA LEKSIA	122
3.6.2:	MATATIZO YA SEMANTIKI	131
3.7.0:	MATATIZO YANAYOSABABISHWA NA HALI YA MTAFSIRI KUTOMAKINIKA KATIKA LUGHA	136
3.7.1:	MTAFSIRI KUWASILISHA UJUMBE USIOAFIKIANA KAMWE NA ULE WA MA.	137
3.7.2:	UAMBISHAJI MBAYA	139
3.7.3:	TAFSIRI ISIOZINGATIA KAIDA ZA KIMSINGI ZA LP.	142

SURA YA NNE

4.0:	MATATIZO KATIKA VIWANGO VYA MUKTADHA, UTAMADUNI, MAZINGIRA NA MASWALA MENGINE YANAYOSABABISHWA NA LUGHA.	145
4.1:	UTANGULIZI.	145
4.2.0:	MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA MUKTADHA.	145
4.2.1:	MATATIZO KUHUSIANA NA UTAMADUNI	149
4.2.2:	MATATIZO KUHUSIANA NA MAZINGIRA	153
4.3.0:	MATATIZO KUTOKANA NA MASWALA MENGINE KATIKA LUGHA	156
4.3.1:	TAFSIRI YA SEMI BILA YA KUZINGATIA THAMANI YA MA.	157
4.3.2:	KUBADILISHA TAMATHALI MOJA YA SEMI NA NYINGINE	159
4.3.3:	KUTUMIA LUGHA YA KAWAIDA KUTAFSIRIA MAFUNGU YA KITAMATHALI.	161

SURA YA TANO

5.0:	HITIMISHO	163
	MAREJELEO	167

TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wazazi wangu wpendwa, mama Christine, W. Okuome na baba Andrew, P. Okuome, ambao walinitunza vyema na kujinyima mengi ili nipate kufikia mahala nilipo hivi sasa.

Hali kadhalika nawatabarukia kakangu Bob, O. Osano na dadangu Jane Atieno.

Nashukuru sana kuwepo kwenu kwa ajili yangu kila mara.

SHUKRANI

Natoa shukrani za dhati kwa wote walionisaidia kwa namna tofauti katika masomo yangu. Kwanza kabisa shukrani za kipekee ziwaendee wasimamizi wangu, Dkt. Kineene wa Mutiso na Mw. Rose Shake, ambao waliniongoza vyema na kunipa mwanga ulionimulikia njia niliyoiabiria katika kazi hii. Wao walinishughulikia kwa mioyo mikunjufu kila nilipowaendea kwa ushauri.

Aidha nawapa shukrani mabingwa wa lugha walionisaidia kwa vitabu, majarida na makala ambayo yalinifaidi sana. Wahadhiri wakuu wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, wa Chuo Kikuu cha Nairobi; Prof. Mohamed, H. Abdulaziz, Prof. Okoth - Okombo, Prof. Marzouk Mohamed, Prof. Bakari, M., Dkt. Judith Nyagah, Dkt. Bureng Nyombe, Dkt. Kithaka Wa Mberia, Dkt. Marete, R.G.N., Bw. Mwenda Mbatia, Bw. Mumbo Mosoti, Bw. Muaka Lianza, Bw. Gichobi Mungania, Bw. Mgullu, Bw. Oloo, Bw. Hemedi, Bw. Michira, Bi. Cecilia Thandi na wafuatao kutoka Chuo cha Kikuyu; Bw. Ayub Mukhwana, Bw. John Habwe na Bw. Mbuthia.

Ubingwa wenu na changamoto mlionipa uliniwezesha kupiga hatua nyingi kiusomi, kila mara tulipozungumza pamoja.

Siwezi kuwasahau Prof. Nchimbi, Dkt. Gibbe na Mw. Oriedo wa Chuo Kikuu cha Moi, ambao walinipa msingi imara katika maswala ya lugha na kunihimiza kuendelea mbele. Nyote nawashukuru sana.

Kwa wakufunzi wenzangu; Kilelu Hannington, Osiemo Donald, Nyamberi Hezron, Olali Tom, Kariuki Ann, Mutie Edith, na Dhu Shun Fang, nashukuru sana kwa muda wote tuliokuwa pamoja, mlinifaidi kwa mambo mengi na kunihimiza kila mara tulipoogelea sote katika bahari

hii ya usomi. Nawatakieni kila la heri maishani.

Marafiki na jamaa zangu walionitakia heri na fanaka, nawashukuru kwa moyo wangu wote. Scola Adhiambo, pokea shukrani za kipekee kwa kuwa rafiki mwema. Niliufurahia uvumilivu wako na himizo ulionipa kila mara nilipozamia kazi hii. Nakutolea shukrani za moyo wangu.

Vilevile wahudumu wote wa maktaba ya Summer Institute of Linguistics, wa kule Dallas Marekani na wa hapa nchini Kenya, nawashukuru sana kwa kujitolea kwenu, kunisaidia bila ya masharti yoyote kila mara nilipohitaji vitabu na majarida ya kusoma.

Pia shukrani za kipekee ziwaendee wazazi wangu wapendwa, mama Christine Okuome na baba Andrew Okuome kwa kuyagharamia masomo yangu. Ama kweli natambua ya kuwa bila ya ukarimu na penzi lenu kwangu, safari hii singeikamilisha.

Kakangu Bob, ulinikimu na kujitwika mzigo wangu, nakushukuru sana; pia shangazi wangu Lilian na Eudia na wajomba Dkt. Onyango P.J. na Steve Otieno nawapa shukrani za dhati kwa usaidizi mlionipa.

Hali kadhalika shukrani za dhati nazitoa kwa Bi Julia Nangekhe aliyeipiga chapa tasnifu hii kwa ustadi na uvumilivu mwingi.

Ahsanteni nyote. Heri na fanaka ziwashukie.

MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia dhana na matatizo katika taaluma ya tafsiri. Maswala yote ambayo tumeyajadili yamegusia mada hiyo.

Kazi yenyewe tumeigawa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumetoa mwongozo wa tasnifu hii; ambapo tumezingatia, somo la utafiti tunautekeleza, madhumuni ya tasnifu, upeo wa tasnifu, sababu za kuchagua somo, tumetoa haipotesia vilevile na kurejelea yaliyoandikwa kuhusu somo hili, tukaelezea hata misingi ya kinadharia tuliyoitumia, hii ikiwa ni pamoja na; nadharia ya maana, nadharia ya mawasiliano na nadharia ya uchanganuzi wa usemi. Pia tumeelezea njia za utafiti tulizozitumia katika kazi hii.

Katika sura ya pili tumezingatia dhana muhimu zinazohusishwa na taaluma ya tafsiri. Hizo dhana ni kama; dhana ya tafsiri ambayo pia tumeihusisha na aina za tafsiri zinazopendekezwa na wananadharia wa tafsiri; dhana ya mawasiliano; dhana ya muktadha ambayo tumeijumulisha pamoja na matatizo kuhusiana na dhana ya muktadha, na kisha tumetazama dhana ya maana katika tafsiri.

Katika sura ya tatu, tumefanya uchanganuzi wa matatizo ya tafsiri katika Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), kwa jumla, matatizo tuliyoyashughulikia katika sura hii ni yale ambayo husababishwa na udhaifu au pungufu kadha wa kadha upande wa mtafsiri.

Katika sura ya nne hali kadhalika tumeshughulikia matatizo ambayo kwa jumla yalitokana na sababu ambazo mtafsiri hakuwa na uwezo wa kuyaepuka.

Hivyo basi, ni matatizo yanayohusiana na sababu nyinginezo katika lugha, mbali na pungufu upande wa mtafsiri mwenyewe.

Sura ya tano ndiyo hitimisho ya kazi hii. Katika sura hii, mbali na kuelezea hatua tuliyofikia katika uchunguzi wetu, tumetoa mapendekezo kuhusiana na somo la tafsiri, hasa kwa minajili ya wale ambao watalishughulikia somo hili siku za usoni.

Vile vile tumejumulisha marejeleo yetu katika sura hii kwa kuorodhesha vitabu, majarida, tasnifu na makala tuliyoyarejelea katika kazi hii.

VIFUPISHO VYA MANENO NA TAFSIRI YA ISTILAHU

HP	-	Hadhira Pokezi
K.v.	-	Kama vile
LA.	-	Lugha Asilia
LP.	-	Lugha Pokezi
MA.	-	Makala Asilia
MP.	-	Makala Pokezi
Mw.A.	-	Mwandishi Asilia
n.k.	-	na kadhalika.
Implikecha/Urejeleaji-zida	-	Implicature
Inferensi/Ukisiaji	-	Inference
Inferensi kimantiki	-	Deductive inference
Inferensi Kipragmatiki	-	Pragmatic inference
Kaida za ufaaji	-	Relevance principles
Kaida za ushirikiano	-	Cooperative principles
Maana bwiwa	-	Conceptual meaning
Maana husishi-kimantiki	-	Collocative meaning
Maana kihisia	-	Affective meaning
Maana kimatini	-	Textual/Thematic meaning
Maana kimtindo	-	Stylistic meaning
Maana zalishi	-	Reflected meaning
Maana ziada/kimatilaba	-	Connotative meaning.
Tafsiri kiakademiki	-	Academic translation
Tafsiri kikazi/kihuduma	-	Service translation
Tafsiri kiutambuzi	-	Cognitive translation
Tafsiri ujumbe/habari	-	Information translation

- Tafsiri wazi-kinathari/kitutumbi - Plain-prose translation
- Ufaaji - Relevance
- Ufiche - (Maana isiyo wazi) Implicitness
- Uwazi - (Maana isiyofichika) Explicitness

SURA YA KWANZA

1.0: MWONGOZO WA TASNIFU

1.1: UTANGULIZI.

Taaluma ya tafsiri ilianza karne nyingi sana zilizopita. Mtaalamu Culy (1993:28) anadai; "... tafsiri imekuwa ikifanywa katika viwango mbalimbali kwa maelfu ya miaka ... tokea enzi za mafarao wa Misri; tawala za wafalme wa Babiloni kama vile Hamurabi na hata kufikia sasa ingali ikiendelea kutekelezwa...¹ [Tafsiri yetu]

Miongoni mwa kumbukumbu za awali kabisa katika taaluma ya tafsiri ni Bibilia ya Kiyunani, iliyotafsiriwa kutoka kiyahudi.

Somo hili liliendelea kuimarishwa kama mojawapo ya vitengo muhimu vya sayansi ya lugha. Katika karne ya 19 BK. wataalamu wengi waliishughulikia tafsiri kwa kuihusisha na maswala ya fasihi andishi.

Mtazamo huo ulizua upungufu mkubwa ulioifanya tafsiri kukosa msingi imara wa kinadharia ambao ungehusisha vipengele vyake mbalimbali kama tunavyovifahamu hivi sasa.

Kufikia sasa, ufa mkubwa upo baina ya nadharia za tafsiri na utekelezwaji halisi wa tafsiri, licha ya majaribio machache yaliyofanywa na wataalamu, kuuziba ufa huo. Tatizo ni kwamba nadharia nyingi za tafsiri sio toshelezi, kwa hivyo hazina uwezo wa kutoa miongozo timilifu kwa watafsiri.

Swala la tafsiri kwa ujumla, hivi sasa linatazamwa kwa namna nyingi na wataalamu mbalimbali. Wapo wananadharia wa kisasa kama Hatim na Mason (1990:3-20), ambao wanaiangalia tafsiri kama nyanja ya isimu-jamii ambayo haina budi kutekelezwa bila ya kusahau amali zake za uchanganuzi wa usemi, uchanganuzi wa matini, pragmatiki, semiotiki n.k.

Wengine huihusisha tafsiri na isimu-matumizi, na wengine wakiitazama taaluma hii kama inayooanisha vipengele vya isimu na vile vya isimu-jamii kwa sababu kitendo hasa cha kutafsiri hupata michango kutoka kila upande, yaani ndani na nje ya lugha.

Licha ya tofauti hizo za kimitazamo katika misingi ya tafsiri, pana ukubaliano mkubwa baina ya wataalamu wa tafsiri ya kwamba somo hili lina nafasi muhimu sana katika muktadha wa kijumla unaohusiana na mawasiliano, upashanaji habari/ujumbe na maana baina ya wanadamu wote.

Catford (1965:vii), ameisisitiza umuhimu wa tafsiri katika miaka ya hivi karibuni, kwa maoni kwamba "... ni shughuli yenye umuhimu mkubwa katika ulimwengu wa sasa, nayo ni somo ambalo linawavutia, sio tu wanaisimu bali pia wasomi wa nyanja zinginezo kama vile uhandisi na hesabu"² [Tafsiri yetu].

Tunaafikiana na Catford, katika madai yake. Vile vile tunaonelea ya kwamba, kwa jumla mkondo wa kisasa katika tafsiri umejikita zaidi katika vipengele vya maana na mawasiliano ambavyo vinachukuliwa na wataalamu wengi kuwa vya kimsingi zaidi katika tafsiri borá, jambo ambalo limezua mjadala mkubwa.

Maswala ya maana na mawasiliano, katika somo la tafsiri yanapochunguzwa, lugha asili na lugha pokezi sharti zizingatiwe katika mapana na marefu yao.

Swala kuhusiana na mahala ambapo tunaweza kuliainisha somo la tafsiri, sio muhimu sana kwa vile jambo hilo hutegemea mtazamo na lengo la mtafsiri ama kile anachonua kuwafahamisha wasomaji wake. Lengo la mtafsiri ndilo huathiri mwelekeo wa kinadharia anaouchukua katika kazi anayoishughulikia.

Lililo muhimu ni, uwezo wa mtafsiri wa kupitisha maana kutoka matini asilia hadi matini pokezi, na pia kuweza kuwasiliana na wale watu anaowatafsiria. Tungependa kusesitiza kwamba mambo haya ni muhali sana.

Aghalabu mawasiliano yana uhusiano mkubwa sana na maana, kwa hivyo inatubidi kutilia maanani nyanja zote mbili ndipo tuweze kuupigia msasa wa kutosha, uwanja huu.

1.2: TATIZO LA UTAFITI

Kama ambavyo tumekwishataja katika sehemu ya 1.0, umuhimu na msisitizo unaopewa vipengele vya maana na mawasiliano, umeongezeka maradufu katika somo la tafsiri, hasa katika mielekeo ya isimu-jamii katika miaka ya hivi karibuni.

Msisitizo huu wa kupindukia mipaka, ni zao la jaribio la kuuziba ufa ambao umekuwepo baina ya nadharia za tafsiri na utekelezwaji wa taaluma ya tafsiri.

Usisitizwaji huu wa vipengele hivyo viwili pamoja na dhana zinazohusishwa nazo, kwa bahati mbaya haujauziba ufa huo na wala haujawaepusha watafsiri na matatizo mbalimbali wakati wa kutekeleza shughuli zao kwa jumla.

Tasnifu hii inachunguza na kutathmini matatizo ya aina mbalimbali hasa kutokana na hali hiyo ya kisasa ya wananadharia kuisisitiza zaidi dhana za maana na mawasiliano katika tafsiri. Matatizo tunayochunguza kwa kifupi yanahusiana na vipengele hivyo viwili pamoja na kuelezea dhana mbalimbali ambazo huwakanganya na kuwatatiza wasomi na watafsiri halisi katika taaluma hii ambayo huhitaji makini na uangalifu mwingi.

Matatizo ya tafsiri, kama ambavyo tutaonyesha, hubainika kwa namna tofauti tofauti na katika viwango mbalimbali vya kategoria za lugha kama vile fonolojia, mofolojia, leksia, semantiki, semiotiki, pragmatiki n.k.

Madai ya Culy (1993),³ yanarejelea kiini cha matatizo tunayoyachunguza. Anasema, "miongo ya hivi karibuni imeshuhudia kuibuka kwa miongozo ya kinadharia inayotazamiwa kumwongoza mtafsiri katika kazi yake ... hata hivyo upungufu mkubwa unaozidi kuwepo ni ule wa jinsi/namna ya kutekelezwa kwa kaida zinazopendekezwa na miongozo hiyo ..huu ukosefu wa njia mwafaka umesababisha kutumiwa vibaya kwa miongozo hiyo ya tafsiri" [Tafsiri Yetu].

Tunakubaliana na maoni ya kwamba, sio jambo rahisi, kutafsiri na kuweza kupitisha ujumbe na maana ya matini asili jinsi alivyonulia mwandishi au msemaji wake asilia, hadi katika lugha ya

matini tafsiri au matini pokezi pasipo kukumbana na matatizo kadha wa kadha.

Aidha, lugha pokezi na lugha asili, kila moja huwa na kaida na taratibu maalum za kuwasilisha maana na ujumbe, ambazo zinaweza kutofautiana. Mara nyingi tofauti kama hizo huingiliana na zile ambazo hutokana na kutolingana kwa vipengele vya maana na mawasiliano katika tafsiri.

Hadhira zinazolengwa pia zinaweza kutofautiana baina ya matini asilia na matini pokezi, kama ambavyo tutaeleza katika sura zinazofuata, hasa sura ya nne inayochangana matatizo ya aina hiyo.

Vivyo hivyo nia na mitazamo ya waandishi wa MA na MT, inaweza kutofautiana kulingana na fasiri, tajriba na mazingira yao ya kiuandishi kwa jumla.

Maswala haya yasiyoweza kukwepwa kwa urahisi katika tafsiri, huathiri maana na mawasiliano kwenye matini pokezi. Sisi tutayazingatia kama viini vya matatizo tunayoyachunguza katika diwani ya Risasi Zianzapu Kuchanua (1975), iliyotafsiriwa na ndugu P. Sozigwa.

1.3: MADHUMUNI YA TASNIFU

Tasnifu hii inatazamia kutekeleza madhumuni yafuatayo:

Kupigia mbizi na kuzamia kwa kina, dhana mbalimbali ambazo huzingatiwa katika taaluma ya tafsiri. Dhana hizo hurejelewa na wale wanaojishughulisha na tukio halisi la kutafsiri, baadhi wakiwa hawaelewi kauli na mikiki ya dhana hizo kama wanavyopas

Tunatazamia kuchunguza vilivyo, maswala mbalimbali ambayo huzuka kama matatizo kwa mtafsiri anapojihusisha na vipengele vya maana katika tafsiri ya diwani, Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Vilevile tunachanganua maswala yanayofungamana moja kwa moja na dhana ya mawasiliano katika diwani, Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), huku tukiyaainisha kwa njia ambayo inatuwezesha kutathmini kazi yenyewe na kuelezea kiini cha matatizo yanayodhihirika katika tafsiri hii.

Maswala ya kuzingatia hapa ni kama vile; mambo yapi huhitajika ili ujumbe usemekane kwamba umepitishwa na kupokelewa jinsi ilivyonuiwa na mwandishi wa MA? Ni kwa kuzingatia au kutozingatia hoja zipi za kimuktadha ndipo tunaweza kudai kwamba ujumbe/maana fulani umepitishwa vilivyo katika tafsiri? Iwapo tutadai ya kuwa ujumbe haujawasilishwa vyema, ni mambo yanahusika katika upungufu huo?

Maswala haya yanakuwa kama vigezo vya kukadiria ubora wa upungufu wa kazi yoyote ile ya mashairi katika uwanja wa faalio tafsiri.

Tasnifu hii pia, inadhamiria kuangazia upya mada yetu ambayo inajumuisha dhana na matatizo katika tafsiri, huku tukijika katika mitazamo mipya na ya kisasa zaidi, ambayo haijapata vipengele vya kimuktadha na uziada lugha unaotokana na sifa kijamii; tofauti na mitazamo ya awali ambayo haikuyapa uzito wa maswala hayo.

Mitazamo hii mipya tunayoirejelea inaoanisha michango kutoka na nyanja zinazofungamana na dhana za maana na mawasiliano

vile nyanja ya pragmatiki, semiotiki, mtazamo wa kiufafanuzi, ule wa kiutambuzi, mtazamo wa ufaaji, ufiche na ufichuzi n.k. Aghalabu yote haya yatajumuishwa katika nadharia mojawapo tunayoitumia ya uchanganuzi wa usemi.

Hatimaye tunalenga kuibuka na mapendekezo yatakayojumulisha kaida za nadharia za tafsiri maana, mawasiliano na uchanganuzi usemi. Mapendekezo hayo yatawasaidia wachunguzi wengine wa somo hili, lakini hasa zaidi, watakaoshughulikia mashairi yaliyotafsiriwa. Tunatumaini kwamba mchango wetu utakuwa toshelevu katika nyanja ya usomi kwa jumla.

1.4: UPEO WA TASNIFU

Tasnifu yetu inafafanua dhana mbalimbali zinazohusika katika taaluma ya tafsiri kama vile dhana ya tafsiri, dhana ya maana, dhana ya mawasiliano na dhana ya muktadha, huku tukisisitiza maswala yaliyo muhimu katika kila mojawapo ya dhana hizo kwa somo la tafsiri.

Pamoja na hayo, tasnifu yetu inazingatia matatizo ya tafsiri katika viwango mbalimbali, hasa yakiwa yamefungamana na vipengele vya maana na mawasiliano baina ya MA na MT.

Tutarejelea diwani ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) ambayo itakuwa kiini cha data tutakayoichambua katika tasnifu hii, pia tutarejelea When Bullets Begin To Flower (1972), ili kuilinganisha na tafsiri yake.

Tutapitia mashairi yote, katika diwani hizo, huku tukichagua mambo yanayochangia katika ufafanuzi wa vipengele tunavyovichunguza, na pia kwa kutegemea iwapo yanaakisi maswala tunayotaka kuyachanganua au kama yanalingana na matatizo tunayolenga kuelezea.

Vilevile tutasoma vitabu vingine vya wataalamu wa somo la tafsiri, ili tupate msingi imara wa kuzamia katika dhana tunazozifafanua na nadharia tunazozitumia katika tasnifu hii. Hatua hii itatusaidia kuangazia zaidi kiini cha mada ya tasnifu yetu.

Tasnifu hii itajikita katika vipengele tutakavyoviteua vya nadharia jumuishi tunazozitumia kwa namna ya kuoanisha; kwa minajili ya tasnifu hii. Hizo nadharia ni pamoja na ile ya maana, ya mawasiliano na ya uchanganuzi wa usemi.

1.5: SABABU ZA KUCHAGUA SOMO

Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), ambayo ni tafsiri ya When Bullets Begin To Flower (1972), ni diwani yenye mashairi kutoka mataifa mbalimbali, yakiwemo Angola, Msumbiji, Cape Verde, Sao Tome, Guin'ee n.k., ambayo yalitawaliwa na serikali ya Ureno katika kipindi cha ukoloni.

Diwani ya Kiwahili, ni tafsiri ya tafsiri, kwa vile mashairi hayo, mwanzoni yaliandikwa kwa kireno kisha yakatafsiriwa katika kiingereza na lugha zingine za Ulaya na baadaye yakatafsiriwa katika lugha za kiafrika, ikiwemo kiswahili pia.

Katika utangulizi wa tafsiri ya **Kiingereza**, mtafsiri anadai kwamba shida kubwa aliyokabiliana nayo ni ile ya kuwa, lugha ya **Kireno** haitafsiriki kwa urahisi hadi katika **Kiingereza**, kinyume na ambavyo inatafsirika katika lugha zingine za ulaya zenye nasaba ya 'Romance' kama **Kilatini**, **Kifaransa** na **Kiitaliano**; sababu shaka) ikiwa kwamba lugha hizi zote ni za nasaba hiyo moja, nayo **kiingereza** ikiwa katika nasaba ya 'Germanic'.

Shida aliyokumbana nayo mtafsiri wa matini ya **Kingereza**, ndiyo iliyotuchochea kutaka kuchunguza zaidi matatizo yaliyo katika diwani iliyotafsiriwa kutokana na hiyo ya **Kiingereza**, ambayo ni hii ya **Kiswahili**, Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Tunaamini ya kuwa mashairi hayo yaliyotafsiriwa katika **Kiswahili** yana hoja muhimu ambazo zinaweza vilevile kuchunguzwa kama matatizo katika taaluma hii ya tafsiri.

Tasnifu yetu itakuwa kielelezo cha maswala hayo, ambayo hayajachunguzwa bado, na ambayo kwa sasa yangali yakiwatatiza baadhi ya watu wanaosoma mashairi hayo kwa matumaini ya kuyaelewa vyema, kimaana na kimawasiliano. Vilevile somo hili, tunalotafiti, ni mchango mwafaka na wenye kuhitajika katika uwanja wa tafsiri za **Kiswahili**, hasa nyanja ya ushairi.

Anavyosema Zaja (1986)⁴ ni kuwa, "tafsiri imekuwa ikiendelea katika nyanja mbalimbali za lugha na katika fasihi ... tanzu za riwaya na tamthilia zimepokea tafsiri nyingi ..." Kauli anayoitoa Zaja ni ya kweli, hasa tukizingatia tafsiri za kazi za fasihi kutoka lugha ya **Kiingereza** hadi **Kiswahili**. Inadhihirika wazi kwamba diwani chache sana zimetafsiriwa, kuliko riwaya na tamthilia

zilizotafsiriwa. Vivyo hivyo, uchambuzi wa matatizo katika mashairi hayo yaliyotafsiriwa, umefanywa kwa uchache sana, ukilinganishwa na ule ambao nyanja za riwaya na tamthilia zimefanyiwa.

Sababu hiyo imetufanya kuzingatia somo hili, ili kuibuka na mchango mwafaka katika uwekaji misingi ya tafsiri bora na uhimizaji wa maswala ya kutiliwa maanani wakati wa kutafsiri mashairi kutoka lugha yoyote ngeni hadi katika Kiswahili.

Somo hili pia tumelichagua kwa vile tungetaka kupiga hatua zaidi ya ile hali ambayo imekuwepo ya wataalamu kujikita tu katika nadharia za kimaana na kimawasihano pekee, wanaposhughulikia tafsiri.

Pamoja na hayo, tunatarajia kwamba uchambuzi wa mashairi utatoa fursa kwetu ya kutekeleza uchambuzi unaozingatia nadharia ya uchanganuzi usemi, hasa tukirejelea vipengele vyake vya pragmatiki, urejeshi, uashiriaji, semiotiki, muktadha n.k.

Nadharia hii tunayoijumuisha na zile zingine, haijatumiwa na wataalamu wengi wanaochunguza matatizo na dhana zinazohusishwa na taaluma ya tafsiri. Hii hatua yetu tunaamini, itapanua mitazamo ya watafiti wanaoshughulikia tafsiri kama taaluma ya kiusomi. Uchunguzi tulioufanya kufikia sasa unaonyesha ya kuwa diwani tunayoizingatia haijapigiwa darubini vya kutosha, hasa katika kuchanganua matatizo ya tafsiri.

Aidha dhana tunazofafanua katika tasnifu hii, kuhusiana na taaluma ya tafsiri kwa jumla, haziangaziwa vya kutosha katika kazi za kitaaluma katika lugha ya Kiswahili. Tumechukua fursa hii

kuanzisha shughuli hiyo, tukitarajia wengine wataweza kuiendeleza zaidi ili taaluma ya tafsiri iweze kusomwa na kujitosheleza katika lugha ya kiswahili, bila hasa ya kuhitaji kutafsiri dhana hizo kila mara somo la tafsiri linaporejelewa.

Mwisho ni kwamba, somo hili la tafsiri katika miongo ya hivi karibuni limeimarika katika umuhimu wake, nasi tumeonelea ni jambo la manufaa kuchagua somo la utafiti, katika uwanja huu, ili tuweze kuuendeleza hata zaidi ya pale ulipofikia.

1.6: HAIPOTHESIA

1. Diwani ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) inapolinganishwa na matini yake ya asili; When Bullets Begin To Flower (1972), kama ambavyo tunachukulia katika tasnifu hii, tofauti nyingi sana zinaonekana baina yao, katika viwango mbalimbali.

Tofauti hizi zinaweza kufafanuliwa tunapozingatia sababu, ndani na nje ya lugha za Kiingereza na Kiswahili, kama tofauti za mifumo ya sintaksia, mofolojia na hali kadhalika, tofauti za kimazingira, kijamii na za miktadha ya maeneo ambamo kazi hizo ziliandikwa na jinsi ambavyo hadhira lengwa hupokea na kufasiri maana inayowasilishwa.

2. Msingi imara wa kinadharia unapokosekana katika tafsiri, mtekelezaji wa shughuli hiyo hufanya makosa mengi wakati wa kutafsiri.

Baadhi yao hawajapambanukiwa na nadharia hizo, kwa hivyo wanakabiliwa na matatizo mengi, kama yale tunayozingatia katika diwani ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), (tazama sura za tatu na nne za tasnifu hii.)

3. Kufaulu au kutofaulu kwa mtafsiri wa diwani ya Risasi zianzapo Kuchanua (1975), katika kuwasilisha ujumbe na maana kwa HP, kunaweza kutathminiwa kupitia uchanganuzi wa vipengele mbalimbali vya mashairi yaliyokusanywa humo, hasa vile ambavyo vinaathiri maana na mawasiliano ya ujumbe asilia.
4. Dhana zinazohusiana na somo la tafsiri, hazina budi kueleweka vyema kwa kila mmoja anayejihusisha na tafsiri, ndipo aweze kujiepusha na baadhi ya matatizo, mbali na kule kuyatambua.
5. Kazi ya tafsiri inapoongezea mambo ya ziada au kupunguza baadhi ya mambo kwa zaidi ya kiasi kilichopimika; jambo hilo husababisha kutowasilishwa kwa ujumbe kwa namna halisi aliyonuia mwandishi asilia kwa wasomaji wake. Vile vile utata, huzuka, kugubika kwa maana na ufasiri mbaya wa ujumbe na maana miongoni mwa HP, kwa sababu ya kuongeza na kupunguza baadhi ya mambo wakati wa kutafsiri.

1.7: YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Uchunguzi wetu umeonyesha ya kuwa kazi nyingi kuhusiana na taaluma ya tafsiri zinahusika na tathmini ya matatizo au dosari ambazo huwa katika kazi teule; vile vile nyingi ya kazi hizo zinahusu aina na namna mbalimbali za kutafsiri.

Ni kazi chache sana zinazohusu nadharia za tafsiri na dhana zinazohusishwa na somo hili kwa jumla.

Hali ilivyo sasa ni kwamba nyanja ya ushairi katika lugha ya kiswahili haina tafsiri nyingi za diwani za miaka ya hivi karibuni. Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) na Wimbo wa Lawino ni miongoni mwa diwani chache zilizoko.

Kinyume na hivyo, diwani nyingi mno, hasa tenzi, za awali katika kiswahili, tokea maaajilio ya waarabu huku Afrika ya Mashariki, zimetafsiriwa hadi katika kiswahili sanifu.

Tasnifu kadhaa zimewahi kuandikwa kuhusiana na taaluma ya tafsiri, nazo vilevile zimejikita zaidi katika uchunguzi wa matatizo kwenye matini za kifasihi, hasa katika nyanja za riwaya na tamthilia.

Mchango wa wataalamu wa somo hili, kutoka mataifa ya nje ni mkubwa na maridhawa, hasa katika viwango vya kinadharia.

Tumewarejelea baadhi yao na kuonyesha maoni yao. Post gate (1922), Catford (1965), Brower (1966), Kelly (1979), Larson (1984), Herman (1985), Kirk (1986), Hatim na Mason (1990); wote wamesisitiza umuhimu wa kipengele cha mawasiliano kama dhana inayopasa kuzingatiwa katika tafsiri.

Mchango wao umeiwekea nadharia ya mawasiliano msingi imara ambao umetufaidi pia katika tasnifu hii.

Zaidi ya huko kuisisitiza mawasiliano Brower (1966) amezungumzia nafasi muhimu ya mtafsiri, hasa yale madhumuni yake yanayomwongoza anapoitekeleza kazi hiyo. Maoni ya Brower ni kielelezo kizuri kuhusiana na dhana za mawasiliano na jinsi ya kutekeleza tafsiri nzuri.

Nida (1964, 66, 69) ana mawazo yenye manufaa sana kuhusu matatizo ambayo watafsiri wa Biblia hukabiliana nayo na jinsi yanavyoweza kutatuliwa.

Amezingatia kwa kina kirefu sana, umuhimu wa vipengele, vya sarufi, msamiati na muundo wa lugha, vinavyohusika katika tafsiri.

Matatizo aliyoyajadili yaligusia maswala kama vile ya kisaikolojia na ya kitamaduni katika jamii. Mawazo na mapendekezo hayo ya Nida, yametuweka katika upeo wa kuangazia zaidi matatizo na dhana tunazozichunguza katika somo letu.

Beekman na Callow (1974) walipanua mtazamo wa dhana ya mawasiliano, kuzidi watangulizi, wao walivyofanya. Walizingatia maswala ya; utamaduni, matumizi ya lugha kitamathali, muundo wa lugha na muktadha wa matumizi ya lugha.

Vilevile wamejadili vyema aina mbalimbali za tafsiri. Huu mtazamo wao mpana umetusaidia katika kuzihusisha dhana hizo walizozirejelea, na somo la tafsiri kwa jumla.

Steiner (1975) alishughulikia ukusanyaji wa mikhtasari ya baadhi ya kazi za tafsiri zenye upevu wa juu sana na pia mikhtasari ya nadharia za tafsiri kama ambavyo zilitumika Ulaya magharibi

tangu miaka mingi iliyopita.

Alijikita katika taaluma za; historia ya kijamii, uhakiki wa kifasihi na ule wa kishairi (poetics). Steiner alichunguza mawasiliano ya walimwengu katika tafsiri.

Huo uchunguzi wake unafungamana na baadhi ya maswala tutakayochunguza katika dhana za mawasiliano na muktadha, sura ya 2, sehemu za 2.2 na 2.3.

Newmark (1982, 88) alipanua zaidi mitazamo ya wataalamu wa miaka ya hivi karibuni, kwa kugusia mambo mengi zaidi kuhusu tafsiri; kuanzia nadharia na kanuni za tafsiri, matatizo ambayo watafsiri hukumbana nayo, na hata kufikia kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuyatatua matatizo hayo.

Kwa njia ya kudurusu na kutathmini upya maoni ya wataalamu waliomtangulia, ameweza kujadili kwa kirefu na kwa mtazamo wa kisasa, umuhimu wa kuwepo na misingi imara ya nadharia, kanuni na taratibu zinazomwongoza mtafsiri anapotekeleza kazi yake.

Vilevile ameorodhesha aina za tafsiri ambazo hutumika kulingana na hali mbalimbali za matini, sajili na miktadha tofauti tofauti.

Kazi zake zinatoa mchango mkubwa kuhusiana na nadharia za tafsiri na dhana zinazohusika.

Lafevere (1975) ni miongoni mwa wananadharia wachache walioshughulikia tafsiri za ushairi, hasa matatizo ambayo huzuka. Pia amejadili kanuni mbalimbali zinazosisitizwa na watafsiri wa mashairi na wakati huohuo akaorodhesha manufaa na dosari za kila moja ya kanuni hizo.

Anasema kipengele cha mawasiliano ni muhimu na zaidi ya hayo amependekeza taratibu za kufuatwa wakati wa kutafsiri kazi za fasihi, huku akionyesha nafasi ya tafsiri katika nyanja ya fasihi, yaani jinsi ambavyo tafsiri inaathiri, ukuzaji, usomaji na uchambuzi wa matini za kifasihi.

Hatim na Mason (1990) ambao ni wananadharia wenye mawazo yanayohusisha maswala mengi ndani na nje ya lugha, wamechukua mwegemeo wa uchanganuzi wa usemi na kuhusisha vipengele vyake na tafsiri.

Licha ya kutaja manufaa ya mwegemeo huu mpya kwa somo la tafsiri, wanaonyesha pia pungufu zake ambazo zinahitaji uchunguzi zaidi katika tafsiri.

Madai yao yanaelekea kupendekeza kwamba nadharia ya uchanganuzi usemi ni mwafaka zaidi katika uchambuzi wa kazi za tafsiri kwa sababu inayo vipengele vingi zaidi vinavyoingiliana moja kwa moja na dhana za maana, muktadha, mazingira, tamaduni, mawasiliano n.k. Hivyo vipengele humsaidia yeyote anayetafsiri, kutekeleza jukumu hilo kwa namna iliyo pevu, bila ya makosa mengi.

Madai yao pamoja na mapendekezo waliyoyatoa, yamesaidia sana katika uzingativu wetu, wa dhana na matatizo ya tafsiri.

Kuhusiana na somo hili vilevile, yapo majarida na tasnifu zilizoandikwa kwa kiswahili au kiingereza.

Mengi ya majarida kama ya akina Mohamed (1965) Weston (1965), Harries (1970) Mazrui na Kazungu (1981), Mazrui A. (1973), Mbaabu (1985) na Mutahi (1987), yamehusika zaidi na matatizo ambayo hutokea wakati wa kutafsiri.

Tasnifu zilizoandikiwa somo hili ni kama zifuatazo: Mzee (1980), aliyejadili matumizi ya sajili mbalimbali za lugha katika kiswahili na makosa ambayo huandamana na kila mojawapo ya hayo matumizi.

Ali (1981), alijadili makosa mbalimbali ambayo hutokea katika taarifa za habari za idhaa ya sauti ya Kenya, zilizotafsiriwa, akizingatia jinsi ambavyo mawasiliano mazuri hupotoshwa na makosa kama hayo.

Mchango wake ni muhimu, hasa tunapozingatia matatizo ya tafsiri katika Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Zaja (1986), alijadili sababu zinazosababisha udhaifu ambao huonekana katika kazi za fasihi tafsiri na pia umuhimu wa nadharia katika utatuzi wa makosa ya tafsiri. Hayo yote ni muhimu kwa somo tunalolitafitia.

Shitemi (1990) kwa upande mwingine, alijadili jinsi mtafsiri wa matini hufanya uteuzi katika yale ambayo anayaandika, hasa kwa minajili ya kuwasiliana vyema zaidi na hadhira yake.

Shitemi anaonelea kwamba tofauti baina ya matini ya lugha asilia na yale ya lugha pokezi, hutokana na sababu za uteuzi wala sio kimakosa, jinsi ambavyo wahakiki wengi wa tafsiri huchukulia.

Mada'i ya Shitemi yana mchango muhimu kwa dhana ya mawasiliano ambayo tunatazama vipengele vyake.

Mwangi (1996), alichunguza matatizo ya leksikografia-tafsiri katika kamusi za uwili lugha, hasa akiifanyia tathmini, kamusi ya Johnson (1939) ya kiingereza-kiswahili kama mojawapo ya kazi zilizotafsiriwa.

Vilevile alizingatia dhana ya tafsiri kwa kifupi, dhana ya leksikografia-matini na nafasi ya maana katika tafsiri, kama kipengele chenye umuhimu mkubwa.

Aliyatazama makosa ya tafsiri katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile sarufi, semantiki n.k. Maoni ya Mwangi vivyohivyo yametusaikia, kuangazia zaidi dhana ya maana na matatizo ya tafsiri ambayo tunayashughulikia.

1.8. MISINGI YA KINADHARIA

Tunatumia mwongozo wa tafsiri unaojumulisha mitazamo mitatu ya nadharia kwa pamoja au nadharia jumuishi.

Nadharia hizo ni pamoja na ile ya;

- (i) Uchanganuzi wa usemi,
- (ii) ya maana, na
- (iii) ya mawasiliano.

Kwa kujumulisha nadharia hizi zote, tunaamini kauli/kanuni muhimu za kila mojawapo ya nadharia hizo, itakuwa mwafaka katika kutujengea misingi imara ya kuchanganulia na kushughulikia vyema maswala yanayozingatiwa kuhusiana na dhana na matatizo ya tafsiri, ambayo ni kiini cha utafiti wetu.

Licha ya kuwa na miongozo ya tafsiri ambayo huafikiana kijumla, kungali na tofauti kadhaa baina yazo. Jambo hili limewafanya watafsiri wengi wa kisasa kutekeleza tafsiri zilizoegemezwa zaidi katika maana na mawasiliano kuliko vile ambavyo zimeegemezwa^{kwa} umbo na muundo wa kazi zenyewe.

Ni hatua ya kutia moyo kwamba baadhi ya wataalamu wa kisasa vile vile wameendelea kuisisitiza kipengele kinachohusu maswala ya kitamaduni, ambacho huchunguzwa aghalabu, chini ya miktadha ya jamii zinazotumia lugha zinazohusika. Hatua hii inalingana na ukweli kwamba tafsiri, kama asemavyo Catford, (1965) ...ni kitendo cha kubadilishwa kwa vipengele vya kimatini vya lugha moja na vipengele kama hivyo katika lugha nyingine tofauti ... [Tafsiri yetu]⁵.

Miongoni mwa walioiongezea msisitizo kipengele cha muktadha ni Shaw (1988), Wendland na Ernst (1987) ambao waliwahimiza watafsiri, kutopuuza kaida za kitamaduni katika yale waliyoya wasilisha, kwa vile hatua hii husaidia katika uelewekaji zaidi wa maana ya ujumbe kwenye matini.

Umuhimu wa maswala hayo ya kimuktadha katika mawasiliano na maana inayopitishwa, humlazimu mtafsiri kuhusisha kauli za somo la anthropolojia na zile ambazo huhusiana na kuelewa vizuri muktadha wa makala. Akifanya hivyo ndipo anaweza kujitokeza na matini tafsiri inayofaa kwa hadhira lengwa.

Kuhusishwa kwa anthropolojia ni sawa na kusema kwamba utamaduni wa jamii urejelewe katika shughuli za tafsiri. Kraft (1979) Beekman na Callow (1974), na Nida na Taber (1982), pia wana maoni sawa na hayo.

Hali hii ya kisasa inayorejelea mitazamo mingi katika tafsiri ndiyo inayotufanya kujumuisha nadharia ambazo zitatupatia fursa ya kutazama mambo hayo yote.

}

Uchanganuzi wa usemi. ni nadharia ambayo tumeitumia kuchunguzia vipengele vingi vilivyo katika matini; huku tukifafanua kadri iwezekanavyo, vipengele ambavyo huhusiana na mazingira halisi yanayofungama na jamii zinazohusishwa na matini asili kwa upande mmoja na kwa upande mwingine, jamii ya MP. Nadharia hii hugusia maswala kama desturi na kaida za jamii, ishara zinazotumika kuwakilishia yale ambayo yanamaanishwa katika usemi au maandishi na jinsi ambavyo viashiria vya kisemantiki hufasiriwa na wanajamii. Saikolijia ya kijamii vilevile huingiliana na mambo hayo yote kwa vile athari zake huonekana katika namna ambavyo jamii fulani huweza kufasiri maana katika mambo yote inayokumbana nayo maishani, katika mazingira yao, pia katika muktadha na utamaduni unaowazunguka wakati wa maongezi au maandishi ya usemi wao.

Yule na Brown (1987), wanaonyesha jinsi ambavyo uchanganuzi wa usemi unahusiana na sintaksia na semantiki. Vilevile uhusiano wa nadharia hii na pragmatiki, ambacho ni kitengo cha somo la lugha linalozingatia maswala ya kimuktadha.

Kwa jumla, nadharia hii huzingatia na kuhusisha maswala yote yanayoingiliana na dhana ya mawasiliano. Maswala hayo ni kama; ujumbe ulio kwenye usemi, hali ya msemaji au mwandishi wa ujumbe huo, hali ya mpokeaji au msomaji wa ujumbe, na hali zinazowazunguka za kitamaduni.

Aghalabu msisitizo wa nadharia hii ni katika dhana za uwasilishaji ujumbe muktadha na maana inayolengwa na mwandishi asilia. Hii ina maana kwamba nadharia hii imepiga hatua zaidi katika uchambuzi wa lugha kwa kuhusisha vipengele zaidi ya vile vya

kiisimu au vya kisintasia pekee ambavyo huegemea tu sarufi na muundo; kinyume na hivyo, nadharia hii hutubainishia maswala mengine ya ziada katika jamii zinazohusika, kama upekee wa lugha ya MA na ya MT, saikolojia ya wanalugha wakati wa kubuni na kupitisha ujumbe na maana lengwa. Utegemevu wetu kwa nadharia hii, unatoa nafasi nzuri, ya kuchanganua dhana za tafsiri na matatizo katika diwani ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Maoni ya Hatim na Mason (1990) yanatetea kauli kama hiyo. Wanadai kwamba, "tukio la tafsiri linahusu, kuelewa ulimwengu wa lugha asili ya mwandishi au mnenaji, katika misingi ya kitamaduni na kwa namna ambavyo jamii yake huzua maana katika lugha hiyo; pili ni kuelewa maana zinazoweza kuwakilishwa na ishara za lugha, kisemiotiki na kuelewa mfumo wote wa lugha hiyo kwa namna ambavyo sura za neno au kifungu cha maneno zinaweza kudhihirika; tatu ni, kuelewa ujumbe unaobebwa katika maneno yanayowasilishwa na la nne ni, kufanya uchunguzi unaopigia msasa sababu na nia ya mwandishi asilia au mnenaji ujumbe. Wakati huo huo nia na sababu za mwandishi asilia zilinganishwe na zile za mtafsiri mwenyewe; athari za kisaikolojia baina ya makundi hayo ya kijamii pia zizingatiwe ..."

[Tafsiri Yetu]⁶.

Tafsiri inapotazamwa kupitia kwa nadharia hii ya uchanganuzi usemi, pana uwezekano wa kuchanganua uhusiano tata uliopo baina ya wanadamu na dhana zinazochangia ujenzi wa miktadha ambayo kwayo wanawasiliana na kufasiri maana. Hivyo basi tafsiri sharti itazamwe, sio tu kama shughuli katika utasa wa lugha, bali kama tukio la kimawasiliano ambalo hutekelezwa katika muktadha fulani wa

kijamii.

Tungependa kuisisitiza kwamba upana na utoshelevu wa nadharia hii utatuelekeza katika umakinifu wa kuchambua maswala mengi sana, katika somo hili. Maswala hayo hadi sasa yangali yanawakwepa na kuwakinza wale ambao huhakiki na kusoma tafsiri.

Ni jambo lililo wazi kwamba, "kunavyo vipengele nje ya lugha, ambavyo huhusishwa katika nadharia ya semantiki ...vipengele hivyo hutegemea mitazamo ya sayansi kadha wa kadha; hivi vipengele ni sehemu ya matukio yanayohusika katika ubebaji maana, zilizo ndani ya vipengele-leksia katika usemi wa lugha..."⁷ chambilecho Guenther, F. na Guenther, R. (1978) ambao madai yao yanaonyesha ulingano mkubwa sana na ule wa akina Hatim na Mason (1990).

Wao wanaongezea kwamba "Uhusiano kati ya maana na usemi/tamko la lugha sio tu wa kisemantiki bali huhusisha nadharia zinazohusika na maswala ya kilimwengu na maumbile, kama muktadha au mazingira ya lugha; uhusiano baina ya watumizi wa lugha na mazingira yao na pia uhusiano baina yao wenyewe kama wanadamu..." [Tafsiri Yetu].

Nadharia ya maana, katika tafsiri husisitiza ya kwamba maana iliyo katika MA iweze kuhamishwa vivyo hivyo, bila kubadilishwa, hadi katika mfumo wa lugha ya MP. Hili ndilo jambo la muhimu zaidi katika nadharia hii.

Larson (1984) na wananadharia wengine wanaochukua mwegemeo wa kiisimu wanasema kwamba "...tafsiri hunusu uhamishaji wa maana ya vipengele vya lugha asili hadi kwa lugha pokezi ...maana ndiyo yenye kuhamishwa, nayo haipaswi kubadilishwa kamwe" [Tafsiri Yetu]s.

Maoni yao yanadhihirisha umuhimu wa kipengele cha maana katika tafsiri, sawa na ambavyo nadharia ya maana hufanya.

Kwa miaka mingi, wanafalsafa na wanalugha wameendelea kuainisha aina za maana. Mnamo 1892 B.K. Frege alijaribu kutofautisha maana rejeshi na maana fahiwa.

Kutokana na msingi huo, hivi sasa wataalamu wameweza kuainisha maana katika kategoria mbili za kimsingi ambazo ni pana na hujumulisha mambo mengi, hizo kategoria mbili ni; maana tambuzi na maana kimatilaba au ziada. Tutazielezea vyema zaidi katika sehemu ya 2.4

Kwa muda mrefu, vilevile wataalamu, wakiwemo Beekman na Callow (1974) wamekuwa wakikitazama kipengele cha maana kama ujumbe unaowasilishwa katika mfumo wowote ule wa lugha. Watafsiri wengi wanaafikiana katika kauli kwamba shughuli yao haswa ni kuwasilisha maana kwa wapokeaji matini. Tunakubaliana kwa jumla na maoni hayo ingawa tungependa kusiondha ya kwamba yapo mambo mengine vilevile ambayo ni ya muhimu sana katika tafsiri.

Kwa hivyo, tafsiri inayojikita katika nadharia ya maana, bila shaka, huazimia kupitisha maana kamili na sahihi. Maana zenyewe huwa katika kila mojawapo ya leksia zinazohusika, au katika kila kifungu cha maneno kama vile sentensi. Maana katika kifungu hutokana na leksia zote kwa pamoja.

Nadharia hii inasisitiza kwamba maana ambayo huhamishwa iweze kuchukua mfumo wa lugha pokezi, kwa hivyo mfumo wa lugha asili haufai kuhamishwa hadi kwenye lugha pokezi. Dostert na wanasemantiki wengine wanayasisitiza hayo na pia kutahadharisha ya

kuwa jambo hilo likipuuzwa maana inaweza kuvurugika. Wanaongezea ya kuwa tafsiri ni tawi la isimu tendi linaloshughulika haswa na tatizo la uhamisho wa maana kutoka seti moja ya ishara zilizopangiliwa kwa namna maalum, hadi kwenye seti nyingine iliyopangiliwa.


Tunaonelea kwamba tofauti baina ya seti kama hizo, ndiyo husababisha lugha mbili au zaidi kuwa na mifumo inayotofautiana kimaumbo.

Mtazamo wa Dostert unapofasiriwa katika tukio lolote lile la tafsiri, huonyesha ya kuwa lugha fulani (A) huweza kuvusha vipengele vyake vya maana hadi katika mfumo wa lugha (B) baada ya vipengele hivyo kuchujwa katika mfumo bia wa fikra unaohusishwa na lugha zote za ulimwengu.

Huo mfumo bia ni kama kiungo cha kati mwa lugha hizo. Mfumo bia, hubadilisha na kusahihisha mfumo wa lugha (A) ili ufae katika mfumo wa lugha (B).

Maoni kama hayo ya Dostert yamewahi kutolewa na Beekman, Callow na Kopesec (1981), walipozungumzia nadharia ya uchanganuzi wa muundo kisemantiki, yaani (theory of semantic structure analysis).⁹

Kimchoro, maoni hayo yanaweza kuwakilishwa kama ifuatavyo:




Mtafsiri anayezingatia nadharia hii, hana budi kuzielewa vyema lugha zote mbili anazozishughulikia. Huko kuzielewa vyema ndiko humwezesha kuhifadhi upekee wa lugha asilia kila anapopitisha maana kikamilifu, kulingana na masharti ya mfumo bia, hadi katika mfumo wa lugha pokezi. Wakati huo huo akihakikisha ya kwamba upekee wa lugha pokezi vilevile umehifadhiwa. Hatua hii humkinga na hatari ya kuegemea upande mmoja pekee, wakati wa kutafsiri.

Newmark (1982, 1988) na Catford (1984) pia wanahimiza kwamba tafsiri maana ndiyo yenye kufaa zaidi, katika tukio la tafsiri.

Ogden na Richards (1972) wamechangia sana nadharia ya maana, kwa maoni yao kwamba vipengele vya kiisimu vinaweza kuelezewa kimaadna katika misingi ya uhusiano wenye pembe tatu, uliopo baina ya: dhana ya, kinachorejelewa; ishara zinazowakilisha dhana yenyewe na picha inayozuka; kutokana na ishara za dhana inayojengeka akilini mwa msemaji na msikilizaji.

Kimchoro, utatu wa dhana za nadharia ya maana zinaweza kuonyeshwa kama ifuatavyo:¹⁰"



Vipengele vyote katika mchoro huu vinahusishwa katika tukio la kupatikana kwa maana.

Nadharia ya mawasiliano. katika tafsiri huchukua mtazamo ambao huona kiini cha tafsiri kuwa tukio la kuwasiliana, huku ikisisitiza vipengele vifuatavyo katika hayo mawasiliano.

- (i) chanzo cha ujumbe (msemaji/mwandishi).
- (ii) mpokeaji ujumbe (msikilizaji/msomaji).
- (iii) lengo na hisia za mwandishi/msemaji kama ijitokezavyo katika kazi yake.

Kwa kawaida nadharia hii hujaribu sana kuwasilisha maoni, mawazo, falsafa, itikadi na hata msimamo wa mwandishi wa MA kwenye MP.

Katika mapana yake, mawasiliano yanaweza kuelezwa kama tukio la kubadilishana jumbe kupitia kwa lugha za wanadamu, aidha kimaandishi au kimaongezi.


Kulingana na Shannon na Weaver (1949) waliofafanua nadharia ya mawasiliano, "...jumbe hupitishwa kutoka kwa chanzo chake (msemaji/mwandishi) hadi kwa mpokeaji, kama ishara za sauti au maandishi kwa kutegemea njia inayochaguliwa kupitishia ujumbe huo

unaowasilishwa...¹¹

Yanayowasilishwa huwa yamebuniwa na mwenye kuyawasilisha, nayo yanaweza kuwa mambo ya kweli au yasiyo ya kweli. Vivyo hivyo yanaweza kuonyesha hisia fulani, hali kadhalika yanaweza kufungamana na maswala ya kijamii au ya kitamaduni. Wanaongezea ya kwamba, huwa vigumu sana kwa watu kutoweza kuwasilisha chochote hata wakati ambapo wamenyamaza kimya.

Vipengele wanavyovitaja Shannon na Weaver (1949) kuhusiana na nadharia ya mawasiliano yanaweza kupambanuliwa zaidi kupitia kwa mchoro ufuatao:

Wanasema hivi ndivyo vipengele vya kimsingi katika mawasiliano. Hartmann na Stork (1972) vilevile wanaelezea mchoro huu kuwa ni mfano wa kanuni zinazohusika katika nadharia ya mawasiliano.



Tafsiri ya istilahi katika mchoro ni kama ifuatavyo:

1. Mwenye kupeleka/kutuma ujumbe - Sender

- | | | | |
|----|--|---|---------------------|
| 2. | Mwenye kupokea ujumbe | - | Receiver |
| 3. | Njia ya kupitishia ujumbe | - | Channel |
| 4. | - | | |
| 5. | Msimbo (ishara zinazobeba maana maalum | - | Code |
| 6. | Mada (yanayozungumziwa) | - | Topic |
| 7. | Muktadha | - | Context |
| | Mazingira 1 na 2 | - | Environment 1 and 2 |
- Tutaelezea zaidi mambo hayo yote katika sehemu ya 2.2 inayohusu dhana ya mawasiliano.

Vifupisho : kut. ^-kutuma (encoding), kup.^-kupokea (decoding).

1.9: NJIA ZA UTAFITI

Tumetumia njia zifuatazo katika utafiti wetu:

1. Kusoma na kudurusu kwa kina, kwenye maktaba, vitabu, makala, majarida na tahakiki mbalimbali kuhusiana na somo letu la utafiti, pamoja na yale yanayohusu nadharia tunazozitumia na kuelezea dhana mbalimbali tunazozitazama.
2. Tumeshauriana na wataalamu wa tafsiri kama vile wahadhiri na watafiti ili kupata mwanga zaidi kuhusiana na dhana, matatizo na maswala mengine yanayowakanganya wengi katika taaluma ya tafsiri.
3. Tumesoma matini yetu ya asili When Bullets Begin To Flower (1972) pamoja na tafsiri yake, Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), kwa njia ya kuchambua na kulinganisha ndipo tukaweza kujitokeza na data ya kimsingi kuhusiana na mada yetu ya

utafiti.

Katika usomaji Wetu, tumeweza kujitokeza na mifano halisi ambayo imekuwa ndiyo thibitisho ya yale ambayo tumeyashughulikia katika tasnifu hii.

1.10: HITIMISHO

Tunaamini ya kuwa maswala yote tuliyoyagusia katika sura hii ya kwanza yametuweka katika hali nzuri ya kutekeleza uchambuzi na uchanganuzi wa dhana na matatizo katika tafsiri kama taalum yenye upekee kiusomi.

Tunaamini ya kwamba yale ambayo tumeyagusia, yana umuhimu sana kwa kazi tunayoishughulikia, aghalabu kwenye vipenglele tunavyovichunguza, na pia kwamba yametupatia fursa ya kutathmini iwapo tafsiri hiyo Risasi Zianzapu Kuchanua (1975), imedumisha au kupotosha uaminifu wake kama tukio halisi la kimawasiliano na la upitishaji ujumbe kutoka lugha asilia hadi katika mfumo na muktadha wa kijamii wa lugha pokezi.

1.11: TANBIHI

1. Culy, M.M. (1993), "The Top-Down Approach To Translation" katika, Barnwell K. (mha), Notes On Translation, Vol.7 No 3, Summer Institute of Linguistics, Inc. Dallas USA. u.k. 28.

2. Catford, J.C. (1965), A linguistic Theory of Translation,
O.U.P, London, u.k. vii
3. Kama 1 u.k. 29.
4. Zaja, Ø. (1986) "Fasihi Tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya
kiswahili:matatizo na athari zake." Tasnifu
ya M.A., chuo kikuu cha Nairobi. u.k. 2.
5. Kama 2 u.k. 20.
6. Hatim, B na Mason. I (1990), Discourse and the Translator.
Longman, London/New York u.k. viii.
7. Guenther, F. na Guenther-Reutter. M (1978) Meaning and
Translation. Gerald Duckworth and Co, Ltd,
G.Britain u.k. 29.
8. Larson, M.L. (1984), Meaning-Based Translations: A guide To
Cross-Language Equivalence. University Press
of America Inc. u.k. 3

9. Gutt, E.A. (1991); "Translator's perspective on meaning, A relevance theory: A guide to successful communication in translation", katika Barnwell, K. (ed) Notes On Translation, S.I.L. Inc. Dallas, U.S.A. u.k. 36.
10. Crystal, D. (1987) The Cambridge Encyclopedia of Language. Cambridge Univ. Press, Cambridge/New York u.k. 101
11. Hartmann, R.R.K. na Stork F.C. (1972) Dictionary of Language and Linguistics. Applied Science Pub. Ltd., London, u.k. 42

SURA YA PILI

2.0: DHANA MBALIMBALI ZA TAFSIRI

2.1: UTANGULIZI

Sura hii inahusu dhana zifuatazo; (i) tafsiri, (ii) mawasiliano, (iii) muktadha na (iv) maana, ambazo zina ufungamano mkubwa na tukio la tafsiri. Vilevile sura hii inatazama aina za tafsiri kulingana na maoni, madai na fafanuzi za wasomi mbalimbali wa taaluma hii.

Hata hivyo, si lengo letu kupitia na kuorodhesha maoni au madai ya kila mmoja aliyewahi kuandika kuhusu tafsiri kwa vile jambo hilo haliwezi kutendwa kwa njia rahisi na pia kwa sababu upeo wetu unalenga tu kutazama dhana hizi tunazozifafanua kwa namna ambayo itatuwezesha kuweka wazi vipengele ambavyo hushirikishwa katika uwanja huu uliogubika na ambao unahitaji kueleweka kiusomi.

Kueleweka vyema kwa dhana na nadharia zinazotumika katika tafsiri, huwa msingi imara katika kubainika kwa maelezo ya wataalamu wa somo hili, mbali na kutuwezesha kuhusisha dhana hizo na somo letu la utafiti, ambalo linahusu dhana na matatizo ya tafsiri.

Baadhi ya madai na mitazamo ya wataalamu kuhusu vipengele mbalimbali katika sura hii, yanapingana, ilhali kwa upande mwingine baadhi ya madai yanaafikiana kwa jumla.

2.2: DHANA YA TAFSIRI

Tangu miaka mingi iliyopita na hata kufikia sasa mambo mawili ya kimsingi yaliyotiliwa msisitizo na wananadharia wa tafsiri ni vipengele vya maana na mawasiliano ambavyo hutazamiwa kupitishwa kwa namna iliyodumisha uaminifu na ukubaliano baina ya matini asilia na matini pokezi kama Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Miaka ya hivi karibuni, imeshuhudia ongezeko la msisitizo kwa kipengele cha muktadha wa matini, katika tukio la tafsiri. Hivyo vipengele vyote havina budi kuzingatiwa katika tasnifu hii, ili kuweza kutambua hatua zilizopigwa hadi kufikia sasa katika dhana ya tafsiri, na maswala yote yanayohusiana nayo.

Kuzingatia vipengele vyote tulivyovitaja humwezesha mtafsiri kukwea hadi upeo wa juu, kuzama ndani kwa urefu na hatimaye kuibuka na matini nzuri inayotosheleza kanuni na matarajio ya pande zote zinazohusishwa katika tafsiri, kadri iwezekanavyo.

Uhuru mwingi wa kupindukia, waliojipatia, baadhi ya watafsiri umewafanya kupuuza haja ya kuzingatia vipengele vyote vya dhana ya tafsiri, hii ndiyo sababu mojawapo inayotufanya kupata matatizo kama yale ya mtafsiri kupotosha dhamira ya mwandishi asilia, kuvuruga maana na hata ujumbe uliotazamiwa kuwasilishwa katika Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Dhana ya tafsiri, si mpya kiusomi. Hata hivyo inahitaji ufafanuzi, ambao tutautoa kwa jinsi ambayo inatathmini na kuoanisha maoni ya wananadharia wa tafsiri.

}

Mtazamo wa kwanza ni ule ambao unasisitiza maana na mawasiliano katika tafsiri. Newmark (1981: 88) na wengine, wanadai kwamba tafsiri mwafaka huwa tukio linalojumuisha vipengele vya tafsiri maana na vile vya tafsiri mawasiliano.

Wanaongezea ya kuwa vipengele vya maana au semantiki katika tafsiri huhusiana na; kueleweka kwa ujumbe katika muktadha wa matini pokezi na kwa upande mwingine ujumbe huo kuwa na athari kimawasiliano kwa HP.

Aidha Newmark, anakubaliana na dai kwamba mtafsiri anapaswa kudunisha uaminifu wake kwa:

- (i) mwandishi wa matini asilia,
- (ii) kaida za lugha pokezi na,
- (iii) mpokeaji ujumbe wa tafsiri (hadhira).

Maoni ya Newmark hayaonyeshi kupendelea njia moja maalum na mwafaka zaidi kuliko zinginezo katika kutafsiri. Kwa hivyo tunaonelea ya kuwa mtafsiri anaweza kufanikiwa zaidi kwa kujumuisha njia za kimawasiliano na za kimaana, wakati wa kushughulikia matini yake.

Licha ya ukweli kwamba ujumuishi kama huo unaweza kuleta mafanikio zaidi, hiyo si kinga dhabiti dhidi ya matukio kama vile, matini kuonekana kuegemea upande au aina moja ya tafsiri, hali ambayo ni tatizo kivyake katika somo hili.

Katika diwani tunayoichuguza, tatizo hili linadhihirika katika baadhi ya mashairi; kwa mfano, neno tropics (MA:60), linatafsiriwa kama Afrika (MP:65). Mtafsiri anaonekana kuzingatia zaidi ufasiri

wa neno hilo kwa namna inayoweza kuwasilika kwa hadhira yake, badala ya kuzingatia maana halisi ya neno lenyewe.

Newmark vilevile aliainisha matini katika makundi matatu ambayo ni (i) matini hisishi; ambayo hudhihirisha hisia za mwandishi kwa hadhira yake, (ii) matini tekelezi, ambapo kwayo mwandishi hutoa onyo, wito au ombi fulani, ambalo yeye hutarajia wasomaji wake kuchukua hatua na kulitekeleza.

Kwa mfano mashairi mengi yaliyohusu upiganiaji uhuru kama yaliyo katika Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) yalitazamiwa kuwazindua wote waliozisoma, (iii) matini fahamishi, ambayo dhima yake ni kufahamisha hadhira, mambo ambayo mwandishi anatazamia kuwajulisha, lengo lake ni kupitisha ujumbe bila ya kujali jinsi utakavyopokelewa au athari zake; kwa wapokeaji.

Uanishaji huu ulifungamana na dai la Newmark (1988) kwamba mtafsiri sharti aelewe vyema kundi ambamo matini fulani yanajikita ndipo aweze kutekeleza tafsiri kuambatana na matarajio ya mtunzi asilia.

Kwa kiasi fulani tunakubaliana na Newmark, ingawa tunatilia shaka kigezo alichotumia wakati wa kugawa matini katika hayo makundi matatu. Vilevile si jambo rahisi kutilia kazi za fasihi mipaka ya aina hiyo, kwa kuwa wakati mwingine kazi hizo hutekeleza dhima nyingi kwa pamoja. Dhima zenyewe ni zaidi ya hizo tatu, alizozitaja Newmark.

Chang (1990) ambaye anapinga huu mtazamo wa Newmark wa kugawanya matini katika dhana ya tafsiri, anapendekeza kwamba yanayombidi mtafsiri wa matini ya kifasihi kufanya ni kuumba upya

matini asilia, kwa kuzingatia miundo na mifumo ya lugha pokezi ambayo yatakuwa na manufaa ya kisanaa, sambamba na yale ya matini hayo katika lugha asilia.

Kwa jumla basi Chang vilevile anadokeza umuhimu wakuzingatia maana ya ujumbe katika tafsiri.

Kelly (1979), kama wananadharia wengine, anakiri kuwepo kwa udhaifu katika kila mojawapo ya nadharia tofauti za tafsiri. Kwa hivyo anapendekeza kwamba mtafsiri achunguze vyema lugha zote zinazoshirikishwa katika tafsiri ili aweze kupata mantiki ya matini asilia na kisha kuiwasilisha kwa misingi, kaida na miundo ya lugha ya matini pokezi.

Anaonelea kwamba tafsiri huwa na madhumuni ya kuunda matini yenye maana sawa na ile ya matini asilia. Vilevile anapendekeza kwamba mtafsiri sharti atilie maanani hisia zake mwenyewe wakati wa kutafsiri. Wakati huo huo mtafsiri aonishe mtazamo wake na ule wa mtunzi asilia; kwa minajili ya kujiepusha na utatanishi unaoweza kutokea.

Bila ya kufanya hivyo, Kelly anadai, mtafsiri hawezi kamwe kuibuka na tafsiri nzuri yenye kulingana na kazi asilia. Hayo maelezo ya Kelly, ni hatua kubwa sana katika dhana ya tafsiri kwa vile yaliguzia vipengele vya maana na mawasiliano na viziada vya jumla katika tafsiri.

Kundi lifuatalo la wasomi linakubaliana kwa jumla ya kwamba wakati wa kutekelezwa kwa tafsiri kuna hali ya kubadilishwa au kuhamishwa kwa kitu fulani, aghalabu kitu hicho ni ule ujumbe au maana iliyo kwenye matini.

}

Rabin (1958), kwa mfano alielezea tukio la tafsiri kama, kubadilisha katika lugha nyengine ukihifadhi mantiki ...kadri iwezekanavyo, kwa sababu baadhi ya mambo yaliyo katika kazi/matini asilia hupotea..,"¹ anaongezea ya kwamba dhamira kuu ya huo ubadilishaji ni kuwasilisha maana iliyokuwepo katika lugha ya kwanza.

Maelezo ya Rabin, yana ujumla mwingi sana, nayo hayaonyeshi waziwazi yale ambayo yamebadilishwa, hata hivyo anaporejela uhifadhi wa mantiki anaashiria ya kwamba maana vilevile ni muhimu wakati huo wa kuhamisha ujumbe hadi lugha ya pili.

Maelezo ya Rabin yanaweza kulinganishwa na kule kubadilishwa kwa matini yetu ya asilia When Bullets Begin To Flower (1972) kutoka lugha ya kiingereza hadi Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), katika Kiswahili.

Wengine kama Forster (1958), wanakubaliana na kauli hiyo ya uhamishi wa yaliyomo katika matini ya lugha moja hadi katika lugha nyengine, bila shaka kwa kuzingatia miundo na matumizi ya maneno katika lugha hiyo.

Massamba (1990), vilevile aliitazama dhana ya tafsiri kama, "habari iliyohamishwa kutoka kwenye lugha moja kwenda lugha nyingine."²

Mtazamo wa tatu ambao wananadharia wameupatia dhana hii ni kwamba, tafsiri ni somo ambalo hufungamana na nyanja nyinginezo za usomi kwa vyovyote vile.

Catford (1965) alitilia sana mkazo umuhimu wa tafsiri kuazima mambo kadhaa kutokana na nadharia ya lugha. Alifikia hata

kujitokeza na nadharia iliyozingatia mtazamo wa kiisimu katika tafsiri.

Hiyo nadharia huchukulia/hutazama tafsiri kama "tukio linalotekelezwa katika lugha kwa kubadilisha matini katika lugha moja hadi katika lugha nyingine, huku umbo la lugha likibadilishwa pia."³

Huu mtazamo wa Catford, unatoa kauli muhimu ingawa vilevile unaonyesha kupuuza umuhimu wa vipengele vinginevyo katika tafsiri kama vile muktadha, ambayo ina nafasi kubwa katika tafsiri kijumla.

Larson (1984) vilevile alionelea kwamba tafsiri ilihusu uhamishaji ama ubadilishaji maana iliyo katika matini asilia hadi katika matini tafsiri, kwa kuzingatia muundo kisemantiki. Haya maelezo, sawa na ya Catford, yanaegemea zaidi kwenye nadharia ya isimu.

Kwa jumla, wananadharia wanaozingatia mtazamo huu husisitiza maswala yanayohusiana na leksia, miundo ya kisarufi na maana ya maneno, kwa minajili ya kuunda upya yale ambayo mtafsiri anajihusisha nayo, katika lugha pokezi.

Akifafanua zaidi maelezo yake ya dhana ya tafsiri, Catford (1965), alielezea ya kuwa maneno katika lugha pokezi huwa visawe vinavyoamaanisha dhana fulani, sawa na ilivyo katika matini asilia. Hivyo basi inabidi vipengele vya lugha ya tafsiri kujikita katika hali za kimuundo na kihusiano baina ya vipengele na kanuni za utoaji maana katika lugha hiyo.

Wanavyosisitiza ni kwamba kaida za lugha asili zisilazimishwe kamwe kwenye mfumo wa lugha pokezi. Kwa mfano baadhi ya misamiati

katika makala yetu ya asili When Bullets Begin To Flower (1972) kama vile batuque (MA:61) na quissangua (MA:100), imetafsiriwa katika makala pokezi Risasi Zanzapo Kuchanua (1975) kama batuki⁴ (MP:66) na kisangwa⁵ (MA:109), kwa kuzingatia mbinu ya utohozi ambayo inahamisha msamiati hadi katika lugha pokezi kwa kulipatia neno, umbo linalozingatia kaida za lugha hiyo.

Catford (1965) hali kadhalika anakubaliana na kauli ya kuwa baadhi ya vipengele vya lugha asilia huhamishwa hadi katika lugha pokezi bila ya kubadilishwa kwa namna yoyote ile, kwa mfano katika (MA:45) neno magaica⁶ limehamishwa hadi katika (MP:48) kama magaica, bila ya kutohoa au kubadilisha kitu chochote, kwa sababu neno hilo hurejelea dhana ambayo imejikita kwenye utamaduni na muktadha wa watu wa eneo ambamo MA limeandikwa.

Dostert, anaihusisha dhana ya tafsiri na sayansi, pale ambapo anadai ya kwamba, taaluma hii ni tawi la sayansi tendi ya lugha ambayo huhusu haswa, kuhamishwa kwa maana kutoka seti moja ya ishara zilizopangiliwa hadi katika seti nyingine ya ishara zilizopangiliwa.

Steiner (1975) naye alijadili dhana ya tafsiri kwa kuifungamanisha na mambo manne ambayo husaidia katika kueleweka na kufasirika kwa dhana hii.

Mambo hayo ni (i) uaminifu baina ya MA na MP
(ii) upimifu baina ya lugha zinazohusika, hivi kwamba mojayazo isipunguze au kuongeza kupita kiasi (iii) mtafsiri kuwa na hamu katika shughuli za tafsiri na (iv) kujaribu kufidia matatizo yanayozuka wakati wa kutafsiri, kadri iwezekanavyo.

Alionelea ya kwamba kanuni hizi zinapozingatiwa, mtafsiri anaweza kujiepusha na makosa kama vile kupotosha lengo la mwandishi asilia na hali ya kutoafikiana unaoweza kuwepo baina ya MA na MP.

Mapendekezo ya Steiner kuhusiana na jinsi ambavyo mtafsiri anaweza kufidia tatizo la udondoshi na uongezaji wa vipengele katika MP kupita kiasi ni kwamba, mtafsiri azingatie usawazisho baina ya matini asilia na tafsiri yake, katika viwango mbalimbali vya kategoria za lugha.

Kazi za kinadharia katika miaka ya hivi karibuni kuhusiana na dhana ya tafsiri, zimetuelekeza kutambua ya kuwa mitazamo imeendelea kubadilika mbali na kuhusisha mambo mengi zaidi ya yale ambayo wasomi wa awali waliyaelezea.

Bradley (1991), ni mmoja wa hao wasomi wa kisasa wanaodai kwamba, "kimsingi mtafsiri, hujihusisha na maana ya matini, jinsi anavyoiamisha kutoka lugha moja hadi nyingine kwa minajili ya kuwasiliana."⁶

Madai hayo yanaoanisha dhana mbili muhimu sana katika tafsiri, ambazo ni maana na mawasiliano. Anayomaanisha Bradley ni kwamba mtafsiri avumbue na kujitahidi kuelewa maana sahihi ya matini katika lugha asilia ndipo achukue hatua ya kuihamisha maana hiyo, jinsi inavyotakikana hadi katika MP.

Kunao wananadharia wengine ambao wamehoji maoni ya hao wasomi wanaojikita katika maana na mawasiliano.

Madai ya wanaohoji ni kwamba, katika dhana ya tafsiri maana aliyoilenga mwandishi asilia haiwezi kuwasilishwa na mtafsiri, vile

vile kuna maoni kwamba ukweli na uhalisi ni mambo mawili yasiyotengana katika lugha. Kwa hivyo katika tafsiri ambalo ni tukio katika lugha, ukweli wa kauli zinazotafsiriwa unapaswa kuambatana na uhalisia wa kauli hizo katika maisha.

Kundi la nne, ni la wasomi wanaoegemea uchanganuzi wa usemi na vipengele vyake. Miongoni mwao ni Basil na Hatim (1990) ambao wanarejelea dhana ya tafsiri kama tukio ambalo hutoa nafasi, kwa wasomi; ya kuchunguza na kulinganisha lengo la mtunzi asilia, kisaikolojia na kijamii na lengo la mtafsiri.

Mtazamo huu wa tafsiri, unaifananisha dhana hii na mawasiliano baina ya wanadamu, mbali na huko kutoa fursa ya kuchanganuliwa kwa mahusiano tata ya kibinadamu katika ulimwengu wa MA na ule wa MT. Vilevile unachunguza mahusiano baina ya dhana ambazo hushirikishwa katika uumbwaji wa miktadha ambayo kwayo tunapata kuwasiliana.

Uchanganuzi wa usemi ulitokana na majaribio ya wanafalsafa, ya kuchanganua vipashio vya lugha, ambavyo ni vikubwa zaidi kuliko leksia na hata sentensi, kwa kutazama jinsi ambavyo mafungu yaliyodondolewa kutokana na maongezi au maandishi yaliweza kutoa maana, kuwa na muwala, mshikamano baina ya sentensi mbalimbali zinazojenga hayo mafungu n.k.

Kutokana na upana wa mtazamo huu, tafsiri haichukuliwi tu kama tukio linaloweza kuzingatiwa kiisimu pekee, bali pia kwa misingi ya hali za kijamii na viziada lugha vinginevyo katika mazingira ya maongezi au maandishi yanayotafsiriwa na jinsi yanavyochangia maana ya ujumbe unaowasilishwa.

Wanaongezea kwamba tafsiri ni somo mwafaka katika kumulika swala zima la dhima ya lugha katika maisha ya jamii fulani. Dai lao linathibitika kwa ukweli ya kwamba tafsiri haiwezi kamwe kuepushwa na muktadha wa kijamii kwa namna yayote ile. Iwapo lengo la mtafsiri ni kufikia viwango vya juu kiutekelezaji, hasa katika matini ya kifasihi, hana budi kutilia maanani muktadha.

Kazi tunayoichanganua ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) kama tutakavyoona katika sehemu ya 4.1 imejikita kwa kiwango kikubwa sana katika muktadha wa kijamii wa huku Afrika ya mashariki, ilhali MA. yake When Bullets Begin To Flower (1972), imejikita katika muktadha wa jamii za watu wa eneo la kusini mwa bara Afrika.

Kujitokeza na kitendo kipya cha kimawasiliano (MP) kutokana na kile cha awali (MA), huwaweka watafsiri wengi katika hali ya shindikizo, ambapo ukweli wa hali zao wenyewe kijamii hukabiliana na hitaji la kupitisha maana inayotolewa na mwandishi wa MA, hadi kwa wapokeaji wa matini iliyotafsiriwa. Ulimwengu wa wapokeaji MP. aghalabu huwa tofauti na ule wa wapokeaji wa MA.

Huu mtazamo wa wachanganuzi usemi unaonekana kuzingatia dhana ya tafsiri kama tukio muhimu la kimawasiliano ambalo huendeshwa/hutekelezwa kwenye muktadha maalum wa kijamii. Wamejumuisha maswala mengi ambayo mtafsiri sharti ayazingatie katika shughuli zake. Tunakubaliana nao kimtazamo.

Madai na maelezo haya ya wananadharia tofauti tofauti kuhusu dhana ya tafsiri na utekelezaji wa tukio hilo, yanadhihirisha kuwepo kwa maafikiano makubwa kuhusu vipengele mbalimbali vya taaluma ya tafsiri, ingawa vilevile kwa jumla kuna tofauti

ndogondogo kuhusu yale ambayo wasomi tofauti wameyapa msisitizo zaidi.

2.2.1: AINA ZA TAFSIRI

Beekman na Callow (1974) wamegawa tafsiri katika aina mbili za kimsingi ambazo ni: tafsiri za moja kwa moja na tafsiri huru. Waligawa tena, kila mojawapo ya aina hizi mbili za kimsingi, na hivyo basi kwa pamoja wakawa na aina nne za tafsiri ambazo ni (i) tafsiri za moja kwa moja zilizokiuka mipaka, (ii) tafsiri huru, (iii) tafsiri zilizofanyiwa marekebisho na (iv) tafsiri maana.

Waliyafupisha madai yao kwa mchoro kama ufuatao.⁸

AINA ZISIZOKUBALIKA			
AINA ZINAZOKUBALIKA ZAIDI			
Tafsiri za moja kwa moja zilizo kiuka mipaka	Tafsiri maana	Tafsiri za moja kwa moja zilizofanyiwa marekebisho	Tafsiri huru zaidi

[Tafsiri Yetu]

Madai yao ni kwamba tafsiri maana na tafsiri za moja kwa moja zilizofanyiwa marekebisho, hukubalika zaidi ya hizo zingine kwa vile zina uwezo wa kudhibiti kitendo cha kutafsiri kwa njia bora zaidi.

Kwa upande mwingine, tafsiri huru zaidi na tafsiri za moja kwa moja zisizofanyiwa marekebisho au zilizokiuka mipaka, hazikubaliki sana, kwa kuwa hazitekelezi tafsiri kwa namna bora kama hizo aina mbili tulizotaja awali.

Yale ambayo Beekman na Callow (1974) wanataja kama mitazamo miwili ya kimsingi/aina mbili za kimsingi za tafsiri yalijikita katika dhana ya muundo.

Iwapo muundo wa matini tafsiri unafanana zaidi na ule wa lugha pokezi basi tafsiri hiyo inachukuliwa kuwa ya maana na iwapo, huo muundo wa matini tafsiri haufanani sana na ule wa lugha pokezi na badala yake unafanana na ule wa lugha asilia, basi tafsiri hiyo inachukuliwa kuwa ya moja kwa moja.

Hata hivyo uchunguzi umeonyesha ya kwamba mara nyingi watafsiri huoanisha aina hizo mbili za tafsiri katika shughuli zao.

Madai ya Beekman na Callow (1974), kuhusu aina za tafsiri yanakanganya, kwanza ni kwa vile wanajitokeza na mitazamo miwili ya kimsingi ambayo wanadai inapogawanywa zaidi huzua aina nne za tafsiri, hawaelezi kigezo wanachokitumia katika ugawaji wa aina hizo nne, jinsi ilivyo katika mchoro wao.

Jambo la pili linalowakanganya wengi ni lile dai lao kwamba mitazamo hiyo miwili ya kimsingi ya tafsiri (tafsiri huru na tafsiri za moja kwa moja), huainisha aina za tafsiri kwa mujibu wa muundo pekee na wala si maana. Kufuatana na hayo madai, hatuelewi ni vipi ambavyo wanajitokeza na tafsiri maana ambayo tunajua kigezo chake cha uainishaji kimsingi huwa maana nayo hujikita kwenye vipengele vya maana ya matini.

Ali (1980) na Zaja (1986) waliorodhesha aina zifuatazo za tafsiri : (i) tafsiri za moja kwa moja, (ii) tafsiri maana na (iii) tafsiri huru.

Walizichukulia hizi zote kuwa miongozo ya kutafsiri ambayo hutegemeana kwa kutegemea yale ambayo yanatafsiriwa.

Zaidi ya hizo tatu, Zaja (1986) aliongezea aina ya nne ambayo ni tafsiri mawasiliano. Kufikia sasa, taaluma ya tafsiri inatambua zaidi, hizi aina nne za tafsiri.

Tumeelezea zaidi kila mojawapo ya hizo aina nne hapa chini, tukionyesha ubora na dosari zao zinapotumika kwenye tukio la kutafsiri.

2.2.2: TAFSIRI ZA MOJA KWA MOJA.

Ni aina ya tafsiri ambayo husisitiza zaidi kuwepo kwa ulinganifu wa vipengele kama; maneno, maana, umbo la lugha ya MA na ile ya MP. katika tukio la kutafsiri.

Walivyodai Beekman na Callow (1974) ni kwamba tafsiri hii, hupitisha vipengele vya lugha asili hadi kwenye lugha pokezi, kwa jinsi ambavyo ulingano na uafikiano mkubwa baina ya lugha hizo huweza kudhihirika.

Vilevile tafsiri ya aina hii huzingatia; usahihi, uhalisi na uaminifu wa kupitisha ujumbe.

Inapotekelezwa kwa ukamilifu zaidi, tafsiri ya aina hii, hufikia hali ambapo neno katika MA, linatafsiriwa kwa neno ambalo ni kisawe chake katika MP.

Hatua kama hiyo, ya kutafsiri neno kwa kisawe katika lugha pokezi, bila ya kujali tofauti za kimfumo baina ya lugha zinazoshirikishwa, imefanya tafsiri za moja kwa moja kuwa na matatizo mengi sana.

Jambo la kwanza ni kuwa, maana ambayo hutokana na mpangilio wa maneno katika MA, hupuuzwa katika tafsiri ya aina hii, kwani maneno yanapoambatanishwa tu kiholela bila ya kutilia maanani, mautiki ya ujenzi wa vipashio vyenye maana katika MP, basi sentensi zinazoibuliwa hupoteza mshikamano na mtiririko unaotakikana.

Tafsiri ya aina hii vilevile hukumbwa na udhaifu wa MP, kuwa na maana isiyoambatana vyema na iliyo kwenye MA. Utata pia huzuka katika ujumbe unaowasilishwa, kwa hivyo hadhira pokezi ya MP hutatizika.

Dhamira ya mwandishi wa MA, mara nyingi haiwasilishwi kwa hadhira ya MP.

Tafsiri ya moja kwa moja pia hujaribu kulazimisha sura ya lugha ya MA kwenye umbo la lugha ya MP, bila ya kujali ya kuwa kila lugha huwa na upekee wake wa namna ya kupangilia vipashio vya kisarufi, kuumba maneno, sauti⁹, n.k. Kwa kawaida upekee wa LA huifanya kutofautiana na lugha nyingine yoyote, kwa mfano mfumo wa lugha ya Kiingereza iliyotumiwa kwa matini yetu asilia ni tofauti kabisa na ule wa Kiswahili, ambayo imetumiwa katika matini yetu pokezi.

Dosari lingine, ni kwamba, msomaji/mpokeaji wa MP hupuuzwa na aina hii ya tafsiri ambayo hujikita zaidi katika fikra na mtazamo wa mwandishi asilia na lugha yake kuliko jinsi ambavyo inazingatia

matarajio ya hadhira ya MP, lugha yao na jinsi ambavyo mtafsiri huelewa na kufasiri maana.

Tunavyoelewa, sawa na wasomi wengine ni kwamba huwa vigumu sana kupata maneno na maumbo kwenye lugha pokezi yenye usambamba wa reale kwa ya pili na yale ya lugha asilia.

Usarufi na pia uwasilishwaji wa maana sahihi kwenye lugha pokezi huathirika vibaya na wakati mwingine kuvurugika kabisa, mtafsiri anapotumia tafsiri za moja kwa moja.

Aghalabu tafsiri ya aina hii hukabiliwa na tatizo la upuuzwaji wa muktadha wa matumizi na mahusiano baina ya maneno katika sentensi/ubeti kwa misingi ya uhusiano wa kiusilasila na kiuolezo faridi.¹⁰ Kupunguka kwa thamani ya kimawasiliano na kupotoshwa kwa kauli ya uaminifu kwenye lugha pokezi pia hutokea.

Uchunguzi umeonyesha ya kuwa, uwiano wa vipengele vya lugha kama vile maneno, hutiliwa maanani zaidi na tafsiri ya aina hii. Hatua hiyo wakati mwingine huwafanya watafsiri kujaribu kurekebisha miundo ya kisarufi ya lugha pokezi, ili iafikiane na ile ya lugha asilia, lau sivyo wao hujaribu kuilazimisha moja kwa moja hasa katika matini kama za kishairi ambazo zinaruhusu uhuru mwingi wa kutumiwa kwa lugha na ubunifu wa mtafsiri vile vile.

2.2.3: TAFSIRI MAANA

Tafsiri maana, hulenga kupitisha maana iliyo kwenye MA hadi kwenye MP, huku mtafsiri akitambua ya kuwa miundo ya lugha asilia na ya lugha pokezi hutofautiana. Hivyo basi maana anayoipitisha,

mtafsiri, huifikia hadhira yake katika miundo ya kisarufi na ya kileksia, ya lugha pokezi.

Akifafanua aina hii ya tafsiri, Newmark (1981) alitoa kauli ya kwamba, "tafsiri hii, hujaribu kadri iwezekanavyo kuwasilisha maana kamili ya ujumbe kwenye muktadha wa MA, kupitia miundo ya kisarufi na ya kimaana ya lugha pokezi.

Vilevile tafsiri maana hujikita katika taratibu na utamaduni wa jamii ya MA, bila ya kusahau muktadha wa lugha asilia ili kuhakikisha kwamba maana inayowasilishwa ndiyo ambayo ilitazamiwa na mwandishi wa MA..."¹¹

Kipengele cha maana hupewa nafasi kubwa katika aina hii ya tafsiri, jinsi ambavyo Hollander (1959) ameonyesha kwa maoni kwamba, "kutafsiri sentensi kutoka lugha moja hadi nyingine, kwa namna fulani, ni kuvumbua maana yake na kisha kuunda sentensi yenye maana kama hiyo katika lugha pokezi"¹² [Tafsiri Yetu].

Tafsiri maana inaruhusu neno la MA kutafsiriwa kwa namna nyingi kwenye lugha pokezi kwa kutegemea muktadha wa matumizi yake. Sio lazima kwamba neno la MP liwe na uwiano au usambamba wa moja kwa moja na lile la lugha asilia. La muhimu ni maana ya ujumbe.

Jambo lingine ambalo huzingatiwa na aina hii ya tafsiri ni muwala na muumano wa kisarufi kati ya maneno, jinsi yalivyopangiliwa na ambavyo yanakubalika kufuatana katika sentensi za MP, ili maana halisi ya MA iweze kuwafikia wasomaji wa MP.

Kwa hakika tafsiri maana, hutazamwa kama kiungo cha kati, baina ya tafsiri za moja kwa moja na tafsiri huru, kwa vile tafsiri hii huoanisha baadhi ya kanuni za kila mojawapo ya aina hizi mbili

za tafsiri. Hata hivyo msisitizo wake hubakia kwenye kipengele cha maana.

Zaja (1986) alielezea kwamba, "wakati mwingine tafsiri maana na mawasiliano hupatana na kutiliana nguvu, hasa pale ambapo makala yanayowasilishwa hayafungamani na utamaduni wowote maalum", aliongezea kwamba "ni vigumu kuweka mipaka kati ya hizi namna mbili za tafsiri."¹³

Si jambo geni kwamba tafsiri nzuri hujaribu kuoanisha zaida ya aina moja ya tafsiri. Vivyo hivyo aina za tafsiri zinaweza kufanana sana. Licha ya hayo, tungependa kuisisitiza ya kuwa tafsiri maana ni tofauti na tafsiri mawasiliana hasa tukizingatia yale ambayo kila moja yazo husisitiza kimsingi, na jinsi ambavyo kanuni zao hutekelezwa.

Jambo ambalo huwafanya watafsiri kuoanisha aina tofauti za tafsiri ni kwamba wametambua ya kuwa kila aina ya tafsiri huwa na pungufu zake ambazo zinaweza kupunguzwa kwa njia ya kuhusisha kaida/kanuni za aina nyingine za tafsiri.

Udhaifu mkubwa wa tafsiri maana ni ule wa kuongeza au kudondosha vipengele vya lugha asilia, wakati wa kutafsiri, vilevile kule kujikita zaidi kimaana katika lugha asilia ni tatizo, kwa vile lugha pokezi pia huwa na muktadha wake.

2.2.4: TAFSIRI HURU

Tafsiri huru, hulenga kuuweka wazi na kuufanya ujumbe wa matini kuwa wenye kufaa kwa hadhira ya lugha pokezi.

Mtafsiri hupata maana ya MA, kisha akaifasiri akilini mwake wakati huohuo akiifanyia marekebisho ili kutimiza malengo hayo.

Jambo linalopewa umuhimu zaidi ni ule ufikishaji wa ujumbe kutoka lugha asilia hadi katika lugha pokezi.

Tafsiri ya aina hii vilevile huhusu/hushughulikia mambo kama vile mtindo wa matini, muktadha wa matumizi ya lugha (k.v. katika mahubiri, hotuba ya kisiasa, mafundisho n.k.), sajili ya lugha inayotumika, sarufi ya lugha zinazohusika n.k.

Baadhi ya kauli za tafsiri huru hupingana na zile za tafsiri za moja kwa moja, kwa sababu mambo ambayo hutekelezwa katika tafsiri ya aina hii, hayatekelezwi katika tafsiri za moja kwa moja.¹⁴

Mighairi ya kwamba tafsiri hii hupitisha ujumbe unaotakikana, uwasilishaji wake huwa dhaifu sana kwa vile ni tafsiri inayoandamwa na matatizo mengi.

Tafsiri hii humpa mtafsiri uhuru mwingi sana. Jambo hilo huvuruga maswala/mambo mengi na hata kusababisha mabadiliko kwenye maudhui/ujumbe wa MA, na vivyohivyo kuathiri maana ya ujumbe wote wa matini inayotafsiriwa.

Mabadiliko kama hayo hutokea wakati ambapo mtafsiri ana futilia mbali au kufafanua zaidi yale ambayo yanasemwa na MA. Udondoshi au uongezaji wa vipengele kwenye MP, unafaa kufanywa kwa namna ya uangalifu ndipo uhalisi wa ujumbe uweze kudumu.

Ali (1981) anasema, msisitizo wa tafsiri huru, kwa vyovyote vile hujikita zaidi katika ujumbe au habari inayowasilishwa kwa HP kuliko jinsi ambavyo vipengele vya kimtindo na umbo la matini pokezi

huzingatiwa.

Kama ambavyo tumeelezea, pana uwezekano wa thamani ya ujumbe unaowasilishwa kuzidishwa au kupunguzwa kupita kiasi.

Pia ni aina ya tafsiri isiyoweza kudhibiti vilivyo, umbo la MA, kwa vile inaruhusu kuondolewa na kuongezwa kwa sifa na vipengele mbalimbali katika lugha. Basi matini inayozalishwa baada ya tafsiri hukumbwa na hatari ya kupitisha maana tofauti kabisa na ile ya MA.

Katika matukio yote ya tafsiri, hii pia ikiwemo, ni mwafaka mtafsiri kuzingatia utamaduni, mazingira, muktadha na mtindo wa matini. Tafsiri inaweza kupotosha ujumbe, thamani ya kimawasiliano, uhalisi na uaminifu wa MT kwa MA. Mambo haya hutokea mara nyingi sana katika tafsiri huru.

2.2.5 TAFSIRI MAWASILIANO

Aina hii ya tafsiri imetokana na mitazamo ya miaka ya hivi karibuni zaidi ambayo ilizuka kutokana na juhudi za wananadharia; kama Newmark, Lafevere, Firth, Nida, Beekman na Callow. Juhudi hizo zilihusu majarabio ya kuondosha pungufu zilizoko katika aina mbalimbali za tafsiri.

Dhamira ya kimsingi ya tafsiri mawasiliano ni kuwasilisha ujumbe wa MA kikamilifu kwa mpokeaji. Mwegemeo huu wa tafsiri unadhihirika kupitia nadharia ya mawasiliano.¹⁵

Kadri iwezekanavyo, aina hii ya tafsiri hujaribu kuipitisha mguso wa MA hadi kwa HP. Mambo mengi yanayoweza kuzua utata,

hurahisishwa na mtafsiri kwa minajili ya kuwasiliana vyema na mpokeaji ambaye hutakikana kuuelewa ujumbe vyema, kupitia kwa mfumo wa kisarufi, kimaana na kisintaksia, wa lugha pokezi. Linalotazamiwa na tafsiri hii ni kupokelewa kwa ujumbe sawa na vile ambavyo mpokeaji wa MA angeupata ujumbe huo katika lugha asilia.

Katika aina hii ya tafsiri, mtafsiri anaweza kuzidisha thamani ya mawasiliano aidha kwa kuboresha matini yake ya lugha pokezi au kwa kurekebisha matini asilia ili kuondoa makosa na vizuizi vinavyokinza kueleweka vyema kwa ujumbe unaowasilishwa, pasipo utata.

Wakati mwingine tafsiri hii hufutilia mbali vipengele vilivyoko kwenye lugha asilia iwapo hatua kama hiyo itaimarisha mawasiliano baina ya mtafsiri na hadhira pokezi.

Vilevile tafsiri hii hutilia maanani nafasi muhimu inayoshikiliwa na maswala ya muundo na sarufi ya lugha pokezi; mpangilio wa maneno kiuwiano, mtindo wa matini, mazingira, muktadha, utamaduni, mahitaji ya hadhira na wakati. Hivi vipengele ni miongoni tu mwa viziada lugha ambavyo huwepo katika lugha asilia.

Kwa kuzingatia mambo hayo yote mtafsiri huweza kumfikishia mpokeaji, ujumbe asilia, mawazo, dhamira na falsafa za mwandishi wa MA, bila ya matatizo mengi.

Uchunguzi umeonyesha ya kwamba tafsiri za aina hii huhusisha maswala na vipengele vingi sana kama inavyowezekana; jambo ambalo hutokana na hali ya tafsiri hii ya kujumuisha kwa undani mambo mengine yanayojitokeza katika zile aina zingine za tafsiri.

Kwa njia hiyo, tafsiri mawasiliano inaweza kuchukuliwa kwa jumla kama tukio la tafsiri linalojumuisha kauli za aina zote za tafsiri, kwa sababu za kutaka kufikia ubora wa hali ya juu.

Tafsiri mawasiliano imeweza kuonyesha udhibiti wa kuepuka dosari nyingi. Huu uwezo wa kuepuka dosari nyingi umetokana na kauli ya tafsiri hii ya kushirikisha kwa upana, mambo mengi yanayohusiana na tafsiri kwa jumla.

Zaja (1986) alipendekeza kwamba tafsiri mawasiliano, "ndiyo mwafaka zaidi kwa kuwa ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na kiasi kikubwa cha matatizo ya tafsiri."¹⁶

Tunakubaliana na madai ya Zaja kwa kiwango kikubwa kwa vile, baadhi ya kazi zilizowahi kutafsiriwa vyema zaidi na kufikia upeo wa juu, zilichukua mwegemeo huu wa kimawasiliano ambao hauna matatizo mengi sana kama aina zinginezo za tafsiri.

Newmark (1988), aliorodhesha aina zingine za tafsiri ambazo hata hivyo sio maarufu sana. Alizitolea maelezo mafupi aina hizo za tafsiri. Tunapendekeza ya kwamba hizi aina zaidi za tafsiri zinahitaji kuchunguzwa na wasomi, zaidi ya vile ambavyo zimechunguzwa kufikia sasa. Tumezielezea kwa kifupi hapa chini, hizo aina tano za tafsiri:

2.2.6: TAFSIRI KIKAZI/KIHUDUMA.

Hii ni aina ya tafsiri ambayo hutekelezwa wakati mtafsiri anapitisha matinj iliyo katika lugha ya kila siku na ya kawaida kimatumizi, hadi katika lugha teule. Aina hii ya tafsiri

husababisha MP kujikita katika nyanja teule ya somo au taaluma inayoshughulikiwa.

2.2.7: TAFSIRI WAZI - KINATHARI/KITUTUMBI

Mtindo huu wa tafsiri, uliainishwa na Rieu E.V.; ambao kwao, mashairi na tamthilia zilizo na umbo la kishairi hutafsiriwa kutoka katika mtindo huo, hadi katika mtindo wa kinathari/kitutumbi.

Badiliko la wazi ambalo huonekana katika aina hii ya tafsiri ni ule wa beti kubadilishwa na kuwa aya kwenye MP. Vilevile uakifisho wa kinathari kupitia kwa alama mbalimbali hujumuishwa kwenye tafsiri. Kifani, mabadiliko huwa si mengi, kwa mfano, sitiari na tamathali za usemi wa lugha asili huhifadhiwa kwenye MP.

Tafsiri hii pia hutilia maanani utamaduni wa jamii ya lugha asilia na hujaribu kuudumisha kadri iwezekanavyo.

Sifa za midundo na uwiano wa sauti ambazo kwa kawaida huwepo kwenye mashairi, hazipitishwi kamwe. Kwa hivyo aina hii ya tafsiri hufutilia mbali rithimu ya MA.

Tafsiri wazi-kinathari, huwa na manufaa ya kumwezesha mpokeaji wa MP, kupata maana ya ujumbe ingawa kwa upande mwingine hafikiwi na mguso sawa na ule ambao humfikia mpokeaji wa MA.

2.2.8: TAFSIRI UJUMBE/HABARI

Newmark (1988) anaelezea aina hii ya tafsiri kama ambayo hutilia mkazo uwezo wa mtafsiri kuwasilisha ujumbe wote wa MA kwa

jumla. Aghalabu tafsiri hii huhusu matini ambazo si za kinathari.

Wakati mwingine tafsiri hii hupangilia upya maneno ya MA, ili kuimarisha mantiki ya hayo matini katika MP, na kurahisisha uelewekaji wa MP miongoni mwa HP.

Jambo la muhimu kwa wanaozingatia aina hii ya tafsiri ni kule kupitisha ujumbe, bila ya kujali umbo la kazi yenyewe kwa jumla.

Aina hii ya tafsiri ina pungufu nyingi sana kama vile kufupishwa kwa MT wakati mwingine.

2.2.9: TAFSIRI KIUTAMBUZI

Hii ni aina ya tafsiri ambayo huzalisha upya ujumbe wa matini asilia katika matini pokezi kwa kubadilisha sarufi ya lugha asilia, na badala yake kutumia ile ya lugha pokezi. Mara nyingi tafsiri hii, hupitisha ujumbe, nahau na mafumbo kutoka MA hadi MP kwa njia ya maongezi ya kawaida. Hatua hiyo hufanya mambo kubainika vyema zaidi kwenye MP.

Lengo la tafsiri hii ni kuweka mambo yote waziwazi, kama inavyowezekana kwenye matini pokezi. Tatizo la aina hii ya tafsiri ni kwamba, umbuji, usanii na urembo wa MA, hupotoshwa na mara nyingi kupotezwa kabisa. Pana hatari ya mtafsiri kuzuka na MP isiyo na ladha wala mvuto wa kifani unaolingana na ule wa MA.

Maoni ya Newmark (1988) ni kwamba, aina hii ya tafsiri hufaa zaidi ikitumiwa katika kutafsiri matini zenye ugumu na utata mwingi, kwa sababu ya kuzifanya zieleweke vyema kwa wapokeaji.

Aina hii ya tafsiri inapotumiwa vyema kwa kuijumuisha na vipengele vya pragmatiki; matokeo huwa ni aina ya tafsiri inayooanisha kauli za tafsiri maana na zile za tafsiri mawasiliano.

2.2.10: TAFSIRI KIAKADEMIKI

Tafsiri kiakademiki ni aina mojawapo ya tafsiri ambazo huzingatiwa kule Ulaya, hasa Uingereza, katika baadhi ya vyuo vikuu.

Matumizi ya aina hii ya tafsiri hayajaenea sana katika sehemu zingine za ulimwengu. Kimsingi, aina hii ya tafsiri hubadilisha vipengele vya MA ili kuyafanya hayo matini kuwa yenye manufaa na yenye maana zaidi katika nyanja tofauti za kiusomi ambazo huwa kwenye rejista za kipekee.

Sababu za kuhaulisha lugha ya MA hadi katika rejista ya MP, huwa ni kuwasilisha vyema ujumbe uliotafsiriwa katika nyanja ya kiusomi inayohusika.

Tatizo la aina hii ya tafsiri hata hivyo, ni kwamba athari na mguso wa mwandishi asilia hufifia. Hali kadhalika hamu ya wapokeaji ujumbe hupunguzwa na ule ubutu wa lugha kirejista katika MP. Ili kumakinika katika rejista, mara nyingi mtafsiri huhitajika kuwa na ufahamu tosha wa jinsi rejista hiyo inavyotumika. Kwa vyovyote vile, hii ni aina ya tafsiri ambayo hupuuza mambo mengi sana yenye umuhimu katika taaluma zima ya tafsiri, huku ikijikita katika msisitizo wa ladha ya kiakademiki pekee.

R.L. Graeme Ritchie, aliyekuwa mkurufunzi na mtafsiri kule Oxbridge, ndiye mwasisi wa aina hii ya tafsiri.

2.3: MAWASILIANO KATIKA TAFSIRI.

Wanafalsafa wa lugha, wanasaikolojia na wanaisimu wanaamini kwa jumla, ya kwamba uamilifu muhimu zaidi wa lugha ni ule wa kufahamisha watu, habari fulani yaani kuwasiliana.

Dhana ya mawasiliano ni pana sana, nayo imeweza kufafanuliwa na wasomi, kwa mitazamo tofauti tofauti, ambayo, licha ya kutofautiana, ina manufaa kwa somo la tafsiri.

Mwanaisimu jamii, Lyons (1977) alidai kwamba dhana ya mawasiliano ilirejelea "...hisia, maoni na dhamira ambazo hupitishwa kwenye ujumbe fulani jinsi zilivyonuiwa na chanzo cha ujumbe (Mw.A)".¹⁷

Naye mwanaleksikografia Wales (1989) aliifafanua dhana ya mawasiliano kwa njia pevu, kama, tukio la ubadilishanaji habari kwa kutumia lugha ya mwanadamu, aidha kimaongezi au kimaandishi. Aliongezea ya kuwa lugha ya mwanadamu ndiyo muhimu zaidi na yenye utata mwingi zaidi katika uwanja wa mawasiliano.¹⁸

Kwa kiasi kikubwa, maelezo ya Wales kuhusu dhana ya mawasiliano yanashabihiana na maelezo yaliyowahi kutolewa kuhusu mfumo mpevu ambao huweza kufahamika kwa mujibu wa nadharia maarufu ya mawasiliano ambayo Shannon na Weaver (1949) waliipendekeza na kuipambanua.

Nadharia hii ya mawasiliano hudai kwamba; ujumbe huwasilishwa kama ishara za lugha zinazotoka kwa chanzo cha ujumbe (Mw.A) na kupitishwa hadi kwa anayepokea ujumbe (hadhira), kupitia kwa sauti zinazotamkwa (au kuandikwa)¹⁰

Kile ambacho huwasilishwa (ujumbe ulio na maana) kinaweza kuwa, ama dhana inayorejelea hali halisi maishani au maongezi yenye dhamira na maana maalumu kwa jamii ambayo hufungamana na utamaduni teule, au dhana zinazohusiana na muktadha na mazingira ya watu fulani, kama ilivyo kawaida katika kazi nyingi za kifasihi.

Mtazamo huu unamaanisha kwamba, kila mara ambapo kitendo cha kuwasiliana hutokea, jambo fulani hupitishwa/huwasilishwa na kwamba hata wakati ambapo watu hawaongei kwa sauti inayosikika, mawasiliano huendelea, kwa sababu dhana ya mawasiliano haijafungika kamwe katika sifa za lugha kimaongezi, bali hudhihirika pia kupitia ishara za mwili.

Wanaohusika katika mawasiliano, kimsingi huwa mzungumzaji (Mw.A) na msikilizaji (hadhira). Bennett (1976) anafafanua zaidi ya kwamba, lengo la mzungumzaji huwa ni kumfahamisha jambo, msikilizaji na wakati mwingine hulenga kumwathiri au kumfanya msikilizaji kutenda jambo fulani baada ya kuelewa ujumbe wa matini na kuubwia akilini.

Maoni hayo yanaonyesha kwamba lugha inapotumiwa katika tafsiri, matarajio huwa ni kutekeleza dhima fulani ambayo aghalabu ni kuwasiliana.

Mwandishi asilia wa matini hubuni akilini mwake ujumbe wenye maana. Ujumbe huo, ambao yeye hudhamiria kuupitisha kwa namna

iliyo mwafaka, sahihi na kamilifu, kwani huko ndiko kuwasiliana. Matarajio ya Mw.A ni kwamba ujumbe huo uweze kupokelewa na kufasiriwa na mpokeaji.

Dhana hii ya mawasiliano katika tafsiri, huegemea zaidi upande wa ujumbe, kuliko kipengele kingine chachote, kwa sababu mtafsiri anatazamiwa/anatarajiwa kumfikishia msomaji wake, ujumbe sahihi ambao aliupata kwenye MA.

Katika tasnifu hii ujumbe tunaourejelea uliandikwa kwa lugha ya kiingereza (MA) na kisha ukatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili (MP) katika diwani Risasi Zianzapo Kuchanua (1975).

Tofauti kidogo na mtazamo wa wanaisimu, wanaoikolojia na wanafalsafa wa lugha, ambao huafikiana kwa jumla kuhusu dhima ya lugha kama chombo cha kuwasilishia habari/ujumbe; wapo wanaisimujamii na wanaelimujamii ambao hutazama mawasiliano kwa misingi ya kuwa, lugha sio tu chombo cha kuwasilishia habari, bali pia ni chombo cha kujengea na kudumishia mahusiano katika jamii za wanadamu, baina ya wanaowasiliana.

Madai yao ni kwamba, lugha ina dhima ya; kusababisha na kuwezesha kuwepo kwa maingiliano baina ya watu wawili au zaidi au baina ya makundi ya watu mbalimbali.

Kwa misingi ya madai hayo, kazi ya tafsiri inaweza kuangaliwa kama zao la maingiliano baina ya kunga, tamaduni na kaida za lugha za jamii mbili tofauti ambazo zinawasiliana. Jamii inayolengwa katika MA ya tasnifu hii ni ile ya eneo la kusini mwa Afrika na baadhi ya visiwa katika bahari ya Atlantiki, na hali jamii inayowasilishiwa ujumbe na MP, ni ya Afrika ya mashariki.

Tunapozingatia tukio la tafsiri na kulihusisha na dhana ya mawasiliano katika mtazamo huu, tunapata uhusiano uliopo baina ya watunzi mbalimbali wa mashairi katika When Bullets Begin To Flower (1972); mtafsiri wa Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) na hadhira inayopokea MP, ambayo ni ya eneo hili la Afrika Mashariki. Uhusiano baina yao wote unaletwa na ujumbe ambao unawasilishwa.

Mtazamo wa kisemiotiki kuhusiana na dhana ya mawasiliano katika tafsiri, vilevile umewahi kutolewa na baadhi ya wasomi kama Basil na Hatim (1990) ambao wamesisitiza ya kuwa matini hujengwa kutokana na mfumo wa ishara ambazo hubeba maana, zinazorejelea dhana fulani.

Maana hizo zinazobebwa katika ishara za maandishi ndizo huwasilishwa kwa hadhira pokezi ambayo hutarajiwa kuzipata maana hizo... na hivyo kusababisha hali ya kuwasiliana.²¹

Wanasema mtafsiri anapaswa kutilia maanani mambo yafuatayo wakati wa kuwasiliana na hadhira yake; (i) aweze kuelewa vyema, uwanja unaohusika katika tukio la mawasiliano, (ii) awatambue walioshiriki na (iii) aweze kufahamu njia iliyo tumiwa kuwasilishia ujumbe katika tukio la mawasiliano.

Mambo haya ni muhimu nayo yanaweza kudhihirika kwa njia rahisi tunaporejelea kazi tunayoichanganua ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), ambayo uwanja wake ni wa fasihi, na hasa mashairi ya kuzindushi, walioshiriki wakiwa ni mtafsiri na wasomaji wake, kwani ujumbe wa MA unawafikia wasomaji kupitia kwa mtafsiri. Njia iliyotumiwa kuwasikishia ujumbe ni lugha ya kiswahili, katika hali ya maandishi.

Maoni ya Sebeok (1986) yanakaribiana na ya Hatim na Basil (1990), anapodai ya kuwa "...matendo ya kiisimu ya mzungumzaji (mwandishi) anayeshiriki katika kitendo cha mawasiliano ndiyo huzalisha muktadha unaouzunguka usemi..."²²

Madai yake yanaonyesha kwamba mawasiliano hutokea kwa ajili ya ule uwezo wa msemaji/mwandishi (mtafsiri) wa kutekeleza kitendo fulani cha kiisimu kama vile kuweka pamoja maneno yanayoweza kuleta maana katika kipashio kama vile sentensi au mshororo.

Sebeok alifafanua zaidi kwamba matini yaliyoandikwa ni (kama) rekodi ya ishara za kimawasiliano baina ya mwandishi (mtafsiri) na wasomaji (HP) ...yanayopitishwa wakati wote katika tukio la kuwasiliana huwa ni ishara hizo zinazobeba maana.

Mtazamo wa kisemiotiki katika mawasiliano huchukulia maongezi/maandishi kama kitendo, jinsi alivyoelezea Austin (1962) yule mwanafalsafa wa lugha, aliyeendeleza uchunguzi wa lugha katika viwango vya usemi, vilivyozidi sentensi/mshororo.

Katika tafsiri, mtazamo wa dhana ya mawasiliano kwa misingi ya semiotiki, bado haijaleweka vyema kwa sababu ya ugumu wa kufasiri na kuoanisha dhana za ishara na viashiriwa.

Mbali na upungufu huo katika mtazamo wa mawasiliano kisemiotiki, katika tafsiri, miaka ya hivi karibuni imeshuhudia kujitokeza kwa wasomi wachache kama vile Louw (1984), ambao wameupea mtazamo huu, msukumo.

Louw, alielezea ya kuwa mambo ya kuzingatiwa na watafsiri, ni kama: (i) lugha huwa mfumo wa ishara zinazotumiwa katika uwasilishaji ujumbe, (ii) sio tu ishara za lugha ambazo pekee

hushirikishwa katika upitishwaji ujumbe kwenye tukio la mawasiliano.

Kunazo vilevile ishara zilizo nje ya lugha ambazo hujumuishwa na sifa za viziada lugha vinginevyo. Hizi sifa ziada ambazo si sehemu ya mfumo wa lugha, hata hivyo hutekeleza jukumu muhimu katika uwasilishwaji wa ujumbe. Baadhi ya sifa hizo huhusiana na maswala kama; hali ya matini kiumbo, mpangilio wa sentensi na aya za matini, kipengele cha kiimbo katika matini, usitaji wakati wa kusema, maendelezo ya maneno, uakifishaji katika matini, miundo ya matini, k.m. iwapo ni ushairi, nathari n.k. Pamoja na hayo, maswala ya muktadha, mazingira ya matini na utamaduni wa lugha ya matini huzingatiwa.

Ishara zote, zilizo ndani na nje ya mfumo wa lugha, bila shaka huchangia katika kueleweka kwa ujumbe ambao mtafsiri anauwasilisha kupitia kwa maneno yake (ishara zake).

Matini yaliyohifadhiwa kimaandishi hutoa nafasi kubwa ambao kwao ishara-ziada lugha (extralinguistic signs) zinaweza kujumuishwa kwenye matini inayotafsiriwa. Njia ya wazi zaidi ya kujumuisha ishara-ziada lugha ni ile ya mwandishi/mtafsiri kuongezea maelezo ya ziada ambayo hufafanua hali ya kimazingira na kimuktadha inayoizunguka tukio la usemaji au uandishi wa maneno, kwa mfano katika When Bullets Begin To Flower (1972:54) kifungu:

...in the proud voice of Langston in the beautiful voice of Gullien...; kinapotafsiriwa katika Risasi Zianzapo Kuchanua (1975:58), kama ifuatavyo;

kwa kauli ya kujivunia ya Langston,

Na sauti nzuri ya mshairi wa Cuba,

Aitwave Gullien.

Inaonekana wazi kupitia kwa sehemu zilizopigiwa mistari ya kwamba mtafsiri aliyaongeza hayo maelezo ili HP, iweze kuelewa vyema kwamba yule Gullien alikuwa mshairi, tena wa kutoka Cuba.

Kufuatana na mtazamo kama huo wa Louw, lugha huchukuliwa tu kama sehemu ya mfumo mkubwa zaidi wa ishara nyingi zinazoingiliana na kubainika pamoja wakati wa kupitisha maana inayolengwa na mwandishi asilia wa matini.

Huyo mtaalamu anasisitiza kwamba, mawasiliano katika matini inayotafsiriwa, hayana budi kuvuka mipaka ya usemi wa kawaida na kuweza kuhusishwa na vipengele vilivyo juu zaidi kuliko sintaksia au semantiki.

Kauli hiyo inamaanisha kwamba, matumizi ya lugha huhusisha, zaidi ya maneno matupu, na badala yake, lugha, hasa katika mawasiliano, huhusu matendo-tamshi (speech acts) ambayo huingiliana na lugha kiutendaji. Kwa mfano mashairi mengi katika diwani Risasi Zianzapu Kuchanua (1975) ni matendo kauli yenye kuwazindua na kuwahamasisha wanaozisoma ili wapiganie uhuru wao.

Uchunguzi umeonyesha ya kuwa ishara nyingi sana zipo katika lugha, hivyo basi inawezekana kwamba tamko katika usemi, likawa na maana zaidi ya ile moja tambuzi inayofahamika kwa kila mtu. Vivyo hivyo, ufasiri wa maana, kwa vyovyote vile huambatanishwa na vipengele vingine vya isimuamali/pragmatiki katika lugha yoyote inayohusishwa katika mawasiliano.

Uchunguzi wetu umeonyesha ya kwamba tukio lolote la kimawasiliano, hushirikishwa na mfumo tata, katika viwango vya kategoria mbalimbali za lugha kama vile; kiwango cha fonolojia, morfolojia, leksia, sintaksia, urejeleshi, muktadha, maana tambuzi, maana ziada n.k.

Si ajabu kwamba matatizo ya tafsiri pia hudhihirika kulingana na hivyo viwango mbalimbali kama ambavyo tutaelezea katika sura za 3 na 4. Viwango vyote ni muhimu kwa mawasiliano katika tafsiri.

Mawasiliano baina ya mtafsiri na hadhira yake, yanaweza kutatizika, kutokana na sababu mbili za kimsingi ambazo Makay (1973) aliziainisha kama; (i) ugumu wa (mtafsiri) kujiepusha na mawasiliano yasiyo toshelevu, ambayo kwayo anaweza kuwakanganya wapokeaji wa yale anayoyawasilisha/ujumbe.

Tatizo hili tumelizingatia katika sura ya 4, sehemu ya 2. (ii) Pili ni kwamba, kila mara tunapotumia lugha, mawasiliano huwepo. Maana katika tukio lolote la mawasiliano hutegemea fasiri ya mpokeaji ujumbe ambaye wakati mwingine anaweza kutoa fasiri isiyo na maana aliyoidhamiria mwandishi asilia wa matini. Jambo hili pia huzua tatizo.

Kwa hali yoyote ile, uzingativu wa maana halisi ya ujumbe unaotafsiriwa ni muhimu sana katika kufanikisha au kuvuruga mawasiliano.

Dhana ya mawasiliano pia imewahi kufungamanishwa na matukio ya upitishaji ujumbe, kwa nia hasa ya kuzua athari juu ya mpokeaji. Katika somo la tafsiri, ujumbe unaweza kuwa wa kisiasa, kiusomi, kidini, kiuhamasisho, n.k.

}
Kauli mojawapo katika mtazamo huu ni kwamba kabla ya mawasiliano kuweza kuwa na athari yoyote ile juu ya msomaji/msikilizaji wa kazi ya tafsiri; sharti ujumbe kwenye matini, uzue maana inayoeleweka na mpokeaji, nao kwao mpokeaji huyo ataweza kuathirika.

Kiunzi hiki cha maana ya ujumbe, sharti mpokeaji akizingatie kwa mapana na undani wake wote, kama ambavyo, kwa mfano, baadhi ya mafungu ya When Bullets Begin To Flower (1972) yenye maana fiche, yamefichuliwa na mtafsiri wa Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), kulingana na uelewaji wake wa maana ya ujumbe asilia. Vivyo hivyo mpokeaji anatakiwa kuelewa maana ya mafungu ya MP.

Wananadharia, Nida na Taber (1969), Beekman na Callow (1974) na Larson (1984) ni miongoni mwa wengi katika kundi linalosisitiza kipengele cha maana katika mawasiliano kwa ajili ya kutaka kuboresha mawasiliano ya ujumbe kutoka kwa MA hadi kwa MP. Wanasema ya kuwa maana sahihi ya ujumbe unaowasilishwa, hauna budi kuambatana vilevile na maswala ya ukweli na uaminifu kwa MA.

Kanuni ya ufaaji wa ujumbe unaowasilishwa, imedaiwa kuwa yenye uwezo wa kumsaidia mtafsiri kufikia mawasiliano mazuri.

Wilson na Sperber (1981, 85, 86) na Dye (1988), Walielezea kanuni ya ufaaji kuwa; ufahamu uliopo akilini mwa anayepokea ujumbe na ambayo humwezesha kuchukua hatua za kisaikolojia wakati anaposoma na kufasiri ujumbe unaowasilishwa kwake kupitia matini iliyotafsiriwa.

Ufaaji wa matini fulani kwa mpokeaji, hulingana na jinsi ambavyo anauhusisha ujumbe unaowasilishwa, na hali yake ya kuelewa

na kufasiri maana pamoja na muktadha anaoufahamu. Bila ya uhusisho kama huo mpokeaji wa MP, huenda asiwasiliane na mtafsiri kwa njia inayofaa.

Ni dhahiri kwamba, mtafsiri anaporuhusu kanuni ya ufaaji katika mawasiliano, anampa mpokeaji wa MP nafasi ya kuweza kupokea ujumbe wa MA, bila ya kutatizika kwingi; naye mtafsiri kwa upande wake, huweza kubadilisha anayowasilisha kutoka MA hadi katika muktadha wa MP.

Huu muktadha tunaourejelea,, ni ule ambao hujengeka katika saikolojia ya mpokeaji ujumbe, kufuatana na jumla ya maarifa na ujuzi aliyo nao kuhusiana na yanayowasilishwa, vilevile ujuzi kutokana na kumbukumbu na ufahamu ulio akilini mwake kijumla.

Ikiwa mtafsiri anataka kufanikiwa katika mawasiliano yake, hana budi kuelezea mambo kwa namna ambayo itamsaidia mpokeaji ujumbe/msomaji tafsiri, kung'amua maswala yote yanayouzunguka muktadha anaotazamiwa kuupata kwenye MP. Naye mpokeaji ujumbe anatarajiwa katika mawazo yake aufungamanishe huo muktadha na ujumbe aliopokezwa kwenye MP.²³

Inawezekana ya kwamba mpokeaji ujumbe wa tafsiri, anapochanganyikiwa na ujumbe unaowasilishwa kwake au anapona, kwamba ujumbe hauna maana na faida yoyote kwake, anaweza kuamua kukatiza mawasiliano baina yake na mtafsiri. Hii inamaana kwamba katika mawasiliano, mtafsiri hatajikani kamwe kupuuza hadhira pokezi ya matini anayoitafsiri, lau sivyo, ujumbe anaouwasilisha unaweza kukiuka kaifa ya ufaaji kwa hadhira lengwa.

Mtafsiri anaweza kuliepuka tatizo hili kwa kutilia maanani tofauti za kimsingi baina ya hadhira za lugha zote mbili (za MA na MP).

Wananadharia maarufu wa tafsiri kama Nida (1964), Nida na Taber (1969), de Waard na Nida (1986), Beekman na Callow (1974), Barnwell (1980) na Larson (1984) ni baadhi ya wale ambao wamezungunzia mwegemeo wa dhana ya mawasiliano unaofungamana zaidi na maswala ya kiisimu katika tafsiri. Kauli za kimsingi za mtazamo huu zimejengeka zikizunguka vipengele vitatu: chanzo cha ujumbe (Mw.A)-ujumbe unaopitishwa - mpokeaji (hadhira pokezi).

Mtazamo huu unapunguza kimaksudi hali ya mtafsiri kujikita zaidi katika mfumo maalum wa kitamaduni au katika maswala ya kimuktadha kwenye MA au MP. Badala yake, jambo lililo muhimu zaidi ni ufikishwaji ujumbe wenye maana sahihi kwa mpokeaji.

Hata hivyo tungependa kutahadharisha ya kwamba kutohusisha kabisa maswala ya kimuktadha katika tukio la mawasiliano kunaweza kuzua matatizo mengi zaidi ya kimawasiliano katika matini zinazotafsiriwa kuliko vile ambavyo wanachukulia.

Ni mwafaka kuzingatia ya kwamba licha ya maoni hayo, msomi wa tafsiri Nida (1964) alikuwa ameonyesha kutoridhika na mwegemeo huo ulioelekea kuhusika tu na vipengele vya kiisimu katika mawasiliano kwenye matini inayotafsiriwa. Ukweli ni kwamba vipengele vyote (vya isimu, muktadha n.k.) ni muhimu kwa ajili ya mawasiliano katika tafsiri.

Ili, kupima, iwapo mawasiliano yametekelezwa kwa njia iliyofanikiwa, de Beaugrande na Dressler (1981) walipendekeza

kwamba yafuatayo yaweze kudhihirika katika M.P. (i) ushikamano (ii) muwala (iii) dhamira inayokusudiwa (iv) ukubalifu wa ujumbe (v) ufahamishaji wa ujumbe (vi) ujumbe uwe wenye kuzingatia hali kiwakati na (vii) kudhihirisha ya kwamba umeoanisha vipengele kutoka MA na MP (intertextuality). Vipengele vyote ni muhimu kwa minajili ya mawasiliano.

Tunakubaliana na madai ya Gutt (1991) kwamba "...wazo muhimu ya nadharia ya ufaaji katika mawasiliano ni kwamba mawasiliano baina ya wanadamu huzua tarajio la kupitishwa kwa ujumbe kwa namna inayofaa zaidi; kwa upande wa mpokeaji ujumbe..." 24

Hata hivyo hatukubaliani na madai yake kwamba nadharia ya ufaaji mradi imezingatiwa vyema huwa na uwezo mkamilifu wa kukidhi majukumu ya nadharia nyinginezo za tafsiri.

Ukweli ni kwamba kanuni za nadharia moja pekee haziwezi kutosheleza na kuondoa kabisa haja ya kuwa na miongozo ya nadharia elekevu nyinginezo za tafsiri na wala haziwezi kusuluhisha matatizo yote kuhusiana na mawasiliano katika tafsiri. Ilivyo ni kwamba kila mojawapo ya miongozo/nadharia husheheni pungufu za aina tofauti tofauti ambazo zinaweza kusawazishwa kwa njia ya kuoanisha kanuni za nadharia nyingi tofauti.

2.4: MUKTADHA KATIKA TAFSIRI

Muktadha ni istilahi ambayo imewahi kuelezwa na wataalamu wengi kama; vipengele maalum vinavyoathiri kipashio fulani kutokana na kuwa na uhusiano au kutokea karibu nacho kwa namna fulani.

Wengine wameielezea muktadha kama mazingira au hali inayoathiri maana ya neno, sentensi au sehemu ya kazi ya fasihi (au matini yoyote yale).²⁵

Mfano wa maana hii ya muktadha, unaweza kuonekana katika matumizi ya methali, ambapo ni muhali kuzingatia kwa undani jinsi ambavyo vipashio vyake vimetumika, na namna ambavyo fasiri yake hufikiwa.

Malinowski ni miongoni mwa wanaanthropolojia na wanalugha walioanzisha ushirikishwaji wa vipengele vya muktadha wa hali za matini na vile vya utamaduni wa jamii zinazohusika katika somo la lugha. Jambo hili kufikia sasa linatekelezwa sana katika taaluma ya tafsiri.

Kichocheo cha mtazamo aliouchukua Malinowski kilikuwa ni tukio ambapo alijipata ametatizika wakati wa kufasiri na kutafsiri dhana za kitamaduni za jamii ya watu wa kisiwa cha Tribriand, kutoka lugha ya huko - kimelanesia hadi kiingereza, lugha ya hadhira aliyoilenga.²⁶

Jaribio lake la kutumia tafsiri huru liliambulia patupu kwa vile dhana hizo zilizojikita katika utamaduni wa watu wa Tribriand hazikupitishwa kikamilifu kwa HP.

Maamuzi yake hatimaye yalikuwa ni kutumia mtindo wa kutafsiri ambao ungemwezasha kushirikisha dhana hizo za kitamaduni, kwa njia ya ufafanuzi wa vipashio mbalimbali.

Fafanuzi alizoambatanisha na vipashio hivyo vya lugha, zikawa kielelezo cha uhusishwaji wa sifa za kimuktadha katika matini. Malinowski alitaja sifa zote na vipengele vyote hivyo kwa pamoja

kama muktadha wa hali (situational context), ambayo kwa maoni yake ulihusisha vipengele vyote vya dhana za kitamaduni vilivyokizunguka chanzo cha ujumbe (mwandishi) wa matini na pia hali zilizowazunguka wapokeaji wa huo ujumbe.

Muktadha wa kijamii na utamaduni wa washiriki katika tukio la kutafsiri, ni muhimu wakati wa kufasiriwa kwa ujumbe unaopitishwa, kwani hurejelea sifa kama zile ambazo ni teule katika jamii fulani na pia zile za kijumla ambazo hubainika miongoni mwa watu wengi ulimwenguni kama vile matumizi ya tauria/tasfida kwa minajili ya kuzima ukali au uchafu wa baadhi ya maneno.

Firth, vilevile alijitokeza na kauli zilizojengwa kwa misingi iliyokaribiana na ile ya Malinowski. Alikariri umuhimu wa muktadha na utamaduni kwa mwanalugha yeyote, yule; akiwemo mtafsiri, ambaye alitaka kupata maana kamilifu ya tamko au kifungu fulani cha kimaandishi.

Kwa mfano muktadha wa matini yetu ya asili, When Bullets Begin To Flower (1972) umejikita katika jamii za watu ambao waliishi katika mataifa yaliyotawaliwa na wareno katika kipindi cha ukoloni nayo ni tafauti na muktadha wa jamii ya MP.

Maoni ya Firth na Malinowski yaliendelea kupata umaarufu na upambanuzi zaidi miongoni mwa wataalamu wengi wa tafsiri. Lengo lao, katika kusesitiza dhana za kimazingira na kitamaduni ambazo kwa pamoja hujenga muktadha, limekuwa ni kuboresha uelewekaji wa matini wanazozitafsiri.

Madai ya Catford (1965) yalikuwa kwamba muktadha, ni kama kiunganishi kinachopatanisha maswala yanayoegemea kwenye isimu,

sarufi, leksia n.k., na maswala yanayogusia hali nzima ya matini yoyote yaliyotafsiriwa.

Alichomaanisha ni kwamba tafsiri na vipengele vyake tofauti tofauti haiwezi kujitenga kabisa kabisa na elementi za muktadha.

Uchunguzi wetu umeonyesha kwamba elementi za kihali ambazo hutokea kupitia muktadha huchangia sana katika kujenga mahusiano baina ya vipengele na vipashio mbali mbali vinavyotumika katika lugha, hasa katika tafsiri.

Usemi wowote ule uwe ni katika umbo la kimaongezi au kimaandishi, ni tukio mojawapo katika hali maalum ya kijamii. Hii ndiyo sababu ambayo hufanya maneno yanayotumika katika kifungu fulani kupewa maana moja au nyingine, kwa mujibu wa mahali pa kusemwa, sababu za kusemwa na jinsi ya kufasiriwa kwayo.

Hayo yote huzingatiwa kimuktadha, kulingana na mfumo wa utekelezaji unaojikita katika lugha teule. Katika tafsiri, mfumo huo hutarajiwa kujikita katika lugha pokezi. Lugha pokezi ya matini yetu, Rasasi Zianzapo Kuchanua (1975) ni kiswahili, nao una mfumo wake ulio tofauti na ule wa kiingereza ambayo ni lugha ya matini yetu asilia When Bullets Begin To Flower (1972).

Mtazamo wa dhana za kimuktadha, huzingatia kauli kwamba maana katika kazi inayotafsiriwa, haifungiwi tu kwenye matukio ya maongezi na maandishi ya lugha, bali pia huhusishwa na ishara zinginezo ambazo huwa aidha za kimaongezi au zisizo za kimaongezi, ambazo hata hivyo ni sehemu muhimu sana ya maana jumla ya usemi. Mtafsiri hafai kuzipuuza kamwe.

Inavyofahamika ni kwamba kimuktadha, maana haiwezi kuhamishwa kutoka matini asilia hadi matini pokezi bila ya kubadilisha umbo la lugha, kwa sababu kila lugha ina upekee wake kiumbo. Mtafsiri anapolitimize sharti hilo, muktadha wa matini yake hupokelewa kwa namna inayofaa, katika umbo la lugha pokezi.

Kulingana na maoni ya Wendland (1987) na Shaw (1988), watafsiri hawana budi kutilia maanani ujumuishi wa mielemeo ya kiantropolojia, wakiihusisha na kanuni za kutafsiri; matokeo huwa matini pokezi yenye kufaa kwa vile itawasiliana na hadhira lengwa, mbali na kupitisha maana ya ujumbe wa matini asilia katika muundo unaoeleweka na kukubalika na wapokeaji.

Baadhi ya wasomi wa taaluma ya tafsiri wamedai kwamba tafsiri nzuri ya maana, kwa vyovyote vile ni sawa na utekelezaji wa hatua zinazofungamana na utamaduni wa lugha zinazoshirikishwa katika tafsiri. Inavyodhihirika ni kwamba muktadha wa matini huhusishwa katika tafsiri kwa minajili ya kufafanua maana ya ujumbe unaowasilishwa.

Brown na Yule (1983:25) waliongezea ya kuwa, mchanganuzi usemi, kama vile mtafsiri, hutazama data yake (matini asilia) kama rekodi yenye maana ambayo kwayo lugha imetumiwa na mwandishi, kama chombo cha kimawasiliano, katika muktadha fulani, ili kuzua matini inayotimize dhamira yake (Mw.A).

Kupitia baadhi ya elementi za kipragmatiki, mtafsiri anaweza kutimize matarajio ya matini bora. Pragmatiki hutilia maanani muktadha katika matini ambao umezalisha vipengele vya usemi kama, virejeshi, pronouni, sentensi, aya n.k.

Pragmatiki ina mbinu za kuhusisha vipengele vya sentensi kiusilisila ama kiolezo faridi. Huu uwezo wa kuhusisha amali ziada za vipengele vya matini ni muhali sana katika kuelewa dhana ya muktadha katika tafsiri.

Pierce (1931), msomi wa dhana ya semiotiki aliyeimarisha mawazo sawa na yale ya de Saussure, alifafanua muktadha kwa misingi ya kisemi otiki, kwa dai kwamba maishani mwa binadamu yeyote, akiwemo mtafsiri katika ulimwengu wake, amezungukwa na ishara zingine nyingi, mbali na zile za lugha ambazo watu wengi sana, kimakosa walichukulia kuwa ndizo zenye umuhimu.

Kwa vile uhusiano uliopo baina ya ishara ya lugha na kiashiriwa huwa dhahania, fasiri ya neno (ishara) hutegemea mahusiano mengine ya kimuktadha katika matini.

Maana ya kiashiria fulani, hutegemea maswala kama vile mazingira ya kijamii, kaida za wanalugha kitamaduni na kauli nyinginezo.

Kwa mfano katika mazingira ya kisiasa; ishara, ndugu inaweza kufasiriwa kwa maana ya mshirika, na katika misingi ya utamaduni wa kijamii; ndugu, inaweza kumaanisha mtu uliyezaliwa naye tumbo moja, au mtoto wa ndugu wa baba au dada za mamake mtu n.k.


Katika taaluma ya tafsiri, tunaweza kuangalia mahusiano ya vipengele vya matini ambavyo huumba muktadha, katika viwango vya maneno, virai, vishazi, sentensi, aya/beti, sura n.k.

Uhusiano wa elementi hizo, kama tulivyotaja, huwa ama kiusilasila au kiolezo faridi.

Massamba (1990), ameelezea uhusiano wa usilasila kama, ule uliopo baina ya elementi za lugha au vipashio tungo, kiulalo kama ulio baina ya sentensi moja na nyingine.²⁷ Nao uhusiano wa kiuolezofaridi ni ule wa ruwaza ya mpangilio wa vipengele vya kiisimu, yenye kuonyesha uhusiano wima baina ya kipashio kimoja na vipashio vingine katika muktadha maalum,²⁸ kwa mfano baina ya aya na aya au sura na sura n.k.

Tunaweza kuonyesha mahusiano hayo, kimchoro kama ifuatavyo:


Uhusiano wa kiusilasila,



Kipashio (neni) A, kwenye matini, lina uhusiano na B, B na C, C na D, D n.k., katika ujengaji wa maana timilifu ya sentensi, kirai, kishazi, mshororo n.K. Uhusiano baina ya hivyo vipengele ni wa kimuktadha, nao ndio ambao kwao maana ya kifungu huzalika.

Tulivyoelezea ni kwamba, muktadha utafafanuka vyema kwa mtafsiri anayezingatia mahusiano haya baina ya vipashio vya lugha.

Uhusiano wa kiolezo faridi nao unaweza kuonyeshwa kimchoro kama ifuatavyo:



Vipashio 1,2,3,4,5 ... n.k.,
vinaweza kuwa sentensi,
vishazi, aya beti au sura
zinazofuatana au
kutanguliana katika matini.

Hivyo vipashio vyote
vinahusiana katika kujenga
muktadha wa kazi/matini
inayotafsiriwa.

K.M. katika kifungu kifuatacho kutoka Risasi Zianzapo Kuchanua
(1975:85), Nipo hapa, Mussunda.

Rafiki yangu, nipo hapa.

Uhusiano baina ya mshororo wa kwanza na wa pili ndio
unaotuwezesha kufahamu ya kwamba yule Mussunda anayetajwa ndiye
rafiki wa msemaji, na kwamba mahali alipokuwa ndipo angalipo.
Iwapo tungechukulia kwamba kila mshororo unajisimamia kivyake, basi
hatungeweza kamwe kuhusisha jina Mussunda na dhana ya urafiki, au
kipashio chochote kile na kingine.

Ili kutimiza mahitaji ya kimuktadha katika tafsiri, mambo
yafuatayo yanapasa kuzingatiwa na mtafsiri, kwa mujibu wa Bateman
(1995), (i) mtafsiri afanye uchanganuzi toshelevu wa MA
(ii) azingatie kwa upana na undani, elementi za kimuktadha

zinazomwezesha kufikia maana halisi ya ujumbe anaouwasilisha,
(iii) azingatie muundo wa kipragmatiki baina ya vipashio kwenye
matini anayoitafsiri.

Kwa njia hiyo matini inayotafsiriwa, huweza kuwasilishwa kama
kipengee kikubwa cha semantiki (maana), chenye muwala na mshikamano
mzuri.

2.4.1: MATATIZO YANAYOHUSIANA NA MUKTADHA

Tatizo la kwanza kuhusiana na muktadha ni lile la mtafsiri
kuongeza maelezo mengi kupita kiasi katika MP. Jambo hili
hulinyima uhalisi MP na pia kuwakosesha wapokeaji wa MP, ladha na
mguso ambao mwandishi asilia alinulia kuipitisha.

Anavyopendekeza Lars Lode (1984:101-108) ni kwamba ujumbe wa
ziada unaofungamana na muktadha ufungiwe kwenye mabano katika MP,
ili kuyafanya hayo matini kueleweka vyema zaidi.

Upungufu wa hatua kama hiyo ya kuyafungia maelezo ya
kimuktadha katika mabano ni kwamba umbo la MP hukengeushwa, huku
mvuto wake pia ukiathirika kwa sababu wasomaji hutatizika katika
kuhusisha maelezo hayo na sehemu zingine za matini. Kisaikolojia
wanaweza kuchukulia viziada hivyo kama nyongeza tu na sio sehemu ya
matini yenyewe. Mara nyingi wasomaji huchoshwa na hali hiyo.

Tatizo la pili ni kwamba haiwezekani, mtafsiri kuwasilisha
ujumbe na habari zote kuhusiana na muktadha kikamilifu kwa namna
sawa na ambavyo vipengele hivyo viliwasilishwa kwa hadhira ya lugha
asilia.

Ili tatizo hili lisiwe na athari kubwa sana katika MP, tunapendekeza ya kuwa itafaa zaidi kwa mtafsiri kuteua na kuwasilisha habari na ujumbe wa ziada ambao ni mwafaka zaidi katika kazi inayohusika, ambao usiposhirikishwa, huenda matini tafsiri yasieleweke.

Mchujo wa mambo muhimu na yasiyo muhimu kimuktadha bila shaka yataiboresha tafsiri, ingawaje tahadhari pia lazima ichukuliwe ili uchujwaji wa vipengele vinavyoachwa nje ya matini usipite kiasi, lau sivyo maana ya ujumbe nao utaathirika vibaya.

Tatizo la tatu kuhusiana na muktadha, husababishwa na hali ya mpokeaji ujumbe wa MP; ya kutokuwa na ufahamu wa kutosha, wa baadhi ya dhana za utamaduni na mazingira ya lugha hiyo pokezi. Hali kadhalika hali ya mtafsiri mwenyewe kuzamia na kutekwa zaidi na athari za utamaduni wa jamii yake, husababisha matatizo ya kiufasiri.

Ni wazi kwamba katika hali kama hiyo, mtafsiri atapitisha baadhi ya athari hizo za utamaduni wake mwenyewe, hadi katika matini anayoitaafsiri. Tatizo hili mara nyingi hutokea iwapo mtafsiri hana ujuzi na umahiri wa kaida na vipengele vinginevyo vya lugha pokezi, au iwapo dhana za kitamaduni na za kimazingira zinazodhihirika katika MA, hazijulikani kabisa kwa mtafsiri. Kwa mfano nyumba za waeskimo, zinazoitwa 'igloo', ni dhana isiyoweza kutafsirika kwa njia rahisi katika muktadha wa kiafrika, na hasa ule wa lugha ya Kiswahili, kwa vile nyumba zinazojengwa na waswahili hazifanani kabisa na hizo ambazo waeskimo. hujenga katika sehemu za barafu kule Ulaya kaskazini.

1

Ni wajibu wa mtafsiri kufumbua utata wowote kwenye matini anayoitafsiri, ambao unaweza kukinza upitishwaji mzuri wa maelezo ya kimutadha katika MP.

2.5: DHANA YA MAANA KATIKA TAFSIRI

Maana ni dhana ya kimsingi na yenye umuhimu mkubwa katika lugha ya binadamu. Dhana hii inahusiana na matukio ya kuwasiliana na kuingiliana miongoni mwa wanadamu wote.

Dhana ya maana imechunguzwa kwa miaka mingi sana, tokea enzi za urasimu mkongwe. Chunguzi nyingi, zimekuwa zikihusisha dhana hii na taaluma mbalimbali.

Sisi tunaitazama kupitia taaluma ya tafsiri kwa vile tungependa kuonyesha nafasi ambayo huchukuliwa na maana katika tafsiri na hali kadhalika kubainisha vipengele vya dhana ya maana vinavyopasa kuzingatiwa na mtafsiri wa matini.

Maana sio dhana nyepesi kueleweka katika somo la tafsiri, ikilinganishwa na dhana nyinginezo. Kuelezea na kufafanua maana katika njia wazi na ya kuridhisha ni tatizo kubwa kwa watafsiri na wataalamu wengi.

Sababu zinazosababisha kutoeleweka na kutofafanuka kwa maana ni kwamba uchanganuzi wa kiisimu, ulilipuuza kipengele cha maana, katika lugha, kwa muda mrefu sana.

Kinyume na hivyo, uchunguzi wa vipengele vya kategoria zingine za lugha kama fonolojia, morfolojia na sintaksia, ulimarishwa sana. Pamoja na hayo, maana vilevile huwa sio rahisi kueleweka kwa kuwa

ni kipengele chenye udhahania mwingi sana katika lugha.

Katika historia ya somo la semantiki, kumekuwa mitazamo mitatu ambayo Crystal (1987:100-101) amelezea kama ifuatavyo;

Kwaza, ni mtazamo ambao unahusishwa na dai kwamba maneno katika matini hutaja au hurejelea vitu. Unaweza kuonyeshwa hivi, kimchoro:

Maneno \longrightarrow vitu²⁹

Huu mtazamo ndio wa awali zaidi, nao ulielezwa hata na Warasimi wakongwe kama Plato katika kitabu chake Crytvlus.

Mtazamo wenyewe ulitokana na hali ambapo maneno katika lugha yalitumika kutajia vitu k.v. miji, watu, mahali, milima, mimea, mito n.k.

Hata hivyo, udhaifu katika mtazamo huu ni kwamba hautilii maanani kwamba sio kila neno katika lugha linaweza kuhusishwa moja kwa moja na kitu kinachoashiriwa. Kwa hivyo kauli ya kwamba neno linataja kitu haidhihiriki. Vilevile katika hali kama hiyo, uhusiano baina ya kitajwa na neno la kutajia kitu, huwa ni dhahanifu tu, k.m. neno mti linalotumika kurejelea mmea wa aina fulani, ulio na mizizi, shina na matawi, ni kiashiria dhahanifu ambacho kingeweza hata kurejelea au kutumika kutajia kitu kingine tofauti k.v. mtu.

Mtazamo wa pili, ulipinga madai ya kuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja baina ya maneno na vitu. Huu mtazamo ulipambanuliwa na wananadharia wa semantiki kama Ogden na Richards (1923:99).

Wao walidai kwamba uhusiano baina ya maneno na vitu uliweza tu

kuelezewa kwa kuhusisha kila neno na dhana, akilini mwa watumiaji lugha.


Dhana iliyo akilini ndiyo ambayo ilirejelea kile ambacho kilitajwa, kupitia kwa neno, na wala sio neno lenyewe kurejelea kitu chenyewe.

Kimchoro madai hayo yalifupishwa hivi;

Neno —————> Dhana —————> Kitu³⁰

Walipoufafanua mtazamo huu zaidi, Ogden na Richards (1923) walijitokeza na kile walichokiita, pembe tatu ya kisemantiki.

Kimchoro mawazo yao yalifupishwa hivi:



Mbali na kwamba, mtazamo huu ulirekebisha udhaifu wa ule mtazamo wa kwanza, ungali na udhaifu vilevile.

Walioushikilia mtazamo huu wa pili walikosa kuzingatia kwamba baadhi ya dhana zinazopatikana katika lugha huwa hazirejelei kitu kinachoweza kuonekana au kuguzwa. Kwa mfano maneno, mapenzi au wakati, ni fikra dhahanifu. Vilevile fasiri ya maana inayohusishwa nazo hutofautiana miongoni mwa watu tofauti, kulingana na vile ambavyo wanayatazama hayo maneno.

Udhahania wa maneno ni mgumu kufafanua, kwa hivyo hapana vigezo toshelezi vya kutegemewa ili kuhakikisha ya kwamba picha inayojengeka akilini mwa mtumiaji lugha ndiyo fasiri sahihi ya

kiashiriwa ambacho neno au kiashiria hukisimamia/hukiwakilisha.

Tatizo la aina hii hudhihirika katika tukio la tafsiri wakati ambapo maana ya kipashio inapewa fasiri tofauti na mtafsiri au pia na mpokeaji. Maana hiyo inaweza kuwa tofauti au kinyume na alivyomaanisha mwandishi asilia wa matini.

Mtazamo wa tatu, ulijikita katika mapendekezo ya Bloomfield (1933), ambayo yalichukulia dhana ya maana kama kitu ambacho kiliweza kupatikana tu kwa kuzingatia hali ambapo msemaji (r) alichochewa na mambo aliyotaka kuyasema (S), kisha anaposema, huo usemi wake (s) husababisha itikio au jibu (R).

Madai yake yalifupishwa kama ifuatavyo:

S r s R³²

(Maelezo zaidi yametolewa katika tanbihi)

Bloomfield, aliongezea ya kwamba washiriki katika matumizi ya lugha waliweza kupata maana ya r s baada ya kuelewa matukio yaliyojumuiika na kitendo cha usemaji wenyewe.

Udhaifu wa mtazamo huu ni kwamba, mara nyingi inapozingatwa na mtafsiri, huwa sio rahisi kwake kutambua sifa za ufaaji wa kichocheo na itikio/jibu, hasa katika matini ambapo matukio yanayohusishwa na usemi, hayabainiki waziwazi.

Kwa mfano hisia kama vile; furaha, kilio, huzuni, mahaba, chuki n.k., mara nyingi hayawezi kuelezewa kwa njia moja maalum kwa vile zinatokana na udhahania, ulio akilini mwa watu.

Kufuatana na pungufu ambazo huonekana katika kila moja ya mitazamo hiyo mitatu ya dhana ya maana, tungependa kushauri ya kuwa

mtafsiri wa kazi yoyote ile anapaswa kujiepusha na hali ya kujikita kabisa, katika mojawapo ya mitazamo hiyo wakati anapofasiri maana ya matini anayoishughulikia.

Hatua hiyo ya kutoegemea mtazamo mmoja pekee, huweza kumsaidia mtafsiri dhidi ya kupitisha maana potofu ambayo mwandishi wa MA hakuidhamiria.

Ili kupitisha ujumbe sahihi kwenye matini kwa kuzingatia dhana ya maana, mtafsiri hana budi kujaribu kuzalisha upya sentensi na vifungu vya MA katika lugha ya MP, ili maana sawa na ile ya MA iwafikie wapokeaji.

Licha ya kwamba wakati mwingine, mtafsiri hulazimika kuhusisha dhana ya maana na vipengele vinginevyo ndani na nje ya lugha kulingana na ujuzi na tajriba yake maishani; ni mwafaka kufahamu ya kwamba neno, sentensi au kifungu chochote kile katika usemi kinaweza kuwa na maana tambuzi na hali kadhalika maana ya ziada.

Hadi kufikia sasa, tatizo kubwa linalowakabili wanasemantiki ni la kuelezea maana ya dhana maana. Baadhi yao ambao wamejaribu kufafanua dhana yenyewe katika miaka ya hivi karibuni wamefikia hatua ya kugawa maelezo yaliyowahi kutolewa na wanasemantiki katika makundi saba makuu ambayo ni ya kijumla sana. Makundi yenyewe yanalingana na matumizi ya maneno pamoja na athari za vipashio vinavyobeba maana, katika maongezi au maandishi.

Makundi hayo ni: (i) Maana bwiwa/dhahanifu, ambayo kwayo, taswira ya kidhahania huhusishwa na kitu halisi au tukio fulani maishani.

Mtu yeyote anayezaliwa katika mazingira fulani ya lugha hukua

na kuibwia akilini aina hii ya maana.

Aina hii ya maana ndiyo msingi wa mawazo waliyonayo watu kuhusu dhana, vitu na hali mbalimbali katika jamii. Kila mtafsiri huzaliwa na kukua akiibwia aina hii ya maana, kulingana na tajriba zake maishani.

(ii) Pili ni, Maana kimatilaba/ziada, ambayo hujumulisha maana zote ambazo kirejelewa hupewa na watumiaji lugha au maana zote ambazo dhana fulani hupewa ama kuhusishwa nayo. Maana hii hufuatana na matarajio pamoja na itikadi za kijamii, jinsi ambavyo kirejelewa chenyewe huchukuliwa kisaikolojia n.k.

Mara kwa mara, maana ziada, huongezwa katika MP ili kudhihirisha hisia maalum, kwa mujibu wa Massamba (1990:15).

(iii) Tatu ni Maana kimtindo, ambayo hudhihirika kulingana na jinsi ambavyo lugha ya matini hutumiwa na mwandishi katika muktadha maalum na kwa njia ya kipekee.

Mikondo ya kimuktadha ambayo kwayo maana kimtindo hujikita ni kama upekee nafsia wa mtumiaji lugha; lahaja ya lugha; wakati wa kutumiwa kwa lugha ya aina fulani na kubadilika kwake kiwakati; msimbo wa lugha, ambayo inaweza kuwa ama ya kimaongezi au kimaandishi; uwanja/rejista ambamo lugha ya matini inatumika, kwa mfano lugha ya sheria, dini, matangazo ya kibiashara, ushairi n.k.; umbo la lugha ya matini, kwa mfano iwapo ni barua, aya, beti n.k.

Hayo yote hukuza na kuendeleza weledi wa mtafsiri kuhusiana na maana kimtindo katika matini anayoitafsiri.

(iv) Nne ni maana kihisia, ambayo huwepo katika lugha, kulingana na hisia na mtazamo wa mtumiaji lugha.

Hisia zenyewe hufungamana na mada inayozingatiwa. Kwa mfano hisia zinaweza kubainika kama dharau, mapenzi, furaha, huzuni, mshangao n.k. mara kwa mara kupitia maneno ya sifa kwenye matini.

(v) Tano ni maana zalishi, ambayo husababishwa na hali ambapo fahiwati (sense) moja ya neno humwelekeza mtafsiri au msomaji katika fahiwati nyingine.

Kwa kawaida, katika vipashio vya matini, maana moja tambuzi huwa imeshika sana, zaidi ya maana zingine zinazohusishwa na vipashio hivyo.

Hivyo basi, maana tambuzi, ndiyo huzua zile maana zingine, kwa mfano neno jogoo humaanisha kuku wa kiume au jimbi ingawa pia inaweza kuhusishwa na maana zifuatazo: shujaa, hodari, mshindi, kiongozi n.k.

Mara nyingi, maneno ambayo ni mwiko kutaja ndiyo huzalisha maana zingine za aina hii, ili kutokiuka kaida za kijamii.

Mtafsiri anapoyaelewa vyema maneno katika MA na matumizi ya lugha katika lugha pokezi ndipo ataweza kuzingatia vyema utambuzi na uzalishi wa maneno katika matimi.

(vi) Sita ni maana husishi-kimantiki, ambayo hutokana na utumiaji wa maneno kwenye ujirani maalum. Katika lugha; baadhi ya maneno hutumika yakifuatwa tu na maneno maalum na wala sio neno lolote lingine.

Kwa mfano, tunapozungumzia uzuri wa umbo la mwanamke, neno la sifa mrembo linaweza kutumiwa kujumulishia hayo maelezo yote.

Kwa upande mwingine, ni nadra sana katika lugha ya Kiswahili sanifu, kusikia mwanamme akielezewa kama mrembo. Vivyo hivyo katika lugha ya Kingereza, ni nadra kusikia 'beautiful man'. Sababu ni kwamba umantiki wa lugha hizo, unachukulia kwamba, kufuatana huko kwa maneno hayo sio sawa, wakati wa kumrejelea mwanamme .

(vii) Saba ni maana kimatini, ambayo hubainika kwa kutegemea namna ambavyo maneno kwenye matini yameoanishwa na kuambatanishwa.

Umbo na mpangilio wa matini unaweza kutazamwa kuanzia kwa vipashio vyenye ukubwa wa sentensi au mshororo na kuendelea.

Kwa hivyo, aina hii ya maana maḡa nyingi huhusishwa na; kuwepo au kutokuwepo kwa mpangilio bayana, wa sentensi, aya, sura n.k. katika MA.

Mpangilio maalum husababisha maana kupokelewa na hadhira kwa njia maalum. Mtafsiri anapozingatia aina hii ya maana, hulazimika kujaribu kupangilia ujumbe wake kwa njia ambayo haiwezi kuwakanganya wapokeaji wa MP.

Ni muhimu kwa mtafsiri, kupata na kung'amua maana halisi ya usemi katika matini anayoyashughulikia. Anapoiielewa vyema maana ya MA, shughuli zake za kuhamisha maana hiyo hadi kwenye MP huwa rahisi.

Tukio la kung'amua maana katika kifungu cha maneno kama vile sentensi, mshororo, aya, ubeti n.k. hufungamana na uwezo wa mtafsiri wa kuzingatia kauli za ukweli na uhalisi wa ujumbe anaouwasilisha kwa MP.

Bila ya kuzingatia kanuni za ukweli na uhalisi, mtafsiri anaweza kupotoka kimaana. Hata hivyo kauli hizi za ukweli-kimaana na usahihi-halisi wa ujumbe unaotafsiriwa, haziwezi kufikiwa kwa kuzingatia tu kaida za kisemantiki bali pia kwa kuhusisha viziada vingine vinavyoambatanishwa na lugha.

Uchunguzi wetu unaonyesha ya kwamba dhana ya maana, kupitia kwa nadharia ya semantiki, hutegemeana na maswala mengine yasiyo ya kisemantiki ili kuwezesha kuwepo kwa ukubalifu wa maana ya kitu ambacho kinaashiriwa kwenye matini.

Maana katika matini inayotafsiriwa huwa si rahisi kueleweka, hasa iwapo dhana inayoashiriwa kwenye kifungu cha maneno haifahamiki katika ulimwengu wa lugha ya MP.

Mara nyingi, matini huwa imefungamana na muktadha wa lugha. Vivyo hivyo maana ya matini huwa imejikita katika miktadha maalum.

Kuhusiana na haya, Nida (1975) alidai ya kuwa "maana ya usemi kwenye matini huhusiana na elementi za msingi, kimawasiliano ... kama vile chanzo cha ujumbe (mwandishi), ujumbe anaowasilishwa na wapokeaji ujumbe (wasomaji)."33

Mtafsiri anapozingatia kipengele cha; mwandishi, anaweza kuelewa maana ya MA huku akielewa pia dhamira ya mwandishi asilia. Anapofanya hivyo, ujumbe anaowasilisha huwafikia wasomaji wake vyema, kwa vile anadumisha ile dhamira ya mwandishi asilia.

Kwa mtazamo wa Beekman na Callow (1974) pamoja na wasomi wengine, maana ni (kama) ujumbe ambao huwasilishwa kupitia umbo maalum la lugha.

1

Waliongezea ya kuwa maana ya MA yangeweza kuwasilishwa vyema zaidi iwapo yangefikishwa kwa HP kupitia mfumo wa umbo la lugha pokezi. Kwa njia hiyo, maana kwenye ujumbe huzalisha mguso halisi kwenye lugha hiyo pokezi.

Wasomi wengi wanakubaliana ya kwamba sifa za kisemantiki katika lugha ya ushairi ni pamoja na kwamba; katika shairi, maana inayopewa kifungu kama vile mshororo au ubeti hujengeka kulingana na uhusiano baina ya maneno yaliyotumika, jinsi ambavyo yanapakana na kutegemeana kwenye kifungu.

Tunakubaliana na madai haya ya kwamba kutokana na maana ya kila neno linalotumika kwenye matini, msomaji anaweza kuhusisha dhana na kile umbacho kinarejelewa, na hatimaye akaweza kufikia maana kamili inayoeleweka kwake.

Inavyodhihirika ni kwamba mtafsiri pamoja na wasomaji wa MP, hawana budi kusoma shairi, neno kwa neno jinsi yanavyofuatana hadi mwisho ndipo waweze kudai ya kuwa wameelewa maana halisi ya matini.

Mtafsiri vilevile hulazimika kujifahamisha na maswala mengi yanayohusu mawasiliano na pia kupata ujuzi kamili wa lugha ya ushairi, ili aweze kufikia fasiri mwafaka kimaana.

Pamoja na kuzingatia hayo yote kuhusiana na tafsiri ya ushairi, inavunja moyo kwamba kipengele cha maana katika uwanja wa ushairi bado haujaeleweka vyema kwa wengi wanaoyasoma mashairi.

Kwa jumla, ushairi una utata mwingi sana na maana katika mashairi yanayotafsiriwa, inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya namna moja. Mara nyingine baadhi ya mashairi huwa mafumbo magumu.

Kutokana na utata wa maana katika mashairi yanayotafsiriwa kama katika diwani ya Risasi Zianzapu Kuchanua (1975), tungependa kuzingatia swala hili kwa kuhusisha dhana ya maana na mitazamo inayotilia maanani uwazi na ufiche wa ujumbe unaotafsiriwa. Swala hili tumelitazama kwa undani katika kurasa zinazofuata.

Mtafsiri ni lazima aamue mambo yapi yaliyo na umuhimu kwenye MA na pia kuamua mambo yanayopasa kufahamika kwa hadhira pokezi. Ili kufanikisha upitishwaji wa maana katika MP, mtafsiri vilevile ni lazima aamue ujumbe anaopaswa kuuweka wazi na upi kati ya ujumbe ulio wazi, anapaswa kuufutilia mbali.

Culy (1993:43) anasisitiza ya kuwa, mtafsiri anapochukua hatua hiyo ya kuuweka wazi au kuufutilia mbali ujumbe, anaweza kupata tafsiri yenye uhalisi zaidi kimaana. Hayo madai yana mashiko kwetu. Tanaonelea kwamba ni kauli inayofaa kuzingatiwa na watafsiri wote.

Wakirejelea mtazamo wa Lyons; Brown na Yule (1983:28) walifafanua dhana ya maana, kiurejeshi ambayo ni muhimu kwa mtafsiri anayezingatia vipengele vya ufiche na uwazi wa ujumbe kwenye matini.

Madai ya Lyons (1968:404) ni kwamba, upo uhusiano wa kiurejeshi baina ya maneno na vitu vinavyorejelewa na maneno hayo katika matini.

Aliongezea Lyons (1977:177) ya kuwa mzungumzaji (mwandishi) ndiye ambaye hurejelea kitu kupitia kwa maneno anayoyatumia. Huko kurejelea, kwa hakika ni kuhusisha dhana na neno. Hiyo ndiyo maana halisi ya kirejelewa.

Kipragmatiki, urejeleaji ni dhana mojawapo ya utendaji katika maana, ambayo hutazamwa kama tukio ambalo msemaji au mwandishi wa matini hulitekeleza kupitia kwa maneno yake.

Mtafsiri vilevile hulazimika kutilia maanani kaida za udhanifu au presaposisheni katika matini anayoishughulikia. Kipengele hiki huhusiana na maana kiurejeshi.

Kwa kutumia kauli hizo za udhanifu, mtafsiri huweza kukata kauli kimaana, kuhusiana na yale ambayo mwandishi wa MA aliashiria na kumaanisha kwa maneno aliyoyatumia.

Mtafsiri akiweza kudhania maana iliyoashiriwa na mwandishi asilia, anaweza hatimaye kuipitisha hiyo maana hadi kwa hadhira pokezi. Mtafsiri hufikia maamuzi kuhusiana na yale anayoyadhania kimaana kwa kutilia maanani maswala mengi ambayo huwepo ndani na nje ya matini anayoitafsiri.

Givon (1979a:50), hata hivyo anawatahadharisha watafsiri ya kwamba, licha ya manufaa ya kutumia presaposisheni katika ukadiriaji wa maana, watafsiri lazima wakumbuke kwamba yale ambayo wanachukulia kuwa yanaashiriwa na kumaanishwa na mwandishi asilia, hayana budi kukubalika vilevile miongoni mwa wapokeaji ujumbe.

Ili kuimarisha ukubalifu wa maana inayoashiriwa katika MP, mtafsiri atalazimika kuzingatia umantiki wa ujumbe. Umantiki wenyewe ni lazima udhihirike kwa wafuatao: mwandishi asilia, mtafsiri na wapokeaji ujumbe.

Kipengele hiki cha udhaniaji hakiwezi kupuuzwa katika ulelewaji wa maana kwenye MT na katika usemi wowote ule.

Kipengele kingine kinachochangia uelewekaji wa maana kiurejeshi ni kile cha implikecha.

Grice (1975) aliitumia istilahi hii, implikecha, katika kuelezea hali ambapo mwandishi wa matini humaanisha kitu, zaidi au tofauti na ile maana tambuzi ya maneno hayo anayoyatumia.

Katika lugha ya kiswahili dhana ya implikecha inaweza kudhihirika kwa mfano; katika misemo, istiari, nahau n.k.

Msemo kama vile, tia motoni, humaanisha kuingiza mashakani au taabani, na wala sio, kitendo cha kuchukua kitu na kukitia motoni ili kukichoma.

Mtafsiri anapotumia implikecha, yeye hufasiri maana ya vifungu maalum vya maneno kwenye matini, kulingana na ujumla wa maneno yote yaliyotumika. Kaida hii humfaidi sana mtafsiri anayekabiliana na lugha ya kitamathali katika matini.

Mara nyingi maana inayofikiwa na mtafsiri huwa haidhihiriki moja kwa moja kwa wasomaji wasioelewa uimplikecha wa lugha ya MP, kama ambavyo tumeelezea katika huo mfano wa usemi.

Akiweza kuelewa na kuzingatia kaida za urejeleaji ziada zilizopo katika implikecha, mtafsiri anaweza kufasiri maana ya mafungu yaliyotumiwa kimafumbo ama kinahau, bila ya kutenda kosa au kupotoka kimaana.

Grice (1975:45)³⁴, alielezea kaida za ushirikiano kiimplikecha katika matini yaliyosemwa au kuandikwa.

Kaida hizi zinaweza vilevile kumsaidia mtafsiri, nazo ni: Kwanza, maneno anayoyatumia mwandishi/msemaji yawe na ujumbe ulio na itifaki na maana isiyoziidi wala kupunguka.

Pili ni kwamba, mwandishi/msemaji aseme mambo ya kweli na aliyo na hakika nayo pekee.

Tatu ni kwamba, ujumbe ambao anaupitisha mwandishi uwe ni wenye kufaa kwa hadhira lengwa pamoja na mwandishi mwenyewe.

Nne ni kwamba msemaji/mwandishi ajiepushe na njia ya kuwasiliana ambayo inaweza kusababisha utata na ugubikaji wa maana ya ujumbe. Mtafsiri anaposhindwa kuzingatia kaida za ushirikiano, anaweza kupotoka kimaana au kuwasilisha ujumbe usioeleweka kwa wapokeaji.

Ukisiaji/inferensi ni kipengele kingine ambacho mtafsiri lazima akizingatie katika dhana ya maana kiurejeshi.

Kupitia kwa inferensi, mtafsiri huweza kurejelea maana iliyofichika kwenye muktadha wa maneno yaliyotumika katika matini.

Ingawa inferensi hukaribiana zaidi na implikecha; jambo muhimu zaidi ni kwamba inferensi hudhihirika kupitia kitendo cha ukisiaji maana.

Ukisiaji ni ujengaji wa wazo linaloweza kuwa na maana sawa na ile ya kitu ambacho kinarejelewa kwenye matini.

Mtafsiri; kama vile msomaji yeyote yule, hupokea ujumbe kutoka kwa matini asilia. Wakati ambapo maana ya matini asilia haieleweki vizuri kwake, analazimika kukisia tu hiyo maana bila ya kuwa na hakika.

Mtafsiri anaweza kukisia maana kwa kujumulisha ujumbe anaoupata kwenye matini asilia. Aina hii ya inferensi ni lazima ihusishwe na umantiki unaodhihirika kwenye ujumbe wenyewe.

Kwa mfano sentensi zifuatazo zinaonyesha namna ambavyo mtafsiri anaweza kutekeleza ukisiaji kimantiki.

- A. Iwapo jua linawaka, kuna joto.
- B. Mchana wa leo kuna jua.
- C. Kwa hivyo leo kuna joto.

Ukisiaji wa aina hii unapaswa kufanywa kwa tahadhari na makini kwa sababu wakati mwingine maana inayotokana na inferensi kimantiki haiafikiani na ukweli wa mambo au hali halisi ya ujumbe wa matini.

Katika mfano wa sentensi tulizozitumia hapo juu, ukweli wa mambo ni kwamba sio lazima kuwa, wakati wowote ambapo kuna jua, hali ya joto kuwepo.

Kimazingira, jua linaweza kuangaza lakini mtu aliye juu ya mlima mrefu atahisi hali ya baridi kwa sababu ya upepo mkali n.k.

Ukisiaji mwingine ni ule wa kipragmatiki ambao unaweza kuonekana kupitia mifano ya sentensi zifuatazo:

- A. John alikuwa anaenda shule.
- B. 1, Mtu alikuwa anaenda shule.
2, John alikuwa anaenda mahali
3, Mtu alikuwa anaenda mahali

Kutokana na sentensi A, wasomaji wengi wa MA wanaweza kukisia ya kwamba John ni mwanafunzi kwa vile anaenda shule.

Lakini ujumbe zaidi unapofahamika kwao kama vile ujumbe wa sentensi C. Wiki iliyopita alishindwa kulithibiti darasa lake.

Ukisiaji wao unakuwa hauafikiani tena na ukweli wa mambo, ambao ni kuwa John ni mwalimu pale shuleni, na wala sio mwanafunzi kama ambavyo sentensi A. iliwafanya kufikiria.

Sentensi tatu kwenye kitengo B. ni mifano zaidi ya sentensi zinazoweza kumfanya mtafsiri kufikia ukisiaji usioafikiana na ukweli. Jambo kama hilo linaweza kutokea wakati wa kutafsiri matini yenye utata na ufumbaji mwingi kama vile shairi.

Hizo sentensi huhitaji ujumbe zaidi kama unaopatiwana katika sentensi A na C, B, 1-3 ndipo ziweze kueleweka na kufasirika vizuri.

Mtafsiri anayelenga kufikia ukisiaji wenye uhakika na uaminifu zaidi anapaswa kuhusisha ujumbe anaoukisia katika matini na ujuzi wake wa maswala yanayoizunguka lugha ya MA na hali kahdhalika maswala ya utamaduni wa jamii ya watu wanaohusika.

Ufiche na uwazi wa maana katika matini ni muhimu vilevile kuzingatiwa na mtafsiri, kama ambavyo tulikuwa tumetaja katika sehemu ya 2.2:

Maana iliyofichika ni ile ambayo haibainiki moja kwa moja katika jumla ya maneno yaliyotumika kwenye matini.

Maana ya aina hii, licha ya kutodhihirika moja kwa moja huwepo ndani ya matini kulingna na dhamira ya mwandishi asilia.

Mtafsiri ambaye ni kama kiungo cha kati kwenye mawasiliano baina ya mwandishi asilia na wapokeaji matini, huwa hana budi, ila kuiweka wazi hiyo maana iliyofichika, katika MP, ambayo ametafsiri.

Farrell na Hoyle (1995) wanadai kwamba hatua hiyo ya kuweka maana wazi, ni kitendo cha kujumulisha maswala yote yanayohitajika kimaana na wala sio tu hatua ya kutia nyongeza kwenye matini.

Maana isiyo wazi kwenye matini inaweza kutazamwa na mtafsiri kwa misingi ifuatayo:

- (i) Msingi wa kisaussure³⁵, ambao kwao, maelezo ambayo mtafsiri huhusisha anapofafanua ujumbe wa matini, hutazamwa kama uziada ambao unafaa kusaidiana na ujumbe ulio wazi katika kufanikisha uelewekaji wa maana ya matini pokezi.

Baadhi ya wananadharia wanaozingatia msingi huu, huonelea ya kuwa ujumbe wa kimaelezo ufungiwe kwenye mabano au utolewe kupitia maelezo ya tanbihi, sherehe au kurasa maalum zinazoambatanishwa na matini.

Tungependa kutahadharisha ya kuwa pana matatizo kadhaa ya kuzingatia mapendekezo kama hayo. Hamu ya wasomaji inaweza kupotea kwa vile MP itakosa mtirikiko wa moja kwa moja na hali kadhalika msomaji atalazimika kurejelea tanbihi au sherehe kila mara anaposoma. Jambo hili linaweza kuichosha sana HP.

- (ii) Msingi wa ufaaji³⁶, ambao kwao, tajriba na ujuzi wa msomaji au mpokeaji ujumbe wa matini ndio ambao humwezesha kufasiri maana isiyo wazi.

Msomaji hufanya hivyo, kwa kuhusisha ujuzi wake na muktadha unaorejelewa kwenye matini, kwa namna ambayo itamwezesha kufikia maana kamilifu.

Kulingana na msingi huu wa ufaaji, jukumu la mtafsiri ni kupitisha maana ya MA hadi katika lugha na mfumo wa MP.

Mtafsiri hutumainia ya kuwa baada ya kuupitisha huo ujumbe; msomaji ataweza kuuelewa na kisha kuuhusisha vyema huo ujumbe na maswala ya ziada yanayofungamana nao, wakati wa kuweka wazi maana iliyojificha.

Ujumbe ziada anaouongeza, msomaji (HP) wa matini unapaswa kuwa wenye kufaa na kuaminika, lau sivyo mawasiliano yatatumbukia nyongo na maana inayotazamiwa kufichuliwa haitafichuka.

(iii) Msingi wa kiutambuzi³⁷ ambao kwao, maana isiyo wazi na ambayo haidhihiriki kupitia ujumulisho wa maneno yaliyoandikwa, huwepo kwenye MA kwa sababu ni kitu ambacho kinafahamika akilini mwa mwandishi na wasomaji wake, akiwemo mtafsiri.

Ujumbe uliojificha mara nyingi huwekwa wazi kwa kujumulishwa na jumbe zingine zilizo wazi katika matini inayotafsiriwa.

Lazima mtafsiri ahusishe dhana ya maana na maswala mengineyo katika lugha ya matini.

Kwa kawaida, maneno kwenye matini huwa katika mazingira ya mahusiano tata ya kinfumo ambayo huingiliana na udhahania na uziada mwingi sana.

Mtafsiri ana jukumu la kuamua jinsi ya kutafsiri matini yoyote yale kwa kuzingatia vigezo kama usahihi, uelewekaji na ufaaji kimaana.

2.6: TANBIHI

1. Rabin, C. (Mha) (1958): Aspects of Translation. University of London Communication Research Centre, uk vii
2. Massamba, D.P. (Mha.) (1990): Kamusi ya Isimu na Lugha. Educ. Pub. and distributors Ltd, Dar es Salaam uk. 5
3. Catford, J.C. (1965): A Linguistic Theory of Translation O.U.P., London uk. 1
4. Dickinson, M. (Mha) (1975): Risasi Zianzapo Kuchanua E.A. Pub. Hse, Nairobi uk 66. Batuki imeelezwa kuwa aina ya ngoma inayopigwa kwa rithimu.
5. _____ uk. 109. Kisangwa ni neno linalotumiwa na jamii ya watu wa kule Angola kwa maana ya pombe ya kienyeji.
6. Bradley, V. (1990): "Assumptions Involved in Interpretive Decisions" katika Barnwell, K. (Mha.), Notes On Translation S.I.L, Dallas. uk 23
7. Hatim, B. na Mason, I. (1990): Discourse and the Translator. Longman, London/N.York uk.viii - ix

8. Beekman, J. na Callow, J. (1974): Translating The Word of God.
Zondervan Pub. Hse, Michigan uk 21
9. Zaja, O. (1986): "Fasihi Tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya
Kiswahili: Matatizo na athari zake", Tasnifu
ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. uk. 40.
10. Brown, G. na Yule, G.(1983): Discourse Analysis. Cambridge
University press, Cambridge uk. 28
- i) Uhusiano wa vipashio tungo kiulalo/kiusilasila (Syntagmatic
association).
- ii) Uhusiano wa elementi kiuolezo faridi, huwa ni uhusiano wima
wa vipengele vya kiisimu katika matini (paradigmatic
association.)
11. Newmark, P. (1981): Approaches to Translation. Pergamon Press,
New York uk. 39
12. Ali, C. W. (1981) "The problem of translating from English Into
Swahili as exemplified by V. O. K. News Items" :
Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi uk. 24
13. Kama 9 u.k. 45
14. Kama.12 u.k. 11

15. Newmark, P. (1988): A textbook of Translation. Prentice Hall,
Newyork. uk. 282
16. Kama 9, u.k. 49
17. Lyons, J. (1963); Structural Semantics. Basil Blackwell,
Oxford u.k. 83
18. Wales, K. (1989): A Dictionary of Stylistics. Longman,
London/N. York uk. 79
19. Hartmann, R.R.K. na Stork, F. C. (1972): Dictionary of Language
and Linguistics. Applied Science Pub. Ltd. London
uk. 42
20. Crystal, D. (1987): The Cambridge Encyclopedia of Language
Cambridge Univ. Press, Cambridge/N. York uk. 10
21. Kama 7 u.k. 104
22. Kama 7 u.k. 104
23. Goerling, F. (1976) "Relevance and Transculturation" katika
Barnwell, K. (Mha.) Notes On Translation. Vol.10
No 3, S. I. L. Inc, Dallas uk. 50

24. Gutt (1991); "Translator's Perspective on meaning, Arelevance theory: A guide to succesful communication in translation; katika Barnwell, K. (ed) Notes On Translation, S.I.L. Inc. Dallas, U.S.A. u.k. 34.
25. Kama 2, u.k. 16
26. Kama 23, u.k. 50
27. Kama 2, u.k. 55
28. Kama 2, u.k. 44
29. Kama 20, u.k. 100
30. Kama 20, u.k. 101
31. Kama 20, u.k. 101
32. Kama 20, u.k. 101, S, inasimamia 'stimulus', Y, inasimamia 'speaker', s, inasimamia 'speech', R, inasimamia 'response'.
33. Nida, E. A. (1975): Componential Analysis of Meaning. Mouton pub, The Hague/N. York uk. 28

34. Kama 10, u.k. 32 wakimnukulu Grice (1975:45) ambaye alieorodhesha kaida za ushirikiano (cooperative principle) wakati wa kuwasiliana kuwa:

Upimifu (quantity)

Ubora (quality)

Ufaaji (relevance)

Namna ya kuwasilisha (manner)

SURA YA TATU

3.0: MATATIZO YALIYOSABABISHWA NA PUNGUFU UPANDE WA MTAFSIRI...

3.1: UTANGULIZI.

Katika sura hii tunajadili matatizo mbalimbali ya tafsiri ambayo kwa jumla yanaweza kuelezewa kama yaliyosababishwa na pungufu upande wa mtafsiri.

Matatizo katika sura hii yanahusu maswala ya kiisimu na sarufi ya lugha asilia na lugha pokezi.

Uchanganuzi wenyewe unatekelezwa kwa kulinganisha vipengele vya kiisimu vinavyopatikana katika MA na vile vya MP.

Tumezingatia viwango vya kiujenzi wa vipashio vya lugha; kuanzia/grafolojia, fonolojia, mofolojia, leksia, sintaksia na hata kufikia uambishaji wa vipengele vya lugha zinazohusishwa katika tafsiri.

Athari kutokana na matatizo tunayojadili zina dhihirika kupitia kwa umbo la lugha, mpangilio wa maneno na mfumo wote wa MP. Hayo tumeyaelezea kinaganaga katika sura hii.

Tumechanganua kwa undani, kila mojawapo ya sababu za kutoafikiana kwa namna nyingi, ambao huwepo baina ya vipashio vya MA na MP.

Ili kuweza kujadili vilivyo matatizo tuliyoyarejelea katika sura hii; tumenyuku mifano mwafaka kutoka katika mafungu tofauti tofauti ya MA na MP.

3.2.0: MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA GRAFOLOJIA.

Katika kiwango hiki, tumezingatia maswala kama ya uakifishaji na alama zinazohusika kama vile, alama za kuuliza, kushangaa, ritifaa, dukuduku, mabano n.k.

Tumechunguza jinsi ambavyo kuongezwa au kufutiliwa mbali kwa alama hizo katika MP hutatiza maana na mawasiliano baina ya mtafsiri na HP.

Vilevile tumetazama matatizo yanayosababishwa na hatua ya mtafsiri ya kubadilisha herufi ndogo na kubwa au kubwa na ndogo; pia tukio la mtafsiri kubadilisha nafasi za baadhi ya vipengele au kuvipangilia upya vipengele katika mishororo ya MP.

Vipengele vyote vya kigrafolojia vinapobadilishwa na mtafsiri kwa njia yoyote ile, MP hayana budi kuathirika.

3.2.1: KUONGEZWA KWA ALAMA ZA GRAFOLOJIA KATIKA MP.

Mtafsiri ameongezea alama ya mshangao katika baadhi ya vifungu vya MP. kwa mfano;

1. (MA:39) - but they sing
(MP:42) Lakini wanaimba!

Kuongezwa kwa hiyo alama ya mshangao katika MP, kumesababisha kifungu hicho kupata toni ya ushangao, tofauti na toni iliyo kwenye MA ambayo haikuashiria ushangao wowote. Jambo hilo huitatiza HP,

kimawasiliano, kwa vile hiyo toni ya ushangao inaiongezea thamani kifungu cha MP. Nyongeza hiyo ya thamani inasababisha tofauti kati ya MA na MP.

Vivyo hivyo, mtafsiri ameongeza alama ya kuuliza katika MP.

Kwa mfano;

1. (MA:78) and mourned

the Funda women's fate.

(MP:85) Huku tukilia kwa mikasa

ya wanawake wa Funda?

Kifungu hicho cha MP kilichoongezewa alama ya kuuliza na mtafsiri, kimebadilika kutoka kauli ya kawaida kiusemi hadi kauli ya kuuliza.

Maana inayoletwa na swali hilo kwenye MP ni tofauti na maana iliyoko kwenye MA, ambapo HP haikuhitajika kufikiria jibu lolote akilini mwao. Hivyo sivyo ilivyo katika MP.

Zaidi ya hayo, muwala baina ya mishororo hiyo miwili na mingine katika ubeti wa shairi umepotezwa katika MP kwa sababu ya hiyo hatua ya mtafsiri kuongeza alama ya kuuliza.

Ujumbe unaowasilishwa kwa msomaji umefikwa na ugumu kwa kiasi kidogo kwa vile uitifaki ambao hutokana na mtiririko katika mshororo unaotangulia na ule unaofuata kwenye MA umepotezwa. HP ya tafsiri, haielewi waziwazi, kule ambako swali; ya wanawake wa funda? linatoka wala kuelekea.

3.2.2: KUFUTILIWA MBALI KWA ALAMA ZA GRAFOLOJIA KATIKA MP

Alama ya ritifaa ambayo hutumika mara nyingi katika lugha ya kiingereza pamoja na majina ya watu au vitu wakati wa kuashiria umilikishi, kwa mfano katika John's car, maana inayosababishwa na hiyo alama ni kuwa gari linalozungumziwa ni la John.

Katika lugha ya kiswahili, mtafsiri hulazimika kufutilia mbali alama hiyo kwa vile matumizi ya alama hii haiashirii umilikishi katika lugha hii.

Jambo la kuzingatiwa hapa ni kwamba tofauti za kiumbo zilizopo baina ya lugha asilia na lugha pokezi ndizo humfanya mtafsiri kufutilia mbali alama ya ritifaa katika MP. Badala yake, mtafsiri hana budi kutafsiri kifungu cha MA kimaelezo.

Tatizo ni kwamba umbo la kigrafolojia la MA hubadilika nao ujumbe unaowasilishwa hali kadhalika huathirika kwa vile maelezo hayo hufafanua MP zaidi ya kifungu cha MA.

Kwa mfano;

1. (MA:65) With the English sailor's swiss watch

(MP:71) Saa ya mkono toka uswisi

Mali va baharia wa Kiingereza.

Maelezo, mali va baharia, ndiyo yanayoakisi dhana inayotokana na kifungu sailor's, ambamo alama ya ritifaa ilitumiwa.

Katika mishororo mingine ya MP, mtafsiri alifutilia mbali

alama ya kuuliza kimakosa. Kitendo hicho hutatiza maana inayowasilishwa kwenye MP. Mifano ni kama vile

1 (MA:78) My good friends, my brothers, Benge, Joaquim, Gaspar, Ilididio, Manuel and who else?

(MP:95) Rafiki zangu wakubwa, ndugu zangu, Benge, Joaquim, Gaspar, Ilididio, Manuel na wengine;

Mighairi ya kwamba swali la MA ni la balagha, ambalo halihitaji jibu lolote, ingefaa zaidi iwapo mtafsiri angehakikisha ya kuwa amedumisha hiyo alama ya kuuliza, ndipo thamani ya kimawasiliano ya MA. iweze kudhihirika katika MP.

Tatizo linalotokana na huko kufutiliwa mbali kwa alama hiyo ya kuuliza ni kwamba, dhana ya ubalagha iliyowasilishwa na MA imetoweka katika MP.

Kwa jumla, kauli za MA na MP zinatofautiana sana, kwa vile MA ni swali. ilhali MP imefanywa kuwa kauli ya kawaida isiyomwuliza msomaji, swali lolote.

Mtafsiri hali kadhalika alifutilia mbali alama za duku duku zinazopatikana katika MA. Kwa mfano;

1 (MA:56) of your moonlight ... My beginning and my end ...

(MP:61) Upole wa mbalamwezi yako

Mwanzo wangu na mwisho wangu

2 (MA:55) ... of sunlight, of the sun, immortal, fecund and beautiful.

(MP:59) Katika mionzi ya jua lisilosinzia. Alama za dukuduku ni mbinu mojawapo anayoitumia mwandishi katika umbuji wa kazi yake.

Katika MA ambamo alama hizi za duku duku zimetumika HP, hupata hisia akilini mwao ya kwamba baadhi ya maneno yalifutuliwa mbali na mwandishi katika makala hayo asilia.

Vilevile inawezakana kwamba mwandishi wa MA alitumia alama hizo ili kuyarembesha na kuyapa matini yake mvuto zaidi.

Alama hizo zinapofutuliwa mbali na mtafsiri kwenye MP, tatizo linalozuka ni kwamba ladha na mvuto wa kisanii wa MA inapotea kwenye MP.

Mishororo ya MP vilevile inabadilika kiumbo, inakuwa kama kwamba mtafsiri ameyaumbua matini ambayo mwandishi asilia aliyaumba kwa lengo maalum.

Mabano pinde, ni alama zingine za grafolojia ambazo mtafsiri alizifutilia mbali katika baadhi ya mafungu ya MP kwa mfano;

1. (MA:48) They have a way of sucking strength an infallible system for robbing youth (cry of the chope man who went away without the right of return).

(MP:52) Ni maarifa kunyonya nguvu za watu
Kilio cha mchope, aliyekwenda
Bila ya haki ya kurejea.

2. (MA:100) It will be small, our well built house
(although I have millions of brothers)

(MP:110) Itakuwa ndogo
Japo ninao ndugu mamilioni

Kufunguwa kwa vifungu vya maneno katika mabano pinde kwenye MA, kunawafanya wasomaji kuvitazama vifungu hivyo kwa namna maalum.

Kimawasiliano, hivyo vifungu, vimefungiwa katika mabano pinde kwa sababu vinatekeleza jukumu la kufafanua ujumbe unaopitishwa na mishororo inayovitangulia hivyo vifungu.

Tatizo linalosababishwa na huko kufutiliwa mbali kwa alama hizo ni kwamba umaalum wa vifungu vilivyofungiwa pamoja na thamani ya kimawasiliano ya hivyo vifungu; ambayo ni kufafanua jumbe zinginezo kwenye matini, inatoweka bila ya kuifikia hadhira ya MP. Wao watachukulia vifungu hivyo kuwa tu mishororo ya shairi bila ya kutambua jukumu hilo maalum kuhusiana na hicho kifungu.

3.3.0: MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA FONOLOJIA

Matatizo katika kiwango hiki huhusu vipashio vya lugha vinavyoingiliana na utankaji wa maneno na ubunifu wa sauti zozote zenye maana katika lugha.

Sauti yoyote yenye maana katika lugha, vilevile huwa na thamani yake kimawasiliano. Hivyo basi mtafsiri anapoongeza au kufutilia mbali kipashio kinachowakilisha sauti yenye maana katika lugha, tafsiri yote huchujuka au kuimarika kithamani.

Hatua hizo husababisha tofauti za kimawasiliano kutokea baina ya MA na MT.

3.3.1: KUONGEZWA KWA SAUTI KATIKA MP

1 (MA:58) MOTHER !

(MP:63) Ee Mama!

Kipashio Ee kilichoongezwa na mtafsiri kwenye mshororo wa MP, kina thamani ya ushangao, na hivyo basi MP inapata msisitizo wa dhana hiyo.

Hata ingawa MA vilevile imeonyesha dhana hiyo kupitia matumizi ya alama (!) ya mshangao, jambo muhimu kuzingatiwa ni kwamba MP inasisitiza zaidi huo ushangao kupitia kwa sauti Ee na alama (!).

Tatizo linalohusiana na mfano huu ni la kutoafikiana kwa MA na MP katika thamani ya kimawasiliano.

3.3.2: KUFUTILIWA MBALI KWA SAUTI KATIKA MP.

- 1 (MA:73) Oh why have they stolen Joao from us?
(MP:80) Kwa nini; kwa nini wametuibia Joao.
- 2 (MA:67) Oh, my white teeth of ivory
(MP:73) Meno yangu meupe kama pembe
- 3 (MA:47) Oh, and they've lost their heads
(MP:50) Na tena wamekwisha kuchinjwa

Katika mfano wa kwanza, tatizo lililosababishwa na hatua ya mtafsiri ya kufutilia mbali sauti oh, ni kwamba mshororo wa MP umebakia tu kama swali la balagha linaloulizwa na mtafsiri ilhali katika MA, fauka ya mshororo huo kueleweka kuwa ni swali, vilevile unadhihirisha toni ya msiba uliowapata wahusika wanaosononeka na kuhuzunika kwa sababu ya kuibiwa kwa Joao.

Toni hiyo ya msiba inayoletwa na sauti oh kwenye MA haionekani katika kifungu cha MP.

Mifano inayofuata, (2 na 3) inadhihirisha tatizo linaloshabihiana na 1, ambalo ni kwamba, ushangao au ustaajabu unaowasilishwa na MA, unafifia na kutodhihirika katika MP.

Tatizo hili linaifanya MP kuonekana tofauti na MA kiumbuji. Sifa za fani katika MA zimepotezwa katika vifungu vya MP.

3.4.0: MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA MOFOLOJIA

Katika lugha yoyote ile, vipashio vya kimofolojia ndivyo ambavyo huunganishwa ili kuzalisha vipashio vikubwa zaidi ambavyo vinaweza kuwa ama virai, vishazi, sentensi/mishororo n.k.

Kipashio cha kimofolojia nacho hujengeka kwa kuunganishwa kwa vipengele vya kifonolojia katika lugha. Ujenzi huu wa vipashio hutegemea mfumo wa lugha inayohusika.

Mbali na kuunganisha vipashio ili kujenga vingine vivubwa zaidi ya hivyo, mwanalugha hulazimika vilevile kupangilia vipashio vya kimofolojia kwa njia inayokubalika katika lugha yoyote ile, ndipo maana ya kifungu cha maneno ipatikane na kueleweka kwa HP.

Katika MP tunayoishughulikia, mtafsiri amebadilisha nafasi ya baadhi ya maneno kwenye mishororo aliyoitafsiri. Uhuru wa mshairi unaweza kumruhusu kubadilisha nafasi ya maneno na kupangilia upya maneno katika mishororo ya shairi; hata hivyo, jambo hili likifanywa kupita kiasi, mtiririko na rithimu ya ujumbe anaowasilisha kwa HP, huvurugika.

Kwa mfano katika mafungu yafuatayo:

- 1 (MA:105) With weapons and with courage - hurry
(MP:115) Haraka: kwa silaha na ushujaa
- 2 (MA:108) Your image comes close to me.
It is for you too I am fighting, mother
(MP:119) Mama, nakumbuka sana
Maana napigana kwa ajili yako pia
- 3 (MA:121) ALL OF US
TODAY
TO ACOMPLISH OUR TASK
(MP:131) Tutekeleze wajibu wetu :
Sisi wote leo -

Katika mifano 1 na 2, maneno yanayopatikana mwanzoni mwa mishororo ya MA yamehamishwa hadi mwisho wa mishororo ya MP, na yaliyokuwa mwishoni mwa MA yakahamishwa hadi mwanzoni mwa MP.

Huu ubunifu upya wa hiyo mishororo, unaofanywa na mtafsiri haukuhitajika, kwa vile hata kama hangeyahamisha hayo maneno hadi mwisho au mwanzo wa mishororo ya MP ujumbe ungali ungepitishwa sawa na ulivyo kwenye MA.

Katika mfano 3, mtafsiri alikihamisha kifungu cha maneno kutoka mwanzo wa ubeti hadi mwisho wa ubeti. Tatizo lililosababishwa na huo upangiliaji upya wa hivyo vipengele vya kimofolojia ni kwamba, kaida za utunzi wa sentensi za lugha ya kiswahili sanifu zilikiukwa. Hivyo basi badala ya kuanzia kirai

nomino na kisha kirai kitenzi, mtafsiri ametenda kinyume cha jambo hilo. Mpangilio huu wa mtafsiri haukubaliki sana katika mfumo wa kiswahili sanifu.

3.5.0: MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA SINTAKSIA.

Vipashio tunavyovichunguza hapa ni vile vyenye kujengeka kwa muungano wa zaidi ya neno moja. Hivi vipashio ni kama vile virai, vishazi/vijisehemu vya mishororo, mishororo yenyewe na hata kufikia beti za shairi.

Mtafsiri ameitatiza hadhira pokezi katika kiwango hiki kwa kuchukua baadhi ya hatua zifuatazo:

3.5.1: KUGAWANYA MISHORORO YA MA.

Mifano ni kama vile:

1. (MA:52) to bring back our days together in our secret
haunts, nights lost in the long grass.
(MP:56) Kukumbusha zamani
Tulipojificha peke yetu manyasini
Hadi usiku ukacha
2. (MA:66) And the brown body of Mulatto Margarida
(MP:77) Na chotara Margarida
Rangi yake maji ya kunde
3. (MA:96) Those strange times
When the affront blew burning

Through the cells of a brain rebelling at humiliation

...

(MP:105) Nyakati zile za dhiki

Machukizo yalipozidi

Na ubongo kusita

kukataa kupuuzwa.

4. (MA:101) The height

Of each furrow

And the light of each star

(MP:110) Kimo cha kila

Mwangaza wa kila nyota

Mtafsiri anapogawanya mishororo ya MA katika vijisehemu vingi katika MP, kuliko ilivyokuwa katika MA, tatizo ni kwamba anabuni mishororo mingine isiyoweza kujisimamia yenyewe kama vipashio vya kisintaksia wala kujitegemea kimaana.

Mifano inayodhihirika kupitia mishororo ya MA iliyopigiwa mistari chini yazo ni ya mafungu tegemezi ambayo hata hivyo mtafsiri ameyaweka kujisimamia yenyewe kana kwamba ni vipashio huru. Tafsiri ya ushairi ifanyayo hivyo mara nyinyi, huitatiza HP, kimawasiliano.

Bila ya HP kuhusisha mishororo hiyo na ile mingine kwenye MP, maana kamili ya hivyo vipashio vya kisintaksia vilivyopigiwa mistari haiwezi kudhihirika waziwazi, kwa vile haijitegemei yenyewe.

3.5.2: KUTAFSIRI MISHORORO YA MA. MOJA KWA MOJA KATIKA MP.

Mifano ni kama vile;

1. (MA:77) This is the land
Where we were born
(MP:84) Hii ndiyo nchi
Sisi tulimozaliwa

2. (MA:41) Four and twenty moons
not seeing women
(MP:44) Ishirini na minne miezi
Bila mwanamke

3. (MA:80) ... beneath the claw
(MP:88) Chini ya makucha

Katika mfano 1, kifungu cha MA, we were born, kinapotafsiriwa moja kwa moja kama sisi tulimozaliwa katika MP, mfumo wa utunzi wa vipashio vya kisintaksia vya lugha pokezi, unatatizika kwa vile ni mpangilio alioulazimisha mtafsiri katika LP, nao unaathiri mtiririko wa ujumbe.

Mfano wa 2, unadhihirisha jinsi ambavyo tafsiri ya moja kwa moja ya maneno, unasababisha muwala katika kifungu cha MP kuvurugika, vilevile maana ya kifungu hicho cha MP, haiwasilishwi vyema kwa HP, kwa vile inawalazimu kukisia tu kile ambacho ujumbe wa kifungu hicho humaanisha/hurejelea.

Hali kadhalika, katika huu mfano wa pili, mtafsiri ameipitishia hadhira ujumbe usiolingana na ule wa MA, kwa vile

anatafsiri neno women lililo katika wingi kama mwanamke ambalo ni neno katika hali ya umoja.

Mfano wa 3, vilevile unawatatiza wasomaji wa MP kwa vile tafsiri chini va makucha, ambayo ni ya moja kwa moja haikuakisi vya kutosha, dhana ya MA, beneath the claw, HP, hailewi wala kupata mantiki ya ujumbe wa MP.

Tatizo lingine alilolisababisha mtafsiri ni la kutafsiri neno claw, lililo katika kauli ya umoja kama makucha, ambalo ni neno katika kauli ya wingi.

3.5.3: KUFUTILIWA MBALI KWA BAADHI YA VIPENGELE KATIKA MP.

Hatua kama hii mara nyingi huchukuliwa na mtafsiri aidha kimaksudi akitarajia kuimarisha maana ya ujumbe wa MP au kimakosa, bila ya kutambua athari za hatua kama hiyo.

Ni muhimu hata hivyo, kuelewa kwamba kufutiliwa mbali kwa baadhi ya vipengele katika MP, wakati mwingine husababisha upungufu wa kimaana na kimawasiliano katika ujumbe ambao hatimaye huifikia HP ya tafsiri.

Katika diwani hii ya Risasi Zianzapo Kuchanua (1975), mtafsiri, amefutilia mbali baadhi ya vipengele vya kisintaksia na kwa njia hiyo akaathiri ujumbe wa MP, kama ambavyo inadhihirika kupitia mifano ifuatayo.

1. (MA:79) Hearts beating rhythms

(MP:86) Mioyo inadunda

Neno rhythms katika MA, linaelezea zaidi jinsi ambavyo midundo

ya mioyo ilitendeka kwa rithimu. Mtafsiri amelifutilia mbali neno hilo katika MP.

Tatizo linalosababishwa na hatua hiyo ni kwamba HP ya tafsiri, inapata tu kufahamu kwamba mioyo inayozungumziwa ilidunda lakini, hadhira hiyo haipati kufahamu jinsi ambavyo huo mdundo uliendelea kwa rithimu maalum.

2. (MA:97) This is the time of armed struggle
(MP:106) Huu ni wakati wa mapambano

Kufutiliwa mbali kwa neno armed, kumesababisha maelezo hayo kuhusiana na aina ya mapambano yanayozungumziwa katika MA, kutodhihirika kwa hadhira ya MP.

Neno armed, linaashiria ya kuwa hayo mapambano ni ya kijeshi na pia yanahusu matumizi, ya silaha. Hata hivyo katika MP, wasomaji wanaweza hata kuchukulia kimakosa ya kuwa hayo mapambano yalikuwa ya aina nyingine isiyohusisha matumizi ya silaha; k.v. mapambano yanayotumia maneno ya kushtumu na kukashifu au propaganda ama hata mapambano mengine yanayohusisha njia za kichini chini na usiri mwingi.

Ufasiri wa ujumbe kwa njia isiyofaa kama hiyo ambayo tumeielezea hapa ni zao la hiyo hatua ya kufutiliwa mbali kwa baadhi ya vipengele vya kisintaksia.

3. (MA:99) When my brothers come home

(MP:108) ndugu zangu watakaporudi

Maana ambayo ingewafikia wasomaji wa MP, kupitia kwa neno home ambalo limefutuliwa mbali katika MP, imetoweka.

Badala yake, ujumbe unaoifikia HP, haudhihirishi kule ambako hao ndugu zangu, wanaozungumziwa, watarudi, yaani nyumbani. Katika MP, kule wanakorudi hakujulikani kwa vile mtafsiri hakukutaja. Kwa jumla, mifano yote mitatu inaonyesha kuathiriwa kwa ujumbe wa MA, kutokana na hatua ya kufutuliwa mbali kwa vipengele vilivyopigiwa mistari.

3.5.4: KUFUTILIWA MBALI KWA MAFUNGU YA KISINTAKSIA KATIKA MP.

Mifano ifuatayo inahusu kufutuliwa mbali kwa mafungu ya maneno yaliyozidi kipashio kimoja katika mishororo ya mashairi katika diwani hii.

Jambo hili linapotendwa na mtafsiri, pana uwezekano wa kutokea kwa matatizo kama yafuatayo:

1. (MA:54) Gleaming (ai, the colour of those backs ...)

Gleaming backs twisted on the torso

(MP:59) Angalia ing'aravyo rangi ya migongo hiyo.

Kufutuliwa mbali kwa kifungu kilichopigiwa mistari kumeikosha HP ya tafsiri, maelezo kuhusiana na migongo hiyo inayong'ara.

Ujumbe huo kwamba, licha ya kung'ara, migongo hiyo vile vile ilikuwa imepinda, haudhihiriki kwenye MP. Mbali na tatizo hili

kuhusiana na ujumbe unaowasilishwa; mtafsiri hakufungia kwenye mabano, kijisehemu cha matini kama ilivyo katika MA.

Kufungiwa huko kwa maneno katika mabano kulifanywa na mwandishi asilia ili kudhihirisha umaalum wa sehemu hiyo ya mshororo katika shairi linalohusika.

Hata hivyo, katika MP ambapo mabano hayo yamefutuliwa mbali, huo umaalum wa kifungu hicho haudhihiriki kamwe.

2. (MA:50) in which to sow and to bring to flower
the concesssion's seed

(MP:54) Walime mpaka wavune

Kifungu cha maneno kilichopigiwa mstari, kinatekeleza dhima ya ufafanuzi wa MA, kwa kuelezea jinsi ambavyo mbegu zinazozungumziwa zinatazamiwa kuwa na mavuno mema yenye kukubalika.

Hiyo maana inayofafanuliwa katika fumbo hilo, the concesssion's seed imepotezwa katika MP kwa sababu mtafsiri aliifutilia mbali sehemu hiyo ya kifungu cha shairi.

Maelezo yanayowafikia wasomaji wa MP, hayana ujumbe uliokamilika kama ulivyowasilishwa katika MA. HP inaelezwa tu ya kwamba, walime mpaka wavune; pekee ndio ujumbe wa kifungu hicho. Jambo hili silo pekee wanalopaswa kufahamu kwa vile yapo maelezo zaidi, ambayo hata hivyo yamefutuliwa mbali.

3. (MA:43) And voices left traced on the matting floor like the
dust on the streets
Their songs parting

(MP:46) Na sauti zilizoachwa zamani

Nyimbo zao za kuagana

Nyingi kama mavumbi ya barabarani.

Kufutuliwa mbali kwa kifungu; traced on the matting floor
kumeitatiza maana aliyolenga mwandishi, kuifikishia hadhira yake.

Kifungu hiki alikitumia mwandishi wa MA, ili kutoa ufafanuzi wa ujumbe kuhusiana na dhiki za vibarua waliokwenda migodini, ambako waliishi maisha duni, wakilalia mikeka kwenye sakafu zilizojaa vumbi tupu.

Dhana hiyo ya uduni wa hali zao za maisha, hasa jinsi walivyolala kwenye vumbi mithili ya vumbi inayoonekana barabarani, imefifishwa na mtafsiri kwa vile hakulitaja jambo hilo.

Badala yake, mtafsiri alifutilia mbali kifungu hicho, papo kwa hapo ujumbe wa kifungu hicho, nao ukafutika kabisa.

3.5.5: KUONGEZWA KWA MAFUNGU ZAIDI KATIKA MP.

Kimsingi, jambo ambalo humchochea mtafsiri kuongeza vipengele na mafungu zaidi kwenye MP, ni hamu kubwa ya kuimarisha mawasiliano baina yake na HP kupitia kwa MP anayoishughulikia, vilevile jaribio la kuweka wazi zaidi baadhi ya mambo yaliyofumbika katika MA, humfanya mtafsiri kuchukua hatua kama hiyo.

Ikiwa hatua hii ya kuongeza mafungu ya kimaelezo kwenye MP itasababisha kuimarika kwa maana inayowasilishwa na matini hayo, basi hatuwezi kudai ya kwamba mtafsiri amesababisha tatizo.

Hata hivyo si kauli ya lazima kwamba kila mara mtafsiri anapongeza kifungu zaidi katika matini, nayo maana huimarika.

Wakati mwingine kitendo hicho cha kuongeza mafungu zaidi ya kisintaksia husababisha matatizo yanayoathiri maana na mawasiliano katika jumbe zinazowasilishwa na MP kwa HP.

Mifano ifuatayo inafafanua tatizo hilo:

1 (MA:128) War

(MP:139) Mapambano ya vita

Neno war, lina maana ya vita, hivyo basi, hatua ya mtafsiri ya kuongeza kifungu mapambano ya katika MP, haijaboresha maana ya neno vita.

Kifungu hicho kilichoongezwa na mtafsiri hakikuhitajika kwa sababu, inafahamika kwamba mara nyingi, vita huwa hali inayohusu mapambano, silaha n.k. Jambo hilo tayari linaeleweka kwa HP.

2 (MA:120) Wearing out our hands and eyes
in the great sustained effort

(MP:131) Tukivichosha viungo, mikono na macho
katika juhudi zetu.

Neno lililoongezwa na mtafsiri katika MP halitekelezi jukumu la kiufafanuzi na wala halikuhitajika kuongezwa. Sababu ni kwamba HP tayari inaelewa ya kwamba mikono na macho ni miongoni mwa viungo katika mwili wa mwanadamu.

Kwa hivyo nyongeza hiyo inasababisha uradidi usiohitajika kwenye MP. Inafahamika kwamba hata bila ya kuongeza kiungo hicho katika mshororo huo, yale maneno mengine; mikono na macho. yalitoshwa kuwafahamisha wasomaji kwamba, yanayozungumziwa ni viungo vya mwili.

3. (MA:120) But air and space are free comrades

(MP:130) Lakini ndugu tukumbuke

Hewa na anga ni mahali huru

Tukumbuke, ni neno lililoongezwa na mtafsiri katika MP. Neno hilo limeufanya ujumbe unaowasilishwa uonekane kana kwamba unadhamiria ukumbusho wa jambo ambalo lilikuwa tayari limekwisha sahaulika.

Kulingana na MA, kauli ya kifungu hicho, haikuashiria wala kudhamiria ukumbusho wa namna yoyote ile, bali ililenga tu kutaja na kufahamisha ya kwamba hewa na anga ni mahali huru.

Tatizo ni kwamba kuongezwa kwa kipashio, tukumbuke. kumesababisha kauli ya ujumbe wa mehororo huo kubadilika kwenye MP.

4. (MA:104) In the gentle gifts of harvest

(MP:114) Yaendelee kustiri zawadi za mavuno

Hiki kifungu kilichopigiwa mstari, kimeongezwa na mtafsiri katika MP, lakini badala ya kuimarisha uwasilisho wa ujumbe katika kifungu hicho, kifungu hicho kimesababisha utata katika MP.

Sababu za mtafsiri kuongeza kifungu hicho hazionekani waziwazi kwa vile hata bila ya kukiongeza hicho kifungu, maana inayoifikia

hadhira ya MP haingevurugika jinsi ambavyo imetendeka katika haya MP.

Kwa kiwango kikubwa kifungu hicho cha MP, kimepotelewa na mtiririko na umantiki wa kimawasiliano, kikilinganishwa na mshororo wa MA.

5. (MA:70) Joao dreamt of Zambezi's flowing books

(MP:76) Joao aliwaza vingeandikwa vitabu

Kueleza bonde la mto Zambezi

Kwa mujibu wa MA, vitabu vingi sana kuhusiana na mto Zambezi vimekwisha andikwa. Mwandishi ametumia tashihisi la kububujika ili kuashiria huo uwingi wa hivyo vitabu alivyoviona katika ndoto/mawazo.

MP, inapoelezea ya kwamba Joao aliwaza kuhusu vitabu ambavyo vingeandikwa, ujumbe unaoifikia HP ya tafsiri unakuwa ni tofauti na ule wa MA ambao unaelezea ya kwamba vitabu hivyo tayari vipo, vimekwisha andikwa.

MP inaashiria ya kwamba vitabu hivyo bado havijaandikwa, hata hivyo upo mpango wa kuviandika. Utata huu wa kimaana baina ya kifungu cha MA na kile cha MP, umesababishwa na huo uongezwaji wa mafungu yasiyohitajika ya kisintaksia.

Vilevile bonde la mto Zambezi, ni nyongeza ambayo haitekelezi dhima ya kufafanua ujumbe katika MP. MA, hayakuzungumza kwa namna yoyote ile kuhusu bonde la mto, badala yake imeeleza tu ya kwamba vitabu alivyowaza kuvihusu Joao, vinazungumzia Zambezi. Mto wowote mkubwa, una mambo mengi sana ya kuzungumziwa na wala sio bonde pekee.

3.6.0: MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA LEKSIA NA SEMANTIKI.

Kiwango hiki kwa ujumla huhusiana na uchunguzi wa vipengele kama vile maneno na misamiati tofauti tofauti, yanayotumiwa na mtafsiri katika matini yake.

Vipengele hivyo, kwa kawaida huwa na maana ambayo wakati mwingine, inaweza kufikishwa kwa HP kwa njia isiyo nzuri au kwa namna ya kuwatatiza wasomaji.

Matatizo kama hayo yanapotokea katika kifungu chochote kile cha MP, ujumbe unaowasilishwa pia hutatizwa.

Kisemantiki, mtafsiri anaweza kuamua kutafsiri vifungu vya MA kwa namna inayoweka wazi maana ya hivyo vifungu katika MP. Hatua kama hiyo inaweza kusababisha matatizo katika kiwango hiki cha semantiki.

3.6.1: MATATIZO YA LEKSIA

Katika mifano ifuatayo, mtafsiri ametumia leksia za kijumla ambazo haziakisi dhana halisi zinazorejelewa katika MA.

1. (MA:61) hard wood of my land

(MP:66) Mti wa nchi yetu

"Hard wood" ni aina maalum ya mti, ulio mgumu sana. Dhana hiyo haidhihiriki katika MP ambapo mtafsiri ametumia leksia ya kijumla, mti. Thamani ya leksia hardwood, imefifia katika MP.

2. (MA:66) ... romantic nights

(MP:69) Starehe za usiku.

MA, inazungumzia starehe za aina maalum, nyakati za usiku. Romantic, inaashiria zaidi tukio la kimapenzi hasa baina ya watu wanaopendana. Hii ni aina mojawapo tu ya starehe tofauti tofauti.

Tatizo ni kwamba katika MP ambapo mtafsiri anaitaja aina hii ya starehe kwa maneno yanayojumulisha na aina nyingine nyingi za starehe; dhana hiyo kwamba ni usiku wa kimapenzi haiwafikii wasomaji wa MP.

3. (MA:118) With a submachine gun, a bazooka, a 12.7

(MP:128) Wakitamba na silaha za kisasa

Mtafsiri ametumia kifungu tulichokipigia mstari kama tafsiri ya aina mbalimbali za bunduki zilizotajwa katika MA.

Leksia za MA, zinarejelea aina za kipekee za bunduki ambazo hutofautiana kwa njia nyingi sana. Vivyo hivyo mtafsiri hakutilia maanani ya kwamba bunduki ni mojawapo tu ya aina nyingi za silaha zinazoweza kutumiwa vitani.

Tafsiri, silaha za kisasa, ni ya kijumla sana. Ni tafsiri inayochujua kabisa dhana inayofaa kuwafikia wasomaji, ambayo ni, aina tofauti za bunduki.

Inavyoeleweka kwa HP ni kwamba silaha za kisasa, hujumulisha sio tu bunduki bali pia mabomu, vifaru, ndege za kivita, meli zinazosafiri chini ya maji, guruneti na silaha zingine nyingi.

Hivyo basi, kwa kutumia leksia ya kijumla katika MP, mtafsiri ameikanganya hadhira pokezi kimaana. Thamani inayobebwa na leksia

ya kipekee si sawa na ile ya leksia ya kijumla.

Mifano mingine ni kama vile katika leksia zilizopigiwa mistari:

4. (MA:38) Where at night all alone the wild beast goes weeping
(MP:40) Isipokuwa vilio vya wanvama pekee
5. (MA:55) they gleam, they gleam, drummers of jazz
(MP:59) Wanang'ara, wanang'ara wapiga dansi
6. (MA:99) With roses and bougainvilleas
(MP:108) Ya waridi na maua

Tatizo hili la mtafsiri kutumia leksia za kijumla, mahali pa leksia ya kipekee ni kwamba, mara nyingi HP ya tafsiri hupata ujumbe tofauti kimaana, kithamani na hata kimawasiliano ukilinganishwa na ujumbe ulio kwenye MA.

Ni tatizo ambalo kwa jumla hutokea, wakati ambapo mtafsiri anashindwa kutumia leksia mwafaka wakati wa kutafsiri maneno anayokumbana nayo katika MA. Vilevile linaweza kusababishwa na hali ya mtafsiri, ya kutotaka kujiingiza katika utoaji wa maelezo mengi kuhusiana na baadhi ya leksia, wakati wa kutafsiri kutoka lugha ya MA.

Tatizo la pili kuhusiana na leksia ni la mtafsiri kuwasilisha baadhi ya leksia jinsi zilivyo katika MA, bila ya kuzitafsiri. Jambo hili mtafsiri hulifanya, fauka ya kwamba visawe vya leksia kama hizo, vipo katika lugha ya MP.

Kwa mfano:

1. (MA:45) Magaica
(MP:48) Magaica
2. (MA:46) Mamparra m'gaiza
(MP:50) Mamparra m'gaiza

Leksia hizi zina maana ya kibarua anayefanya kazi ya kuchimba madini kwenye migodi.

Dhana ya uchimbaji madini inafahamika vyema miongoni mwa HP ya tafsiri. Iwapo mtafsiri angetumia kisawe cha mchimba madini au mfanyikazi wa migodi; dhana inayowasilishwa na leksia magaica na mamparra m'gaiza ingeifikia HP.

Kinyume na hivyo, uamuzi wa mtafsiri wa kutotafsiri leksia hizo katika MP, umesababisha maana ya leksia hizo kutoeleweka kwa HP ambayo haifahamu lugha ya MA.

Tatizo la tatu kuhusiana na leksia ni kwamba wakati mwingine mtafsiri hutapatapa anapoteua visawe vya kutumia katika kutafsiri baadhi ya leksia. Kwa mfano katika:

1. (MA:47) The train is back from "Migoudini"
(MP:50) Gari moshi linarudi kutoka migodini
2. (MA:46) the rand
(MP:49) Migodini
3. (MA:47) Mine
(MP:50) Migodini

Mtafsiri ametumia ile ile leksia moja, migodini kama kisawe cha maneno tofauti ya MA. Tukio hili linaonyesha kwamba mtafsiri aliyumbayumba katika kutumia hiyo leksia. Tatizo alilosababisha ni

la kutowasilisha vyema kwa HP jumbe halisi zinazobebwa na kila moja ya hizo leksia tofauti za MA.

'Migoudi' ni neno lililokopwa na lugha ya Kiswahili, kwa maana ya migodi, kutoka maeneo ya kusini mwa bara Afrika.

Hata hivyo, Rand, ni neno linalomaanisha eneo fulani kule Afrika kusini karibu na mji wa Jahanesburg, ambako kuna migodi mingi ya dhahabu. Kwa hivyo hili ni jina la eneo na wala sio kisawe cha migodi kama alivyochukulia mtafsiri.

Neno mine, vilevile halina ulinganano wa moja kwa moja na tafsiri migodi, kwa vile mine humaanisha kwa jumla, mahali popote Pale ambapo madini huchimbwa.

Migoudi, jinsi ilivyoelezwa katika tanbihi ya, (MA:47) ni dhana inayorejelea kundi maalum la watu, hasa wafanyikazi wanaoajiriwa kutoka mataifa na sehemu mbalimbali zinazopakana na eneo ambamo madini huchimbwa, kwa kawaida hao vibarua walilipwa ujira mdogo sana na hali yao ya maisha ilikuwa duni sana.

Migoudini, basi ina maana ya eneo kubwa sana lenye machimbo ya madini ambayo ni muhimu sana kiuchumi kwa watu wengi ambao maisha na utamaduni wao huhusiana moja kwa moja na eneo hilo.

Dhana hii ni tofauti na ya leksia Rand na mine, ambazo, hata hivyo mtafsiri alizitafsiri kama migodi.

Mifano mingine inayofafanua tatizo hili la kuyumba yumba kwa mtafsiri katika uteuzi wa visawe vinavyowakilisha leksia za MA ni kama ifuatayo.

4. (MA:61) Poetry
(MP:66) Utenzi
5. (MA:48) Poem
(MP:52) Shairi
6. (MA:64) African Poetry
(MP:69) Utenzi wa kiafrika
7. (MA:90) Fourth poem
(MP:99) Shairi la nne

Inavyodhihirika kupitia mifano hii (4-7), wakati mwingine mtafsiri hutumia neno/leksia shairi na wakati mwingine yeye hutumia leksia utenzi kama visawe vya dhana ile ile moja ambayo inahusu ushairi.

Shairi ndiyo leksia mwafaka zaidi inayoakisi dhana poem ya MA. Vivyo hivyo dhana poetry ingetoshelezwa zaidi na leksia ushairi na wala sio utenzi kama alivyoitafsiri mtaajumi katika MP.

Utenzi ni aina ya ushairi unaoweza kuimbika navyo sivyo ambavyo mwandishi wa MA alitaka kumaanisha kwa hadhira yake.

Huku kuyumbayumba kwa mtafsiri katika uteuzi wake wa visawe vya leksia zinazoakisi dhana za MA, kunamfanya kuwakanganya wasomaji wa MP. Wasomaji wanakosa kupata maana halisi kuhusiana na dhana poetry ambayo mtafsiri ameipotoa kimaana katika MP.

Tatizo la nne alilosababisha mtafsiri kuhusiana na leksia ni lile la kutumia leksia zisizo sahihi kimaana zikilinganishwa na leksia za MA. Mifano ifuatayo inaonyesha tatizo hili.

1. (MA:128) Come say to me.

"Here"...

(MP:138) Njo unionyeshe

"Angalia" ...

Katika kifungu hiki, tafsiri ya mshairi sio sahihi kwa vile say to me inafaa kutafsiriwa kama niambie na wala sio unionyeshe. Leksia 'Here', vile vile ingefaa kutafsiriwa kama 'hapa' na wala sio 'Angalia' kama alivyofanya mtafsiri.

2. (MA:60) Just adrum in the hot night of the tropics

(MP:65) Iliayo Afrika wakati wa usiku wa joto.

Leksia tropics, hurejelea sehemu za dunia baina ya miraba inayoizunguka dunia, ambayo hukadiriwa kufikia vipimo vya $23\frac{1}{2}^{\circ}$ kuelekea kaskazini na pia kusini mwa ukanda wa ikweeta. Kwa kawaida haya maeneo ya ulimwengu huwa na joto jingi sana.

Mtafsiri amekosea kwa kutafsiri leksia tropics kama Africa, kwa vile, Afrika ni bara ambalo halijajikita tu kwenye upeo wa miraba hiyo ya tropics.

Vilevile, kijiografia, eneo la tropics halipatikani tu katika bara la Africa, bali pia katika bara zingine kama Amerika-kusini.

Tafsiri hii inaikanganya HP, kwa vile sio leksia yenye maana inayolingana na ile ya MA. Ujumbe unaopitishwa na MP, unakuwa ni tofauti na ule wa MA.

3. (MA:43) Colourless banner
(MP:46) Bendera nveupe
4. (MA:69) ... from the Rovuma to the Incomati
(MP:75) Toka mto Zambezi hadi mto Inkomati
5. (MA:38) On the highside of a hemisphere ...
(MP:40) Upande mmoja wa dunia
6. (MA:139) Each with his own past
(MP:136) Kila mtu njia yake
7. (MA:69) I, player of presages on the keys of Chope
timbillas
(MP:75) Kutumia vyombo vya kabila la wachope
8. (MA:77) to the frank embrace of hope
(MP:84) Nafasi ya kweli ya matumaini
9. (MA:77) With leaves of the heart
(MP:84) Na kwa shangwe za moyoni
10. (MA:86) Voice gladdening with hot rhythms of the land
(MP:94) Zavuma nchi starehe na michezo

Kama inavyoonekana kupitia mifano hii, mafungu ya MA haya-
lingani kimaana na yale ya MP, hasa hizo leksia zilizopigiwa
mistari.

Katika mfano wa 3, colourless imepewa kisawe nveupe, ambayo
kwa hakika ni rangi maalum ambayo hailingani kimaana na hiyo
colourless ambayo ni dhana yenye maana -isiyo na rangi.

Katika mfanó wa 4, mtafsiri amegeuza jina la mto Rovuma na
badala yake akatafsiri jina hilo kama Zambezi ambayo si sahihi kwa

vile jina la MA na lile la MP hurejelea mito miwili tofauti.

Mfano wa 5, leksia highside, inafaa kumaanisha upande wa juu na sio upande mmoja kama ambavyo mtaajumi aliitafsiri.

Katika mfano 6, leksia his own past inafaa kumaanisha ukale wake na wala sio njia yake kama ilivyotafsiriwa.

Leksia presages katika mfano wa 7, inafaa kumaanisha, ishara inayoonya kuhusu tukio litakalotendeka baadaye, hasa tukio baya. Hivyo basi sio sawa mtafsiri kuipa leksia hiyo kisawe cha vyombo kwa vile maana zao hazilingani kamwe.

Katika mfano 8, frank embrace hailingani kimaana na nafasi ya kweli, bali ingefaa kutafsiriwa kama ukumbatio mkunjufu au kukumbatia kikweli na kiwaziwazi.

Inashangaza vilevile kwamba mtafsiri alitoa kisawe cha shangwe kwa leksia leaves ambayo inafaa kutafsiriwa kama matawi.

Gladdening katika mfano, 10 humaanisha, zachangamsha au zafurahisha na wala sio zavuma, kama ambavyo ilitafsiriwa kimakosa na mtafsiri. Vile vile hot rhythms of the land imetafsiriwa kama starehe na michezo ambayo inapitisha maana tofauti kabisa na ile ya leksia za MA.

Kwa jumla, haya matatizo tuliyoyajadili, husababishwa, aidha na hali ya mtafsiri kutokuwa mwangalifu au kutomakinika vya kutosha katika kung'amua ujumbe wa MA. Kwa hivyo anaweza kutoa visawe visivyolingana kimaana na vile vya MA, kwa HP.

3.6.2: MATATIZO YA SEMANTIKI

Tatizo la kwanza ni lile la mtafsiri kupotoka kimaana katika jaribio la kuufafanua au kuuweka wazi ujumbe ziada kwa mbinu za implikecha, inferensi au presaposisheni. Wakati mwingine maana anayojitokeza nayo huikanganya HP hata zaidi.

Kwa mfano:

1. (MA:53) the silk works
(MP:58) Mashamba ya miti ya nondo wanaotengeneza hariri

Jaribio la mtafsiri la kufafanua silk works. limesababisha utata zaidi wa kimaana katika MP, kwa vile ameelezea mambo mengi zaidi, yasiyohitajika kwa HP. Jambo hili linamfanya mtafsiri kutogonga ndipo katika ujumbe anaouwasilisha bali anaubabiababia tu.

2. (MA:60) Come bend over this soul of Africa
(MP:65) Inama uone uchungu huu wa Afrika

Mtafsiri hakuzingatia maana halisi ya kifungu cha MA. Alichukulia kiinferensi ya kwamba, this soul inaashiria uchungu ambao umelikumba bara la Afrika, kutokana na matatizo mengi ambayo watu wa bara hili wameyapitia kwa miaka mingi. Hatua hii ya kufasiri kiinferensi imesababisha ujumbe wa MA kutoifikia HP ya tafsiri, katika maana yake halisi.

3. (MA:78) Our song of sorrows
Our moments of despair
 (MP:85) Tulipokata tamaa
Mbele hatuoni - giza tupu?

Katika mfano huu, mtafsiri alisababisha kukanganyika kwa maana ya MA kwa vile aliyatafsiri mafungu hayo kulingana na jinsi alivyofikiria ujumbe uliashiria na wala sio kwakuzingatia maana ya moja kwa moja inayoeleweka ya kifungu hicho. Kwa hivyo songs of sorrows ingekuwa, nyimbo zetu za majonzi nayo moments of despair ingekuwa, nyakati za kukata tamaa. Alivyofanya mtafsiri ni kwamba aliyaweka MP katika lugha tamathali, hatua ambayo imeifumba maana ya MA badala ya kuiweka wazi kwa HP.

4. (MA:71) ... a forest, a macala tree
 (MP:78) ... mti mkubwa, kama misitu

Huenda, mtafsiri alikosa kupata kisawe cha kiswahili ambacho kingeakisi maana ya a macala tree, hivyo basi akaamua kuitafsiri kama mti mkubwa.

Tatizo la kufanya hivi ni kwamba katika mazingira ya hadhira ya MP, zipo aina nyingi za miti mikubwa, kwa hivyo hadhira hiyo haiwezi kwa njia yoyote ile kufahamu mti unaorejelewa katika shairi.

Kwa jumla ni kwamba HP inanyimwa na mtafsiri, maana halisi ya ujumbe wa MA.

5. (MA:89) Of the land called green
(MP:97) Katika nchi iliyoitwa huru

Ingawa green inapochukuliwa kimafulmbu inaweza kumaanisha au kuashiria mmea unaoota na kuleta matumaini ya kitu kipya miongoni mwa watu walioipanda mbegu.

Dhana hii iliyofumbika katika jazanda green inaweza kuwa na maana sawa na neno huru la MP. Hata hivyo, hatua hii ya kutafsiri maneno kulingna na dhana zinazoashiriwa, badala ya maana wazi wazi ya maneno hayo, kama ilivyo katika mfano huu, husababisha tatizo katika ujumbe unaowasiliswa kwa HP.

Hadhira hiyo italazimika kuufasiri ujumbe wa MP, kwa njia sawa na vile ambavyo mtafsiri aliufasiri. Jambo hili wakati mwingine haliwezekani kwa vile watu tofauti hufasiri jumbe mbali mbali kwa namna tofauti kulingana na tajriba zao tofauti. Hivyo basi maana katika MP hutatizwa.

Tatizo la pili la semantiki ni lile la mtafsiri kutoa tafsiri ambazo hudhoofisha na kuchujua maana asilia ya ujumbe.

Katika mifano ifuatayo, tatizo hili linadhihirika:

1. (MA:83) Apoem with Batuque and tchabeta and the badias of St. Catherine.

(MP:92) Shairi lenye starehe za ngoma
Na wanawake wa mtaa wa katarina

Tafsiri starehe za ngoma, kwa maana ya batuque and tchabeta, imesababisha maana ya kifungu hicho kufifia katika MP kwa vile maneno hayo hayarejelei tu starehe za ngoma kwa jumla bali humaannisha ngoma maalum ambazo huchezwa kulingana na mdundo fulani unaotambulika miongoni mwa watu wa sehemu za Angola.

Hali kadhalika neno badias halimaanishi wanawake kwa jumla bali humanisha wanawake wanaoshiriki katika ukahaba kama njia ya kujipatia riziki. Neno hilo hutumika sana kule Santiago.

Hivyo basi tafsiri alizozitoa mtaajumi, ambazo ni za kijumla, zimedhoofisha kwa viwango vikubwa, dhana zinazorejelewa na MA.

2. (MA:68) In the astral Capulana of an intangible sky

(MP:74) Imefunikwa na nguo inavopendeza

Dhana ya Capulana imedhoofishwa na mtafiri, katika MP ambapo ameitafsiri kama nguo inavopendeza. Tafsiri hiyo ni ya kijumla sana inapolinganishwa na maana halisi ya neno Capulana.

Capulana, ni aina ya nguo ambayo hufanana na kanga ambazo huvaliwa na wanawake katika maeneo ya waswahili. Hata hivyo Capulana, huvaliwa na wanawake wa jamii fulani zinazoishi kule Msumbiji. Ingekuwa bora zaidi iwapo mtafiri angechukua neno kanga kama kisawe cha capulana badala ya kusema tu nguo inavopendeza.

3 (MA:48) "Sunless gallery"

(MP:52) Kifungo

Anapotafsiri "sunless gallery" kama kifungo, maana ya kifungu hicho inadhoofika kwa vile, ile dhana ya kwamba kifungu hicho kinachozungumziwa ni mahali penye giza na pa kutisha haiwafikii wasomaji wa MP kwa vile neno kifungo hurejelea kwa jumla tu, mahali ambapo wafungwa huwekwa k.v. gereza, ilhali "sunless gallery" inaashiria zaidi kizuizi ambapo wafungwa wa kisiasa waliwekwa, wakiwa wametengwa na wale wafungwa wengine.

4. (MA:87) ever victorious in their death for life

(MP:95) katika ushindani

Wa kujizamisha katika starehe

Kwa maana ya moja kwamoja, victorious. ingefaa kutafsiriwa kama kufaulu ama kupata ushindi. Kwa njia hiyo, maana asilia ya ujumbe ingeifikia HP. Sababu zilizomfanya mtafsiri kuchukua neno ushindani kama kisawe cha victorious ni kama vile; kufasiri maisha katika mapana yake, ambapo kimantiki, binadamu hutambua ya kuwa maisha ni tukio linalohusisha mapambano na ushindani wa kila mara. Hata hivyo tungependa kusesitiza ya kwamba wakati mwingine ile maana halisi ya matini na wala sio maana itokanayo na ufasiri wa mtafsiri, ndiyo huhitajika zaidi kupitishwa kwa wasomaji. Mtafsiri akosapo kufanya hivyo kama katika mfano huu, basi maana ya ujumbe huchujuka.

Vilevile kifungu cha MA, in their death for life. ni fumbo lenye maana nzito ambayo inazidi, kujizamisha katika starehe. kama ilivyotafsiriwa.

Ufasiri huo, haukung'amua kikamilifu, dhana ya MA, na hivyo basi ufasiri huo ukaidhoofisha dhana hiyo. Maana halisi ya kifungu hicho haikuwasilishwa na mtafsiri ambaye tunaonelea anaamini ya kwamba ule ushindi unaotokana na harakati na ushindani katika maisha, hufikia kilele chake, watu wanapopata fursa ya kujizamisha katika starehe za maisha.

Kauli hii sio ya lazima katika uhalisia wa maisha ya wanadamu.

3.7.0: MATATIZO YANAYOSABABISHWA NA HALI YA MTAFSIRI KUTOMAKINIKA KATIKA LUGHA

Katika kiwango hiki tunachunguza maswala ambayo husababisha utata na ukengeusho kwenye MP kama vile maendelezo mabaya ya baadhi ya maneno; kutowasilishwa kwa ujumbe sahihi katika MP; mtafsiri kubuni upya ujumbe asilia na kisha kuupitisha huo ujumbe alioupotoa kimaana na wakati mwingine mtafsiri hukosea kwa kufasiri maana kimakosa.

Mara nyingi matatizo haya hudhihirika kupitia miundo ya sarufi, ngeli na uambishaji unaokiuka kaida za lugha pokezi.

3.7.1: MTAFSIRI KUWASILISHA UJUMBE USIOAFIKIANA KAMWE NA ULE
WA MA.

Mifano yote inayofuata inadhihirisha tatizo hili:

1. (MA:56) As if beyond the cinemas
no longing for your strange horizon, stirred

(MP:61) Kama kwamba haikuwako haja
Baada ya senema na mikahawa
kukumbuka uzuri wa nchi, Afrika

Mtafsiri amebuni upya kifungu cha MA huku akitafsiri vibaya strange horizon, kama uzuri wa nchi Afrika na kuongezea leksia mikahawa ambayo haikuwepo katika MA. Nyongeza hiyo haikufanywa kwa sababu yoyote maalum, na wala haikuimarisha maana ya MP, kwa namna yoyote. Kutomakinika huku kwa mtafsiri, kumemfanya kutoweza kuwasiliana inavyohitajika na HP.

2. (MA:124) discovering a new, the colours of the world

(MP:134) Tunafunguka macho tukigundua
Mambo mapya ya ulimwengu

Kupotoka kwa mtafsiri kimawasiliano kunaonekana katika mfano huu, kupitia kwa mafungu kama vile discovering ambayo ameifasiri kama tunafunguka macho na pia colours of the world ambayo ameitafsiri kama mambo mapya ya ulimwengu.

Maana ya MP imekengeushwa na matatizo hayo yaliyosababishwa na kutomakinika kwa mtafsiri kuhusiana na ujumbe anaouwasilisha kwa HP.

3. (MA:108) there is a message of justice

(MP:119) Yaenda kutafuta haki

Maana sahihi ya ujumbe wa MA ni; pana ujumbe wa haki. Kwa hivyo tafsiri yaenda kutafuta haki inazalisha maana isiyolingana kamwe na ile ya MA.

Tafsiri hiyo inawatatiza wasomaji kwa vile hawaelewi sababu za mtafsiri kusema haki yaenda kutafutwana hali MA yanaonyesha ya kwamba huo ujumbe wa haki ambao unarejelewa tayari upo.

Ukiushi wa namna hii, unaiathiri na hata kuibadilisha maana aliyoilenga mwandishi wa MA. Kifungu cha MA kinapolinganishwa na kile cha MP; kinaonekana kama kifungu tofauti kabisa, ambacho hakihusiani na kile cha MP kwa namna yoyote, na hali matarajio ya HP ni kwamba, ujumbe katika kifungu cha MP uwe wenye kulingana na ule wa MA.

4. (MA:83) A poem without words choked

(MP:91) Shairi lisiloeleza dukuduku

La wale wanaonyamaa kimya

Tafsiri ya A poem without words choked, haikuzingatia usahihi wa kimaana na pia ulingano na MA. Kwa hivyo badala ya kupitisha ujumbe unaorejelea dhana ya shairi lililojazwa kwa maneno kama inavyotakikana, mtafsiri amezalisha ujumbe tofauti usioidhihirisha dhana hiyo. Shairi lisiloeleza dukuduku ni tafsiri isiyoakisi na kupitisha dhana ya ujumbe wa MA.

5. (MA:67) With the futile creek-croak of the fat cicadas
(MP:73) Au vya chura mnene kijitoni

Kifungu cha maneno katika MA kinaashiria hali ya wingi na hali kile cha MP kinaashiria hali ya umoja. Hili ni tatizo la kutomakinika kwa mtafsiri katika LP au mtafsiri kutokuwa mwangalifu.

Vilevile maana ya mafungu hayo inatofautiana sana kwa sababu cicadas ni leksia inayorejelea aina ya mdudu mnene ambaye hupatikana zaidi katika maeneo ya joto ulimwenguni kama vile katika nyanda za tropiki. Mtafsiri hakuipitisha maana hii sahihi kwa vile aliitafsiri leksia hiyo kwa kisisawa Chura, ambaye kwa namna yoyote ile ni kiumbe tofauti sana na mdudu.

Tatizo hili la mtafsiri, limesababisha kupotoshwa kwa maana katika MP.

3.7.2: UAMBISHAJI MBAYA

Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi ambavyo hatua ya mtafsiri ya kuongeza viambishi fulani fulani katika baadhi ya maneno, bila ya uangalifu, huweza kugeuza maana ya naneno hayo na hatimaye kuathiri kifungu kizima, kimawasiliano na kisemantiki. Matatizo haya yanaonekana katika mifano inayofuata.

1. (MA:42) to see women
(MP:45) kuonana na wakeze

Uambishaji alioufanya mtafsiri katika mshororo wa MP umesababisha badiliko la maana katika kifungu hicho. Maana ya to see ni kuona, nalo neno women humaanisha wanawake.

Tatizo ni kwamba, mtafsiri anapoambisha-na, katika neno kuona anapata neno kuonana ambalo linarejelea kauli tofauti na ile ya neno la MA. Kuonana ni kauli ya kutendana ambayo si sawa na kuona, iliyo katika kauli ya kutenda.

Vivyo hivyo mtafsiri amesababisha tatizo kwa kutafsiri neno women kama wakeze. Huu uambishaji wa, -ze, umeibadilisha kauli ya neno hilo, kutoka wanawake, na kuifanya kuwa nomino yenye dhana ya umilikishi.

HP inapata ujumbe, usiolingana na ule wa MA; ya kwamba wanawake wote wanaozungumziwa ni wa mtu mmoja kwa sababu wakeze ni ufupisho wa wake zake. Hii maana haikuashiriwa na ujumbe wa MA, bali ni maana iliyozalishwa na uambishaji mbaya alioufanya mtafsiri.

2. (MA:129) Bullets are beginning to flower
(MP:139) Risasi zimeanza kuchanua

Kifungu cha MA, kipo katika hali ya kuendelea kwa kitendo, wakati uliopo. Katika kiswahili sanifu kifungu hicho kinapaswa kuwa risasi zinaanza kuchanua na wala sio risasi zimeanza kuchanua.

Kuambishwa kwa, _me_, badala ya, _na_, katika neno la MP, zimeanza, kumekifanya kifungu hicho kuwa katika kauli ya kitendo ambacho kimeshatimilika ingawa sio muda mrefu uliopita. Kauli hii ni tofauti na ile ya MA, na hivyo basi maana ya mafungu hayo mawili inatofautiana pia, kwa sababu hiyo ya uambishaji usiozingatia ulinganu baina ya MA na MP.

3. (MA:72) and was intermingled with Mozambique

(MP:79) Akajiunganisha kabisa na Msumbiji

Katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili sanifu, uambishaji kama alioufanya mtafsiri katika neno la MP lililopigiwa mstari, huruhusiwa bila shaka yoyote k.m. akajitambulisha.

Kinyume na hivyo, neno akajiunganisha, halikuambishwa vizuri nalo linahisika kama halikuzingatishwa na mtafsiri, kaida za lugha hii pokezi ya kiswahili. Vilevile kisarufi sio mwafaka kusema akajiunganisha. Neno sahihi badala ya hilo ni kujiunga iwapo kitendo kinamrejlea mtu, na iwapo ni kitu kisicho na uhai, neno sahihi lingekuwa kuunganisha (vitu hivyo).

Ni muhimu kutambua ya kuwa tatizo hili la uambishaji potofu limesababishwa na kukosa kwa mtafsiri, kuzingatia kaida za kisarufi za LP.

3.7.3: TAFSIRI ISIYOZINGATIA KAIDA ZA KIMSINGI ZA LP.

Kupitia kwa mifano inayofuata, tatizo hili linadhihirika:

1. (MA:52) in the long grass
(MA:56) Tulipojificha peke yetu manvasini
2. (MA:113) Wild grass
(MP:124) Manyasi

Mtafsiri amesababisha tatizo la kisarufi kwa kuongeza kiambishi awali ma-, mwanzoni mwa neno nyasi, katika jaribio la kuashiria wingi wa neno grass, kwenye MP.

Lugha ya kiswahili sanifu hairuhusu kuongezwa kwa kiambishi ma-, mwanzoni mwa neno nyasi sawa na maneno mengine pia katika ngeli ya N- ambayo kwa kawaida hayachukui viambishi vinavyoashiria wingi. Neno nyasi hubakia vivyo hivyo aidha katika umoja au wingi.

3. (MA:55) Rocking these other people
(MP:59) Inayowabeba wale wengine

Kiashiria these ni kisawe cha hawa, ambacho ni kiashiria cha nafsi ya kwanza, kauli ya wingi.

Hivyo basi mtafsiri amesababisha tatizo la kisarufi kwa kutoa kiashiria wale katika MP, kuwa kisawe cha these. HP inapitishiwa ujumbe usio sahihi kwa vile neno wale, huashiria nafsi ya tatu, kauli ya wingi, ambayo ni tofauti na kauli ya neno la MA.

Sio jambō linaloruhusiwa katika lugha ya kiswahili sanifu kwa kauli na nafsi za viashiria tofauti (ya kwanza, ya pili au ya tatu) kubadilishwa na nyingine kiholela, kama alivyofanya mtafsiri.

4. (MA:64) a man, sleepless, dreams
(MP:70) Mtu mume kakosa usingizi

Sio jambo la kawaida kuwasikia wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu wakitoa maneno kama vile mtu mume, kama kisawe cha a man kwa vile kaida za kisarufi za lugha hii hazikubali utunzi wa maneno kama hayo.

Badala ya mtu mume, ingefaa zaidi iwapo mtafsiri angetumia neno mwanamme, ambalo linatosheleza maana ya neno hilo la MA.

Ubunifu huu alioufanya mtafsiri katika MP, umekiuka usahihi wa kisarufi wa lugha ya kiswahili sanifu. Lengo la mtafsiri, aidha halikuwa kutaka kudhihirisha ubingwa wake wa kuchezea maneno au kubuni miundo mipya ya upangiliaji wa maneno katika LP. kwa namna inayoweza kuwavutia zaidi wasomaji.

Bila shaka hili ni kosa la kisarufi lililotendwa na mtafsiri.

5. (MA:101) They are coming swiftly
(MP:111) Nakuja kwa haraka

Katika mfano huu, ulinganifu wa kisarufi baina ya kifungu cha MA na kile cha MP haupo. Licha ya kwamba MA inaonyesha ya kwamba wale ambao wanazungumziwa ni wengi, nao wako mbali, MP inaonyesha kwamba ni mtu mmoja/msemaji.

Mtafsiri amesababisha tatizo la kuwakanganya wasomaji wake kwa kutafsiri, kifungu they are coming ambacho katika MA kiko katika nafsi ya tatu, wingi, hadi kifungu nakuja kilicho katika nafsi ya kwanza, umoja.

SURA YA NNE.

4.0: MATATIZO KATIKA VIWANGO VYA MUKTADHA, UTAMADUNI, MAZINGIRA NA MASWALA MENGINE YANAYOSABABISHWA NA LUGHA.

4.1: UTANGULIZI.

Katika sura hii ya tasnifu yetu tunazingatia matatizo yanayofungamana na maswala tofauti tofauti, ambayo kwa jumla yanarejelea uziada lugha na vipengele vyake mbalimbali ambavyo mtafsiri hana uwezo juu yavyo.

Vipengele hivi vinavyosababisha tofauti baina ya LA na LP humwathiri mtafsiri kwa kiwango kikubwa sana, katika kazi yake, naye hana uwezo wa kujiepusha navyo.

Tumechukua mwelekeo ambao umemulika jinsi ambavyo mtafsiri hutatizika anapojaribu kushughulikia maswala hayo ya muktadha, utamaduni na mazingira.

4.2.0: MATATIZO KATIKA KIWANGO CHA MUKTADHA.

Maana na mawasiliano ya vipengele katika tukio la lugha, zinapotazamwa kimuktadha, jambo ambalo hudhihirika ni kwamba, hali ya kijumla ya jamii zinazohusishwa katika tafsiri, jinsi ya kuelewa ujumbe katika jamii hizo, jinsi zao za kufasiri maana, na kuwasiliana kwao, humtatiza mtafsiri.

Iwapo mtafsiri hatayaelewa vyema maswala haya kuhusiana na jamii hizo, basi atatatizika sana katika upitishaji maana na kuwasilisha ujumbe wa MA kwa hadhira ya MP.

Utata mwingi hubainika katika MP, hasa mtafsiri anapolazimika kutumia ufundi wake wa kubuni upya, ili kutosheleza mahitaji ya HP. Dhana anazozitafsiri zinapokuwa hazieleweki au hazipo kabisa miongoni mwa jamii ya HP, hatari inayozuka ni kwamba mtafsiri anaweza kupitisha maana inayowatatiza wasomaji wake.

Mifano ifuatayo inafafanua matizo kuhusiana na muktadha.

- 1 (MA:83) A poem without exiles complaining
(MP:91) Ya wafungwa waliojikalia kimya

Tafsiri ya leksia exiles kama wafungwa, imefanywa na mtaajumi kwa kuzingatia muktadha wa kisiasa katika enzi za ukoloni ambapo serikali za kikoloni zilikuwa na mazoea ya kuwahukumu vifungo, viongozi wa kiafrika walioongoza harakati za kisiasa dhidi ya mifumo katili ya serikali za kikoloni.

Mara nyingi viongozi kama hao, walikamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uhaini na kuhatarisha usalama wa taifa.

Ili kuhakikisha ya kwamba viongozi hao wametengwa na jamii zao walizozitetea; serikali nyingi za kikoloni zilichukua hatua kali ya kuwapeleka viongozi hao uhamishoni.

Kwa mfano Mzee Kenyatta wa Kenya alipelekwa uhamishoni mahali paitwapo Lokitaung, katika eneo la kaskazini magharibi mwa taifa la Kenya. Nelson Mandela naye alipelekwa uhamishoni kule Robben Island, kisiwa mojawapo katika bahari ya Atlantiki, kusini kidogo mwa mji wa Cape Town.

Katika enzi ya wakoloni wa kireno, wafungwa wa kisiasa kutoka kwa mataifa waliyoyatawala, walipelekwa/waliamishwa hadi visiwa vya SaoTome, ambavyo vilikuwa na kambi na magerenzi za wafungwa kutumika vifungo vyao. Katika kambi kama hizo, wafungwa waliteswa sana kwa kufanyishwa kazi za sulubu na kutendewa ukatili mwingi.

Kwa kuelewa hivyo, mtafsiri amelazimika kuutilia maana ni muktadha huo, ambao kwao, hao 'exiles', kwa hakika sio tu watu waliokwenda uhamishoni jinsi tunavyoweza kuwarejelea katika muktadha wa kisasa; bali ni wafungwa wa kisiasa.

Licha ya kulazimika kutumia leksia isiyolingana na ile ya MA, mtafsiri ameweza kuwasilisha ujumbe ulio na thamani sawa na ile ya MA. Tatizo ni kwamba, HP, inalazimika kuufahamu uziada huu wa kimuktadha ndipo iweze kung'amua maana ya MP. Lau sivyo maana itakayofasiriwa na HP itakuwa tofauti kabisa na ile ya MA.

2. (MA:123) the word of command in the bush and in the towns
smashing the PIDE network.

(MP:133) Amri PIDE, kunguni wa Mreno

Akronimu PIDE imehawilishwa kutoka MA hadi MP, bila ya kutafsiriwa. Hii ni kwa sababu, kutafsiriwa kwake kungehitaji maelezo mengi ya ziada kujumuishwa kwenye MP, kwa vile PIDE haieleweki kimaana katika muktadha wa HP ya tafsiri.

Mtafsiri amejitahidi awezavyo katika kuongezea akronimu hii PIDE, maelezo 'kunguni wa mreno' ili, kuwapunguzia wasomaji wa MP, matatizo ya kuuelewa ujumbe unaowasilishwa.

PIDE ni neno lililotumika katika kuwarejelea polisi wa siri na makachero waliotumiwa na serikali ya kikoloni ya wareno katika kuchunguza na kujaribu kuangamiza shughuli za kisiasa za wanaharakati wa ukombozi katika mataifa yaliyotawaliwa na hao wareno.

Akronimu hii, kwa vyovyote vile, ni neno lililojikita katika muktadha wa kisiasa wa enzi za ukoloni kwenye mataifa hayo yaliyotawaliwa na wakoloni wa kireno.

Kwa vile HP ya tafsiri ni jamii ya watu walio katika muktadha tofauti wa kijamii na wa kisiasa, neno PIDE ni ngeni kwao. Hata kama mtafsiri angeitafsiri akronimu hiyo na kuongezea maelezo mengi zaidi, maana yake halisi ingali ingewatatiza wasomaji wa MP.

Tunavyoonelea ni kwamba mtafsiri hakuwa na uwezo wa kukwepa hali hii ya tofauti za kimuktadha baina ya hadhira ya MA na ile ya MP, kwa hivyo ilimbidi kuhawilisha akronimu hiyo. Hata hivyo tatizo limesalia, licha ya uhawilishaji, kwamba HP ya tafsiri imebakia katika giza la kutafuta maana halisi ya akronimu PIDE, bila ya kuipata.

- 3 (MA:69) I, once a zulu chief.
(MP:75) Nami zamani nilikuwa mtemi.

Katika mfano huu, mtafsiri amelazimika kutumia neno mtemi kama tafsiri ya a zulu chief. kwa sababu neno hilo la MP, ndilo ambalo linaeleweka katika muktadha wa hadhira anayoitafsiria.

Mtemi, ni msamiati uliokopwa na lugha ya kiswahili kutoka kwa jamii mojawapo ya watu wa kule Tanzania. Neno lenyewe hutumiwa katika kumrejelea kiongozi wa jamii hiyo tangu jadi.

Ingawa wazulu ni watu tofauti sana na hao watu wa Tanzania, mtafsiri aliamua kulitumia neno mtemi kama tafsiri ya a zulu chief kwa sababu ya dhana hiyo ya kiongozi wa jamii inayowasilishwa na neno mtemi.

Fauka ya thamani ya neno la MP kuwa sawa na ile ya neno la MA, tatizo lingali kwamba mtemi ni leksia tofauti na zulu chief, hasa katika maana zao tambuzi.

4.2.1: MATATIZO KUHUSIANA NA UTAMADUNI

Tunavyofahamu ni kwamba, tamaduni hutofautiana baina ya jamii mbalimbali za watu. Hizo tamaduni huwa zimejengwa na jamii katika mifumo bainifu inayodhihirika kupitia mila, desturi, kaifa, miiko na mafundisho yanayopitishwa kimapokezi, tangu jadi.

Hali hii ya kutofautiana kwa jamii za watu kiutamaduni, humlazimisha mtafsiri wakati mwingine kutumia maneno yanayoakisi mahitaji ya kimaana na kimawasiliano ya HP, licha ya kwamba maneno hayo sio visawe vya moja kwa moja vya maneno yaliyotumiwa kwenye MA.

Mifano hii hapa chini inafafanua tatizo hili:

1. (MA:81) for right, for peace, for friendship
(MP:89) Haki, amani na undugu

Katika utamaduni wa jamii ya HP ya tafsiri, maisha yaliyojikita katika kaida za ujamaa, yalithaminiwa sana. Kwa sababu hiyo, watu wote hutazamana kama ndugu na hushirikiana sana katika shughuli zao za kila siku maishani.

Mtafsiri, amezingatia utamaduni wa watu anaowatafsiria ndipo akaiwasilisha leksia friendship kama undugu. Sababu kubwa iliyomfanya kutafsiri hivyo ni kwamba alitaka kuwasilisha hiyo dhana ya uhusiano wa karibu, uliopo baina ya watu katika jamii ya HP, na hasa jinsi ambavyo urafiki wa karibu huchukuliwa kuwa jambo muhimu sana.

Katika uziada wake kimaana, neno ndugu, huashiria utangamano, ushirikiano na urafiki wa karibu, baina ya wale ambao huitana vile. Kwa kufanya hivyo, mtafsiri ameweza kuwasiliana vyema na HP. Hata hivyo undugu sio kisawe cha moja kwa moja cha friendship.

2. (MA:61) an assegai
 (MP:94) Mkuki uliosanwa kwa moto mkali
3. (MA:86) Farolim, the ingombata meetings
 (MP:94) Waliokuwamo katika Farolim
 Au mikutano ya Ingombata
4. (MA:94) beautiful like coals of mica in the quizumba
 nights.
 (MP:73) Unavyometameta siku ya giza.

Neno assegai katika mfano wa pili ni la kizulu. Hilo neno hurejelea aina maalum ya mkuki mfupi uliotumiwa na wapiganaji vita wa kabila hilo, miaka mingi iliyopita.

Hili neno linahusiana na utamaduni wa hao wazulu kwa vile ni kifaa kilichotumiwa nao na wala sio jamii nyingine tofauti. Kifaa hicho hakijulikani katika utamaduni wa jamii ya HP ya tafsiri, kwa vile wao walikuwa na mikuki yao iliyotofauti na hiyo assegai.

Mtafsiri hangeweza kuiwasilisha dhana hiyo kwa sababu ya tofauti hizi za kiutamaduni, ila tu kujaribu kadri ya uwezo wake, kutoa maelezo kama alivyofanya katika MP. Maelezo hayo hayatoshelezi kikamilifu dhana hiyo ya assegai.

Katika mfano wa tatu, maneno farolim na Ingombata, haya kutafsiriwa katika lugha ya MP. Haya maneno yanarejelea mikutano ya aina maalum ambayo yalifanywa na jamii za watu wa sehemu za kusini mwa Afrika.

Hiyo mikutano ilifanywa kulingana na utamaduni wa watu hao. Dhana zinazozalishwa na maneno yanayotaja aina hizo za mikutano haziwezi kubainishwa na mtafsiri katika utamaduni wa jamii ya lugha pokezi. Sababu hii ndiyo ambayo ilimfanya mtafsiri kutotafsiri maneno hayo.

Tatizo ni kwamba, kuhawilisha maneno hayo bila ya kuyatafsiri, jinsi alivyofanya mtafsiri, kumesababisha maana ya maneno hayo kutowafikia wasomaji wa MP.

Mfano wa nne unaonyesha jinsi ambavyo mtafsiri alilazimika kupitisha ujumbe ambao umepunguza thamani ya MP kimaana, kwa vile amefutilia mbali maneno kama vile quizumba ambayo hurejelea aina ya ngoma inayochezwa na watu katika utamaduni maalum.

Quizumba ni aina ya ngoma inayochezwa na watu wa jamii za pwani mwa Angola na pia miongoni mwa watu wa jamii za kule Brazili, ambao waliamishwa hadi sehemu hizo, kutoka pwani mwa Angola, katika kipindi cha biashara ya watumwa.

Dhana hii ya kitamaduni haingeweza kutafsiriwa katika LP, ambayo utamaduni wake ni tofauti sana na huo wa jamii hizo za Angola na Brazili. Ilivyo ni kwamba eneo la Afrika Mashariki, halikuwa na maingiliano mengi sana ya kitamaduni na eneo la Angola.

Kwa hivyo dhana za kitamaduni kama vile quizumba hazina visawe wa katika lugha ya jamii ya MP.

5 (MA:41) "Ve nera', ne vera' cufa?"

(MP:44) "Ve nera', ne vera' cufa"

6 (MA:80) - Oio kalunga ua mu bungele

(MP:87) Oio kalunga ua mu bungele

Mtafsiri amehawilisha mafungu ya maneno katika mifano ya tano na sita, kutoka MA hadi MP kwa sababu hata yeye mwenyewe, inavyoonekana, hangeweza kuelewa maana ya mafungu hayo ambayo yamenukuliwa kutokana na nyimbo zilizoimbwa na jamii za watu katika mojawapo ya mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni wa kireno.

Mfano wa tano hasa unarejelea kifungu mojawapo cha wimbo wa zamani kabisa juu ya kifo. Nyimbo kama hizo ni turathi za kijamii, ambazo hupokezwa kiutamaduni tokea kizazi kimoja hadi kingine.

Mtafsiri hangeweza kuyatafsiri mafungu hayo, kwa vile hatari iliyopo ni kwamba thamani ya mafungu hayo katika lugha zao za asili ingechujuka kabisa.

4.2.2: MATATIZO KUHUSIANA NA MAZINGIRA

Mazingira hurejelea hali ya anga na ya kimaumbile inayoizunguka eneo fulani la kijiografia. Mazingira huathiri maisha ya wanadamu kwa namna nyingi. Kwa mfano, mimea,

wanyama na vitu tofauti tofauti hupatikana katika maeneo mbali mbali kwa kutegemea mazingira ya mahali. Baadhi ya wanyama, mimea na vitu, hupatikana katika mazingira maalum na ya kipekee.

Kutokana na hali tofauti za kimazingira, wanadamu hujitokeza na maneno mbalimbali ya kutajia viumbe, mimea na vitu wanavyoviona katika mazingira yao.

Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi ambavyo tofauti za kimazingira baina ya MA na MP humwathiri mtafsiri katika utekelezaji wa kazi yake.

1. (MA:51) Your eyes gentle as the macongue
(MP:55) Macho yamekurembuka kama harita

Mtafsiri alilazimika kutafsiri neno macongue kama harita. Maneno haya yote hurejelea mimea. Hata hivyo ni mimea inayotofautiana, kwa ajili inakua katika mazingira yanayotofautiana.

Katika mazingira ya hadhira ya MP, mmea harita ndio ambao hupatikana kwa wingi. Mmea wenyewe huzaa mbegu nyeusi, za mviringo kama gololi. Macongue nayo hupatikana kwa uchache sana.

Tatizo ni kwamba harita sio kitu kimoja na macongue licha ya kwamba mimea hiyo inafanana kiumbo.

Mtafsiri alilenga zaidi kuwasiliana na HP kuliko kufikia maana halisi ya neno macongue katika lugha pokezi.

2. (MA:52) the hyenas and the buffalo,
the caymens and the river fish could hear
(MP:56) Fisi, mbogo na samaki wa mtoni
Wote wangepata isikia

Caymens ni mnyama wa jamii ya mamba ambaye hupatikana katika sehemu za kati na kusini mwa bara la Marekani. Kiumbo, huyu mnyama hufanana na mamba ambao hupatikana mahali kwingi barani Afrika.

Mtafsiri hata hivyo, badala ya kutumia kisawe mamba, aliamua kufutilia mbali neno hilo, caymens. Sababu ya kufanya hivyo ni kwamba alishindwa kupata kisawe mwafaka ambacho kingeakisi dhana hiyo katika LP, kwa vile mnyama huyo hapatikani kamwe katika mazingira ya jamii ya LP.

Hata kama angetumia neno mamba kama tafsiri ya caymens, dhana ya mnyama huyo ingali haingewafikia wasomaji wa MP kikamilifu, kwa sababu maana halisi ya neno mamba ni tofauti na ya neno caymens, licha ya kufanana kwa wanyama hao kiumbo.

3. (MA:116) It is time to understand
that macala and malapa grow on strong trees

(MP:127) Wakati umefika tukumbuke

Kwamba Makala na malapa ni matunda

Maneno yaliyohawilishwa na mtafsiri ambayo tumeyapigia mistari katika mfano huu wa tatu, yanatumika kutajia aina za matunda ambazo zinakuwa katika mazingira maalum ya jamii zinazotumia LA.

Inavyoonekana ni kwamba mtafsiri alitatizika katika kuyatafsiri majina hayo ya matunda, kwa sababu matunda hayo hayapatikani katika mazingira ya jamii zinazotumia LP.

Tatizo ni kwamba uhawilishaji alioufanya mtafsiri hauna faida kwa hadhira ya MP, ambayo haielewi au hata kufahamu aina hizo za matunda, kwa vile hayamo katika mazingira yao. Mtafsiri hangeweza kupata kisawe chochote mwafaka cha kutajia aina hizo za matunda.

4.3.0: MATATIZO KUTOKANA NA MASWALA MENGINE KATIKA LUGHA

Matatizo katika kiwango hiki yanahusiana na utamathali katika lugha pamoja na matumizi ya mbinu nyinginezo za kifani ambazo hutumiwa katika kuunda na kurembesha kazi za sanaa.

Mbinu kama hizi, vilevile husaidia katika uwasilishaji wa ujumbe kwa namna inayovutia zaidi miongoni mwa wasomaji. Baadhi ya tamathali za usemi anazoweza kutumia mwandishi katika ubunifu wake ni kama; methali, tashibihi, istiari, tauria, tashihisi, jazanda, kinaya, chuku, balagha n.k.

Lugha inapotumika kitamathali, maswala mbalimbali ambayo sio rahisi kuyabainisha kwa kutumia lugha ya kawaida, huweza kushughulikiwa. Kwa mfano taswira inaweza kujengwa na msanii, vilevile anaweza kupunguza makali kuhusiana na baadhi ya mambo anayoyazungunzia.

Mbali na faida nyingi zinazoweza kuhusishwa na matumizi ya lugha kitamathali; yapo matatizo mengi sana katika kutafsiri lugha ya tamathali za usemi na kunga nyinginezo za usanii kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Miongoni mwa matatizo hayo ni kama ifuatayo.

4.3.1: TAFSIRI YA SEMI BILA YA KUZINGATIA THAMANI YA MA.

Katika mifano hii, mtafsiri hakuweza kuuwasilisha ujumbe ulio na thamani sawa na ile ya MA, kimaana na kimawasiliano

1. (MA:49) tangled with a song of steel on steel
to the beat Joao-Tavesse-went to the mines

(MP:53) Magurudumu va chuma kusuga reli
Nacho chuma kingine, kusema
Joao-Tavesse-Kenda-Migodini,

Hali ya magurudumu ya gari moshi kutoa sauti yenye rithimu fulani kila yanapogusana na chuma za reli; imeelezwa kwa njia ya usemi katika kifungu cha MA, a song of steel on steel.

Kupitia kwa kifungu magurudumu va chuma kusuga reli kwenye MP, huo usemi unafifia na mdundo unaohisika katika MA unakosa kuwasilika vyema katika MP, kwa vile LA na LP zinatofautiana kimiundo.

2. (MA:77) and horror touches the naked face

(MP:83) Na hofu zikaingia

Kuonekana nyusoni mwa watu

Kifungu cha MA kinaonyesha uumbuji wa mwandishi asilia kupitia kwa mbinu ya tashihisi ambayo ameitumia katika kutia mvuto zaidi kwenye ujumbe anaouwasilisha. Hata hivyo katika MP, mvuto huo umedhoofika kutokana na sababu kwamba, huo utashihisi wa MA umepotea. MP yameuwasilisha ujumbe huo kwa kuzingatia zaidi lugha ya kawaida kuliko jinsi yalivyofanya MA ambayo yalijikita zaidi katika utamathali.

3 (MA:112) As high as the Savannah

(MP:124) Marefu kimo cha mtu

Ulinganisho unaofanywa na mwandishi wa MA ambao ni tashbihi, unatofautiana sana na ule unaofanywa na mtaajumi katika MP. Huo utashbihi haupo kamwe katika MP.

Kigezo kilichotumiwa na mtafsiri katika kulinganisha urefu wa Savannah na kimo cha mtu, hakibainiki waziwazi. kwa hivyo dhana inayorejelewa na MA haipatani kithamani na ile inayorejelewa na MP. Mafungu hayo yanawasilisha maana mbili tofauti ambazo hazihusiani hata kimuktadha.

Savannah ni uwanda wenye majani usio na watu au pori yenye nyasi ndefu na visitu vidogo vidogo. Kwa upande mwingine, kimo cha mtu, ni kifungu kisicho na maana maalum kwa vile hapana kipimo maalum kilichowekwa kwa minajili ya kusawazisha vimo vya watu; badala yake vimo hivyo hutofautiana miongoni mwa watu mbalimbali kulingana na sababu tofauti tofauti.

4 (MA:114) the cry, the cry

(MP:125) Ule ukelele

Utakriri unaoonekana katika MA, umetoweka katika MP, kwa vile mtafsiri hakurudiarudia kifungu hicho. Vilevile maana halisi ya MA ambayo imefungamana na dhana ya kilio, haiwasiliki kupitia kwa kisawe ukelele alichokitumia mtafsiri.

Thamani za MA na MP haziafikiani kwa sababu ya matatizo hayo ya tofauti baina ya lugha zinazohusika, katika misingi ya kiusemi kitamathali.

4.3.2: KUBADILISHA TAMATHALI MOJA YA SEMI NA NYINGINE

Katika mifano inayofuata, tatizo hili linadhihirika. Sababu kubwa inayomfanya mtafsiri kubadilisha aina moja ya tamathali ya semi na nyingine ni kwamba, tofauti zilizopo katika utamaduni wa lugha ya MA na ile ya MP, husababisha ugumu wa kutafsiri baadhi ya tamathali kwa tamathali kama zizo hizo.

Jambo ambalo mtafsiri hujaribu kulitimiza wakati anapo badilisha tamathali moja na nyingine ni kuhifadhi dhana na thamani ya ujumbe asilia. Hatua hii, hata hivyo, husababisha kukengeuka kwa maana asilia ya baadhi ya tamathali.

1. (MA:62) ... and thunder in his voice

(MP:67) Na sauti kali kama radi

Tatizo katika mfano huu ni kwamba mwanudishi wa MA alitumia mbinu ya istiara ambayo kwayo kitu ambacho kinazungumziwa hulinganishwa na kingine kwa kuashiria ya kwamba, kinachozungumziwa kwa hakika ndicho hicho kitu kingine.

Tafsiri inayozingatia, huo uistiari uliopo kwenye MA, ungezalisha kifungu kama vile, sauti yake ilikuwa na radi, lakini jambo hili lingesababisha kufifia kwa dhana inayorejelewa na MA.

Kwa hivyo mtafsiri alitumia ulinganisho wa aina ya tashbihi katika MP kupitia kwa kifungu sauti kali kama radi ambapo kilinganishi, kama, kimechukua nafasi ya istiara iliyokuwepo katika MA.

2. (MA:67) ... my white teeth of ivory

(MP:73) Meno yangu meupe kama pembe

Kifungu cha MA, kimewasilishwa kwa mbinu ya semi inayoashiria ya kwamba meno yanayosifiwa kwa ajili ya uweupe wao, yalikuwa ni ya pembe za ndovu na wala sio kama, pembe za ndovu jinsi ambavyo MP inaonyesha.

Mbinu iliyotumiwa katika MA ni istiari nayo imebadilishwa kuwa tashbihi katika MP. Hizi ni aina tofauti za kulinganisha ambazo zina thamani tofauti kwa vile istiari husababisha uhusiano wa karibu sana kuonekana baina ya vitu vinavyolinganishwa, ilhali tashbihi hutumia viunganishi kama 'mithili ya', 'kama ' n.k. ambayo haileti uhusiano wa karibu sana baina ya vitu vinavyolinganishwa vile ambavyo istiari hufanya.

4.3.3: KUTUMIA LUGHA YA KAWAIDA KUTAFSIRIA MAFUNGU YA KITAMATHALI.

Katika mifano ifuatayo, tatizo hili linaonekana.

1. (MA:53) ... Life has written with the pen of centuries
(MP:57) Kilichoandikwa maishani
Kwa kalamu ya karne nyingi
2. (MA:102) We shall go dressed in peace
(MP:112) Tutatembea tukiwa na amani
3. (MA:102) along roads, - twisting snakes
(MP:112) Barabara zinazopinda-pinda
4. (MA:87) there was youthful calm among the old people, more
then goodnes - it was love
(MP:95) Ukawako utulivu miongoni mwa watu, utulivu, lakini si
uzee

Kulingana na mifano yote, mafungu yaliyopigiwa mistari, yaliwasilishwa kitamathali katika MA ilhali katika MP, utamathali wa vifungu hivyo vyote umepotea kabisa kwa sababu ya kutafsiriwa kwa vifungu hivyo kwa kutumia lugha ya kawaida ya maongezi, isiyotosheleza ubunifu wa mwandishi wa MA.

Hali hiyo ya mtafsiri kutumia lugha ya kawaida katika MP, ilisababishwa na kauli ya kwamba lugha asilia na lugha pokezi zinatofautiana katika namna ya kuwasilisha ujumbe.

SURA YA TANO

5.0: HITIMISHO

Katika tasnifu hii tumechunguza kwa undani, maswala yanayohusiana na tafsiri kwa jumla. Pamoja na hayo, tumefanya uchanganuzi wa matatizo ambayo hudhihirika katika matini yaliyotafsiriwa. Tumejikita katika diwani; Risasi Zianzapo kuchanua (1975), ambayo ni kazi mojawao miongoni mwa diwani chache zilizotafsiriwa kutoka lugha ya kiingereza hadi kiswahili sanifu.

Mbali na kuchunguza matatizo hayo mbalimbali, ambayo huathiri tafsiri katika viwango tofauti tofauti vya kiujenzi katika lugha; tumetazama pia kwa upana; dhana za tafsiri, mawasiliano, muktadha na maana.

Tumepata ya kwamba ufahamu wa kutosha na msingi imara wa kila mojawapo ya dhana hizo, una nafasi muhimu sana katika kumwezesha mtafsiri yeyote yule kutekeleza shughuli zake bila ya kukumbana na matatizo mengi katika kazi anayoishughulikia.

Tunapendekeza ya kwamba wasomi wa taaluma ya tafsiri wajiingize katika uchunguzi zaidi kuhusiana na dhana hizi, kwa vile hatua kama hiyo itasaidia sana katika uimarishwaji wa viwango vya kazi za tafsiri zitakazofanywa na wataalamu watakaolewa vyema dhana hizi katika tafsiri. Kauli hii ni muhimu sana kwa vile sio kila mtafsiri ana utaalamu kuhusiana na dhana hizi au somo lote la tafsiri.

Tunasadiki ya kwamba mwongozo tulioutoa katika sura ya kwanza, hasa katika kipengele cha nadharia tulizozitumia kiujumishi, utawachochea wachunguzi wengine wa taaluma ya tafsiri, kufanya uchanganuzi wa maswala yanayodhihirika katika matini zinazoshughulikiwa. Chunguzi hizo za miaka ijayo, tunapendekeza zitekelezwe kwa kutumia nadharia za kisasa zaidi, mathalani uchanganuzi wa usemi, ambao huhusisha vipengele vingi zaidi kuliko nadharia za hapo awali ambazo zilifungamana zaidi na vipengele vya maana na mawasiliano katika lugha.

Wakati mwingi, kujikita huko katika nadharia hizo za awali pekee, kuliwafanya watafsiri wengi kutatizika kwa namna nyingi. Hali hii isiyopendeza hubainika pale ambapo mtafsiri analazimika kutafsiri tu lugha na sio ujumbe kwa vile hajajimudu vilivyo katika taaluma hii.

Kulingana na uchunguzi tulioufanya, ilibainika kwetu ya kwamba matatizo yanayoathiri tafsiri yanaweza kimsingi kutazamwa katika vitengo viwili vikuu.

Kwanza ni kitengo cha matatizo ambayo yanaweza kujumulishwa kama; yaliyosababishwa na upungufu upande wa mtafsiri. Matatizo ya aina hii tumeyashughulikia katika sura ya tatu.

Pili ni kitengo cha matatizo ambayo yanaweza kujumulishwa kama; yaliyotokana na hali ya lugha, ambayo mtafsiri hakuwa na uwezo wa kujiepusha nayo, mathalani tofauti za utamaduni wa kijamii, vifaa vya kitamaduni, imani za watu na tafauti za miundo ya kijamii. Pamoja na hayo kunazo tofauti za mazingirakijiografia na tafauti za muktadha kihistoria, miongoni mwa tafauti nyinginezo.

Kauli nyingine muhimu iliyodhihirika kwetu katika kazi hii ni kwamba; mtafsiri, ni msanii, sawa na alivyo mwandishi wa matini asilia.

Kwa hivyo mtafsiri vilevile hujitwika jukumu la kutathmini kazi anayoishughulikia, hajaribu kujaribu kumwelewa mwandishi wa makala asilia na msomaji anayemtafsiria na wakati mwingine hujiingiza katika kubuni upya na kufanyia marekebisho kazi anayoishughulikia.

Lengo la mtafsiri katika kufanya mambo hayo yote huwa ni kujaribu kujitokeza na kazi bora zaidi, ambayo inakidhi mahitaji ya hadhira anayoitaafsiria, hasa yale mahitaji ya kuwasilisha ujumbe sahihi kimaudhui na wenye kulingana kimaana na ule wa MA.

Tafsiri ya diwani Risasi Zianzapo Kuchanua (1975) imefaulu kwa kiwango kikubwa sana, fauka ya matatizo kama yale tuliyoyajadili katika sura za tatu na nne.

Tathmini yetu imeonyesha ya kwamba tafsiri yenyewe imefaulu kwa vile, ujumbe wa MP umedumisha, kwa kiwango kikubwa, thamani inayolingana na ile ya MA. Vivyo hivyo utata wa kimaana katika baadhi ya mafungu ya MP, haukuvuka mipaka na kuvuruga kabisa ujumbe unaowasilishwa katika MP.

Kwa mujibu wa tasnifu hii, haipotesia zetu zimeweza kupimwa. Kwanza, tumepata ya kwamba zipo tofauti nyingi sana hasa kuhusiana na LA na LP kama tulivyoonyesha katika viwango mbalimbali vya matatizo ya lugha.

Pili ni kwamba, baadhi ya matatizo katika tafsiri yalisababishwa na mtafsiri mwenyewe kwa sababu ya kutozingatia

vilivyo kaida za dhana zinazohusishwa katika tafsiri.

Tatu, tumeweza kutathmini mafanikio ya mtafsiri wa diwani; Risasi Zianzabo Kuchanua (1975) na kuona ya kuwa alifanikiwa vilivyo, licha ya matatizo machache tuliyoyataja katika kazi yake.

Nne, ni kwamba katika sura ya pili tumeshughulikia dhana zinazohusishwa na somo la tafsiri, kwa lengo la kuziweka wazi zaidi kwa wale ambao watahitajika kuzifahamu, hasa watafsiri wenyewe. Dhana hizo ni kama msingi ambao kwao shughuli za kutafsiri zimejengeka, hivyo basi ni mwafaka; zieleweke kwa wasomi wa taaluma hii.

Tano, tumeonyesha jinsi ambavyo ubunifu wa mtafsiri na utashi wa kuboresha matini anayoishughulikia unaweza kumfanya kuongezea au kupunguza baadhi ya vipashio katika MP wakati wa kutafsiri. Mambo haya huathiri tafsiri kwa namna nyingi, kama tulivyojadili katika sura ya tatu.

MAREJELEO:

- Ali, C.W. (1981); "The problem of translating from English into Swahili as exemplified by V.O.K. News Items" Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Bateman, J. (1995); "Context - Based Analysis as a Basis for Translation" pt.1 katika, Barnwell, K. (ed); Notes On Translation, Vol.9. No 1, Summer Institute of Linguistics inc, Dallas, U.S.A.
- Beekman, J. and Callow, J. (1974); Translating The Word of God, Zondervan Pub. House, Michigan, U.S.A.
- Bradley, V. (1991); "Assumptions Involved in Interpretive Decisions" katika, Barnwell, K. (ed); Notes On Translation, Vol.5 No.3, S.I.L Inc., Dallas, U.S.A.
- Brown, G, and Yule, G. (1983); Discourse Analysis, Cambridge University Press, Cambridge.
- Catford, J.C. (1965); A Linguistic Theory of Translation. O.U.P, London.
- Crystal, D and Davy, D. (1969); Investigating English Style, Longman, London.
- Crystal, D. (1987); The Cambridge Encyclopedia of Language, Cambridge University Press, U.S.A.
- Culy, M.M. (1993); "The Top-Down Approach To Translation; katika Barnwell, K. (ed) Notes On Translation, Vol.7 No.3, S.I.L. Inc. Dalls, U.S.A.
- Farrell, T. (1995); "Translating Implicit Information in the light of Saussurean, Relevance and cognitive Theories," katika Barnwell, K. (ed) Notes On Translation, Vol.9 No.1, S.I.L. Inc., Dallas, U.S.A.
- Forster, L. (1958); "Translation, an Introduction;" katika Aspects of Translation, University of London Communication Research Centre.
- Goerling, F. (1996); "Relevance and Transculturation;" katika Barnwell, K. (ed), Notes On Translation, Vol.10 No.3, S.I.L. Inc., Dallas, U.S.A.
- Guenther, F. and Guenther - Reutter, M. (1978); Meaning and Translation, Gerald Duckworth and Co. Ltd., Great Britain.

- Gutt, E.A. (1988); "From Translation To Effective Communication",
katika Olson, R.D. (ed) Notes On Translation.
S.I.L. Inc. Dallas, U.S.A.
- Hartman R.R.K. and Stork, F.C. (1972); Dictionary of Language and
Linguistics. Applied Science Pub. Ltd, London.
- Hatim, B. and Mason, I. (1990); Discourse and the Translator
London/Newyork.
- Kelly, L.G. (1979); The True Interpreter: A history of
Translating Theory and Practice in the West. Basil
Blackwell Co. Oxford.
- Larson, M.L. (1984); Meaning-Based Translations: Aguide to
Cross-language Equivalence. University Press of
America Inc. U.S.A.
- Louw, J. (1984); "A semiotic Approach to Discourse Analysis with
Reference to Translation Theory;" U.B.S.
Translation Workshop 15-26 May, 1984, Stuttgart.
- Macdonell, D. (1986); Theories of Discourse. Basil Blackwell Co.
Newyork/Glasgow.
- Makay, J.J. (1973) (ed); Exploration In Speech Communication.
Charles E. Meril. Public Co. Columbus, Ohio.
- Massamba, D.P.B. (1990) (ed); Kamusi ya Isimu na Lugha. Educational
Pub. and Distributors Ltd., Dar es Salaam.
- Mikai, A. (1976) (ed); Toward A Theory of Context in Linguistics
and Literature. Mouton, The Hague/Paris.
- Newmark, P. (1981); Approaches to Translation. Pergamon Press.
- (1988); A Textbook of Translation. Prentice Hall
Newyork.
- Nida, E. (1964); Towards A Science of Translating: with special
reference to principles and procedures Involved in
Bible translating, Leiden Brill Co. Netherlands.
- (1975) Componential Analysis of Meaning.
Mouton Pub. The Hague/Paris/Newyork.
- Shitemi, N.L. (1990) "Tafsiri: Uteuzi wa mtafsiri", Tasnifu ya MA
Chuo Kikuu cha Nairobi.

- Steiner, G. (1975); After Babel: Aspects of Language and Translation. Oxford University Press, London.
- Thomson, G. (1988); "What Sort of Meaning is Preserved in Translation" Katika, Olson, R.D, (ed) Notes On Translation Vol.12 No.1, S.I.L. Inc. Dallas, U.S.A.
- Wales, K. (1989); A Dictionary of Stylistics. Longman, London/Newyork.
- Zaja, J.O. (1986) "Fasihi Tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili: Matatizo na Athari zake", Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.